

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Tisa – Tarehe 5 Februari, 2016

(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. RAMADHAN I. ABDALLAH - KATIBU MEZANI: Hati za kuwasilisha Mezani.

HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima Nchini kwa kipindi cha Mwaka unaoishia tarehe 31 Disemba, 2014 (*The Annual Insurance Market Performance Report for the Year ended 31st December 2014*).

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:

Taarifa ya Mwaka ya Chuo Kikuu cha Dodoma kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 (*The University of Dodoma Annual Report 2013/2014*).

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete Mbunge wa Busokelo sasa aulize swalii lake.

Tatizo la Maji – Jimbo la Busokelo

MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Busokelo hasa katika Kata za Kandete, Isange, Lutebe Lwangwa, Mpata, Kabula, Mpombo, Lufilyo Kambasegela, Ntaba, Lupata, Itete, na Kisegese wanakabiliwa na tatizo kubwa la maji safi na salama; na kuna maeneo mengi ambayo mabomba uyamepita lakini maji hayatoki kutokana na kukosekana kwa matenki ya maji:-

(a) Je, ni lini Serikali itatatua kero hiyo ya maji kwa kujenga matenki ya maji kwenye Kata hizo?

(b) Mji wa Lwangwa ni Makao Makuu ya Halmashauri mpya ya Busokelo na kuna ongezeko kubwa la watu ukilinganisha na miundombinu ya maji iliyopo; je, Serikali ina mpango gani wa kujenga miundombinu mipy ya uzalilshaji wa maji kwenye eneo hilo jipya la mipango miji?

NAIBU WAZIRI (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2014/2015, Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo ilipokea shilingi milioni 907 ambazo zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji ya Mpanda katika Kata ya Lupata na miradi wa maji Kasyabone na Kisegese katika Kata ya Kisegese. Miradi hii inahusisha ujenzi wa matanki yenye ujazo wa mita za ukubwa 90 kwa Kata ya Lupata na matanki wawili ya mita za ukubwa 45 kila moja katika Kata ya Kisegese. Katika bajeti ya mwaka 1015/2016 Serikali imefanikiwa kupeleka shilingi milioni 171.94 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji katika Kijiji cha Kanyebole Kata ya Kabula, Ilamba katika Kata ya Kambasegela na kijiji cha Mpata katika Kata ya Mpata.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Lwangwa tayari Halmashauri imekamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa mradi wa maji kutoka chanzo cha maji Mano Sekondari. Katika bajeti ya mwaka 2015/2016 Serikali imetenga shilingi milioni 280 ili kuanza utekelezaji wa mradi huu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakibete swali la nyongeza

MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE: Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini kwa mujibu wa swali nilivyouliza pamoja na majibu ambayo yametolewa ni dhahiri kwamba kwa vijiji ama Kata ambazo amezisema mimi mwenyewe ni shahidi kwamba kuna hela ambazo hazijafika hadi sasa hivi na katika jibu lake la msingi amesema zimefika. Kwa mfano Kata ya Mpata, nimepeleka mabomba zaidi ya milioni 10 lakini Serikali mpaka sasa hivi haijatoa chochote. Mheshimiwa Waziri unaweza ukathibitishia wananchi wa Mpata kwamba hizo fedha zimefika kule? Hilo ni swali la kwanza.

Swali la pili, kuna baadhi ya Kata ya Ntaba, kijiji cha llamba wananchi pamoja na wakazi wa eneo la pale wananyang'anyana maji, wananchi na mamba, na zaidi ya wananchi kumi na moja wameshauawa na mamba ama kuliwa na mamba kwa sababu ya kutafuta maji, je, Serikali inatoa tamko gani kwa ajili ya wananchi hawa na ikizingatiwa kwamba kuna mradi ambao umeshafanyiwa upembezi yakinifu tangu mwaka 2008 hadi leo hii kwa thamani ya shilingi milioni 100, haikufanya kitu chochote.

NAIBU WAZIRI (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Naibu Spika, asante.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa taarifa aliyosema kwamba fedha hazijafika ni kwamba ngoja nita-cross check vizuri katika Ofisi yangu nijue ni nini kilichotokea lakini kikubwa ni nini? Ni kwamba kuna changamoto ya upelekaji wa fedha, siyo mradi huo tu isipokuwa maeneo mengi sana, fedha zimeenda kwa kususua na hivi karibuni ndiyo maana Waziri wa Maji juzi juzi alikuwa anazungumza kwamba kutokana na kususua kwa kupeleka fedha katika miradi ya maji na miradi hii mingi sasa mingine ilikuwa imesimama, sasa Serikali iliamua kwamba ile *outstanding payment* ambazo zilikuwa zinakaribia karibuni bilioni 28, kwamba fedha hizi sasa zipelekwe katika maeneo mbalimbali ilimradi wale Wakandarasi walio-demise mitambo waweze kuendelea.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba nikuambia kwamba nitazifuatilia kwa karibu ilimradi kwamba huu mradi lengo letu liweze kufanikiwa na wananchi waweze kupata huduma ya maji.

Lakini sehemu ya (b) ni kwamba kuna changamoto ya wananchi wanakamatwa na Mamba. Kwanza nitoe masikitiko yangu sana katika eneo hilo, kwa sababu kama watu wanaliwa na mamba ina maana kwamba ni changamoto kubwa, tunapoteza jamii ya Watanzania.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba nikiri kwamba nimesikia hili na nakumbuka tulifanya *discussion juzi juzi* kwamba katika ziara yangu

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nitakapokuwa nimeenda katika Mkoa wa Mbeya nimesema kipambele katika Jimbo lako la Busokelo litakuwa ni sehemu mojawapo ambayo nitaenda kutembelea ilimradi mambo haya yote kwa ujumla wake tuweze kuyatazama vizuri tukiwa site na kuweze kupanga mipango mizuri, mwisho wa siku wananchi wa Jimbo hili waweze kupata huduma ya maji, kila mtu aweze kujiona ana faraja na nchi yake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa pale nyuma, samahani naomba ujitambulische

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Naibu Spika, Naitwa Willy Qambalo Mbunge wa Jimbo la Karatu.

Kwa kuwa, matatizo ya maji yaliyoko Busekelo yanafanana kabisa na matatizo ya maji yanayoukumba Mji wa Karatu na vijiji vinavyouzunguka. Na kwa kuwa Mji wa Karatu unakua sana kutohuna na shughuli za utalii zinazoendelea katika maeneo ya jirani. Je, ni lini Serikali itamaliza kabisa matatizo ya maji katika Mji wa Karatu na vijiji vinavyozunguka?

NAIBU WAZIRI (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu huyu tukiri kwanza Busokelo haifanani na Karatu kwa sababu kule Busokelo kuna mamba, na naamini Karatu hakuna mamba. Lakini kubwa zaidi ni jinsi gani kama Serikali itajielekeza kuhakikisha Mji wa Karatu unapata maji kwanza nikiri kwamba mionganoni mwa Miji ambayo Tanzania tunaitegemea katika suala zima la uchumi ni Mji wa Karatu, kwa sababu ni center kubwa sana ya utalii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba Serikali kupitia Wizara ya maji katika programu ya pili tunayoenda nayo ambayo imeanza hii Januari, tumeweka kipaumbele katika Mji Mikakati yote ambayo kwanza ina vivutio vya Kitalii, lakini ni source kubwa sana ya uchumi wa nchi yetu kuipa kipaumbele katika suala zima la huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri wazi kwamba katika suala zima la utalii kama nilivyosema awali, Karatu ni Mji tunaoutegemea sana. Kwa hiyo suala hili tunalilchukua kwa ujumla wake, Wizara ya Maji halikadhalika Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, tutahakikisha jinsi gani tutaipa kipaumbele. Ile miradi ambayo imeanza Singida haijakamilika vizuri, au ni jinsi gani tutumie vyanzo vingine ili mradi tupate maji katika Mji wa Karatu, wananchi wa Karatu waweze kupata manufaa katika nchi yao.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tu, maswali yanayoulizwa ya nyongeza yawe mafupi, ikiwa ni pamoja na ya muuliza swali. Lakini pia Mawaziri mjibu kwa kifupi kwa sababu kila swali limetengewa dakika

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

sita tu. Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mombasa sasa aombe swali ijibewe.

Na.103

Kero ya Ushuru wa Mazao na Mifugo

MHE. DAVID E. SILINDE aliuliza:-

Wakati wa Kampeni za Urais mwaka 2015 wananchi wa Mombasa walipewa ahadi ya kutatuliwa kero ya ushuru wa mazao na mifugo kwenye vizuizi na minada:-

(a) Je, mpaka sasa Serikali imefikia hatua gani katika kushughulikia kero hii?

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya mwenendo mbovu wa ukusanyaji wa ushuru huo?

NAIBU WAZIRI (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mombasa lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ushuru wa mazao hutozwa kwa mujibu wa sheria ya fedha za Serikali za Mitaa Sura Na. 290 kwenye eneo ambalo zao hilo huzalishwa na kuuzwa. Kwa mujibu wa sheria hii ushuru unatozwa kwa mnunuzi wa mazao kutoka kwa mkulima asilimia tatu hadi asilimia tano ya bei ya gharama (farm gate price). Aidha, kwa upande wa ushuru wa Mifugo, ushuru huu hutozwa mnadani au sokoni baada ya mifugo kununuliwa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasisitiza na kuwataka Wakurugenzi wote wa Halmashauri kuhakikisha kuwa wanazingatia sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia utaratibu wa utozaji na ulipaji wa kodi katika ushuru husikia.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kuuliza maswali mado mawili.

Moja ya kero inayowakuta wafugaji wanapokuwa minadani, inatokea mahali mtu amekwenda kuuza bahati mbaya akiwa pale mnadani hajauza mfugo wake, na anapotoka pale anadaiwa ushuru wakati hajapata hiyo fedha. Sasa nilitaka nifahamu kauli ya Serikali juu ya wale wote ambao wanashindwa kuuza mazao ama mifugo yao katika maeneo hayo?

Swali la pili, je, ni kiwango gani ambacho mtu anapaswa kulipa, kwa sababu kuna watu wanatoka mashambani labda ana mahindi wanakwenda nyumbani kwao kuyatunza. Sasa wakikutana na kizuizi, mtu ana gunia mbili, gunia tatu anaambiwa lazima alipe ushuru hata kwenye yale mahindi ya kutumia.

Je, ipi ni kauli ya Serikali juu ya hili jambo? Ahsante.

NAIBU WAZIRI (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa

Naibu Spika, ni kweli katika mazoea ya kawaida watu wengine wanapeleka mazao yao sokoni, lakini kwa bahati mbaya wakifika pale wanakosa kuyauza. Ina maana na concept ya ushuru wa mazao, maana inataka mtu akishauza, yule mnunuzi sasa maana yake anatakiwa alipia ule ushuru. Lakini kama hajauza ukimwambia kwamba yule mkulima sasa aweze kutoa ushuru maana yake unambana mkulima. Na kauli ya Mheshimiwa Rais alipokuwa katika kampeni alizungumza wazi kwanza lengo lake ni kutoa huu usumbufu wa ushuru mdogo mdogo ambao unamkabili mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa zaidi nawahimiza Watendaji wetu hasa katika Halmashauri, jinsi gani wabainishe kwamba katika maeneo yao kuna watu hawa wa kawaida ambao wanaenda kuuza. Kuna mfanya biashara mkubwa ambaye anakuja kuchukuwa mazao pale site, akishachukua lazima alipie ushuru. Lakini yule mtu anayefanya kazi ya kuchuuza kwa ajili ya maisha yake tu hili ni jambo ambalo ni suala zima kuwaelekeza watendaji wetu katika Halmashauri zetu watafanya vipi kuondoa kero hii kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni kwa kiwango gani, nadhani suala la pili sikulipata vizuri lakini kikubwa zaidi ni nini. Ni kwamba mifugo yote inayopelekwa pale eneo la mnada, ndiyo maana nimesema sjjalipata vizuri swali la pili, tuangalie kwamba kwa sababu sheria ndiyo inaelekeza kati asilimia tatu mpaka asilimia tano, sasa mtu anapoenda kuuza mfano ana ng'ombe wake mmoja, ng'ombe wake wawili, ndiyo nimesema hapa utaratibu mkubwa unaotakiwa ni katika Halmashauri husika. Kwa sababu tunajua Halmashauri nyingine zinategemea asilimia karibuni 70 ya mapato yake katika ushuru wa mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jinsi gani kama Baraza la Madiwani pamoja na Watendaji wao watafanya kuangalia mazingira ya kijiografia katika eneo husika ili kuwasaidia wananchi hali kadhalika kuongeza uchumi katika Halmashauri zao.

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa kuwa katika Halmashauri zetu, hususani Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kumekuwepo na tatizo kubwa sana la ushuru huu na unaleta matatizo makubwa na kwa kuwa kuna ahadi ya Rais kwamba hizi shughuli ndogondogo zitaangaliwa upya, je, Serikali sasa iko tayari kuziagiaza Halmashauri zote ziangalie upya maeneo ambayo kuna usumbufu mkubwa na ushuru huu, ili marekebisho yafanywe haraka na wananchi wasipate bugudha ikiwemo Wilaya ya Mvomore?

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake ya ufasaha, na mimpongeze Mheshimiwa Murad kwa ufuatiliaji wake kwa masuala yanayohusu Jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kama ambavyo nilisema wakati nachangia, tunakaa na wenzetu wa TAMISEMI pamoja na Wizara zingine ambazo zinahusiana na sekta ambazo zinahusu mambo ya makato makato na tulishasema tunayafanya kazi mambo ya makato yote ambayo yanamgusa Mkulima na wafanyabiashara wadogowadogo. Lakini kwa leo nitamke tu kwamba kwa yale makato ambayo hayako kisheria, kwa makato ambayo yanawagusa wakulima ambayo hayako kisheria kuanzia leo hii wale wanaohusika waondoke na tamko hili kwamba wayaache, yale ambayo yako kisheria tunaenda kufuata utaratibu na kuangalia kama yote yabaki ama yabaki kiasi ili kuweza kuhakikisha kwamba tunawapa unafuu wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yale hayako kisheria na yale ambayo hayahusiani moja kwa moja na uendelezaji wa zao husika hayo yakome moja kwa moja kufuatana na kwamba yamekuwa yakiwapa mzigo wakulima bila kuleta tija katika kuongeza uzalishaji wa zao husika. Na tutachambua moja baada ya lingine na yale ambayo yanaafikiwa kwa kupitia makubaliano ya wadau wahusika, wasikubaliane wao na kuanza kuyatumia mpaka wapate ridhaa ya Wizara kwamba kuna mambo haya wamekubaliana na sisi tuweze kupima umuhimu wa kuwepo makato hayo katika uendelezaji wa zao husika. (Makofij)

NAIBU SPIKA: Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mbunge wa Mtambile sasa aulize swali lake.

Na.104

Ajira Inayatokana na Sekta ya Viwanda

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM aliuliza:-

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ajira iliyotarajiwa kuongezeka kutoptokana na ukuaji wa sekta ya viwanda haijafikiwa hasa baada ya viwanda vingi kubin afsishwa na kuachwa bila kuendelezwa:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu hili?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nia njema kabisa Serikali ilibin afsisha viwanda na mashirika ya umma ikiwa na matumaini kuwa sekta binafsi ingeliweza kuendesha taasisi hizo kwa faida na kulipa kodi kwa Serikali, kuzalisha bidhaa au huduma na kutoa ajira kwa wananchi. Pamoja na malengo hayo Serikali ililenga kuachana na shughuli za biashara ikielekeza nguvu zake katika shughuli zake za msingi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Masoud, makampuni mengi yaliyobin afsishwa hayakufanya vizuri, ikiacha mfano wa makampuni machache yakiwemo *Tanzania Breweries*, Morogoro Polister ambayo inaitwa *Twenty First Century* na *Tanzania Cigarette Company*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathimini inayoendeshwa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina juu ya viwanda, mashamba na mashirika ya Serikalil yaliyobin afsishwa kuanzia mwaka 1992 inadhihirisha ukweli tunaoujua kuwa wengi kati ya waliyopewa taasisi hizo hawakutekeleza mikataba ya mauziano kikamilifu. Hivyo tunawafutilia kwa karibu wale wote waliopewa mashirika ya umma kwa utaratibu wa ubin afsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu ni kuhakikisha makampuni yote haya yanazalisha kwa tija ili tupate bidhaa, kodi ya Serikali na ajira kwa wananchi wa Tanzania. Wale wote watakaobainika kukiuka makubaliano yaliyomo katika mikataba ya awali, hatua stahiki zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuvitwaa viwanda au mashirika hayo na kutafuta Wawekezaji mahiri wa kuviendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutimiza adhma ya kutoa ajira kwa Watanzania, Wizara inafanya yafuatayo chini ya viwanda vidogo na vya kati unaoshirikisha SIDO na Halmashauri za Wilaya na Mikoa tunahamasisha shughuli za ujasiriamali ikiwa ni pamoja na kuanzisha viwanda vya kuongeza thamani mazao na kilimo, uvuvi na ufugaji huku Mikoani.

Pia kupitia mamlaka zetu za EPZA, TIC na NDC tunakaribisha na kuwaongoza wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika shughuli za kutoa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ajira zaidi. Serikali kupitia Wizara yetu inaboresha mazingira ya uwekezaji hali itakayowajenga imani wawekezaji na kupelekea kupanua shughuli zao zaidi za kibiashara kupitia njia hii ajira zaidi itaongezeka.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nina maswali mawili ya nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko mengi ya muda mrefu kwa wafanyakazi viwandani kupewa mishahara midogo lakini zaidi maneno ya kuudhi kwa wamiliki wa viwanda jambo ambalo halikubaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuulize Mheshimiwa Waziri, je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuunda Tume Teule ya kufuatilia malalamiko ya wafanyakazi hawa?

Swali la pili, katika jibu la Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wale wote watakaobainika kukiuka makubaliano yaliyomo katika mikataba ya awali hatua stahiki zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuvitwaa na kutafuta wawekezaji mahiri wa kuviendeleza hivyo viwanda.

Kwa kuwa viwanda vya korosho vilivyobinafsishwa miaka 1970 na 1980 ambapo Serikali ilikopa kutoka Italia na Japan dola milioni 20 na viwanda hivyo hadi leo haviendelezwi wamiliki wake wanajulikana. Sasa tatizo nini kwa Serikali mnaelewa kila kitu tumekuwa tukisema muda mrefu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa uliza swali.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Je, nini mkakati wa ziada wa kuhakikisha kwamba viwanda vya korosho vimebinafsishwa kule Mtwara na Serikali mkatoa kwa vigogo wengine mnaowajua kwa bei chee! Je, viwanda hivyo ni lini vitarudi kwa wananchi?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika viwanda kuna malalamiko na kama mnavyojua tunao ndugu zetu wanafanya kazi viwandani, sioni haja ya kuunda Tume, Wizara yetu ikishirikiana na Wizara ya Ajira tumeanza kazi ya kufuatilia masuala haya na Kamishna wa Kazi yuko ana kazi maalum ambapo tutahakikisha kwamba wafanyakazi wetu wanatendewa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaeleze wawekezaji, sisi tunatengeneza viwanda kutengeneza ajira, kuzalisha bidhaa na kuwafanya mlipe kodi hatutengenezi viwanda kusudi waje kuteseka watu katika nchi yao, huo ndiyo msimamo wa Serikali na tunawahakikisha tushirikiane Waheshimiwa Wabunge, ninyi ndiyo macho yetu mtushauri na mtuelekeze.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutoa viwanda, viwanda vile viliuzwa kisheria, nimeshasema mara tatu bei waliyolipa ni pamoja na masharti ya kuzalisha bidhaa kwa tija, kutoa ajira na kulipa kodi.

Kwa hiyo, kama ulimuuzia kisheria utamnyang'anya kisheria na niwahakikishie watu wanaotoka kwenye ukanda wa kulima korosho hakuna tatizo viwanda vitafanya kazi. Pamoja na hivyo wako wawekezaji wako tayari kuwekeza kwenye kutengeneza korosho, yaani korosho inatoka pale kiwandani inaingia mikononi mwa mteja tuna-add value, na tutatoka hapa tunakwenda kuza Ulaya siyo tunatoka hapa tunauza India, India ipeleke Ulaya. Tunakwenda moja kwa moja sokoni na kazi hiyo naiweza tushirikiane. (Makof)

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nikushukuru sana kwa kunipa fursa na kwa sababu ni mara yangu ya kwanza nazungumza tangu nichaguliwe tena kuwa Mbunge wa Arumeru Mashariki na mimi niwashukuru Wanameru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nassari tafadhali uliza swali la nyongeza.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, unapoongelea suala la ukuaji wa viwanda huwezi ukaacha kuongelea habari ya viwanda ambayo vilikuwemo lakini leo hii havifanyi kazi. General Tyre Arusha kilikuwa ni kiwanda pekee cha kuzalisha matairi Afrika Mashariki. Mwaka juzi ndani ya Bunge hili nimejibiwa na Mama Nagu hapa kwamba *in less than a year* kiwanda kingerudi kifanye kazi, mwaka jana nimejibiwa ndani ya Bunge hili na Mheshimiwa Janeth Mbene kwamba kufikia mwezi wa 11 mwaka jana kiwanda cha General Tyre kingerudi kufanya kazi.

Sasa na mimi niiulize Serikali ya hapa kazi tu, kwamba ni lini kiwanda cha General Tyre kitarudi kufanya kazi kwa sababu tumechoshwa na ahadi za muda mrefu ndani ya Bunge hili na wananchi wa Mkoa wa Arusha amba walikuwa wanapata ajira ndani ya viwanda vile leo wako nyumbani na matairi tunanunua Korea, India na Japan, lini General Tyre litaanza kufanya kazi?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, General Tyre kinachoendelea General Tyre ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, General Tyre imeshatwaliwa aliyekuwa mbia mwenzetu mwenye asilimia 26 tumemlipa chake kiwanda ni chetu, kinachoendelea ni kurekebisha mitambo yote ya umeme. Lakini mitambo iliyokuwepo kwa ushindani wa sasa ni *absolute zimepitwa* na wakati. Tulikuwa tunatengeneza tyres zenye tube, sasa hivi soko linakula tubeless kwa hiyo, tunapaswa kuleta mitambo mingine. Lakini tunatafakari tuende vipi tutafute mbia mwingine au tutafute mtu wa kumwajiri afanye kazi. Kwa hiyo, sasa hivi

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kinachofanyika ikitoka Government Notice NDC itakwenda kupewa pesa bilioni 60 na itafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Catherine Magige amelifuatilia suala hili tumelizungumza sana, siyo suala la dakika moja naomba Mheshimiwa Mbunge uje au umuone Mheshimiwa Catherine Magige akueleze shule niliyompa masaa matatu kuhusu General Tyre. *General Tyre is coming* na iko kwenye score board yangu, nitapimwa kwa General Tyre. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (Makofi/Kicheko)

Na. 105

Matatizo Yanayowakabili Wakulima wa Tumbaku Urambo

MHE. MARGARET S. SITTA aliuliza:-

Mfumo wa sasa wa kuwashudumia wakulima wa zao la tumbaku wa Wilaya ya Urambo na Mkoa wa Tabora kwa ujumla una mapungufu mengi yanayowaletea wakulima usumbufu kama vile bei za pembejeo kuwa kubwa kutokana na kuagizwa nje na riba kubwa za benki, masoko ya tumbaku kutokuwa na uhakika na hatimaye kusababisha kushuka thamani ya tumbaku, bei inayobadilika pamoja na uchache wa wanunuzi:-

(a) Je, ni kwa nini hasara inayotokana na matatizo hayo ibebwe na mkulima peke yake?

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kuondoa matatizo hayo ili mkulima wa tumbaku anufaike na kilimo na hatimaye ajikwamue kiuchumi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvu kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa yapo maeneo mbalimbali yanayomkosesha mkulima mapato. Maeneo haya ni pamoja na mfumo wa usambazaji pembejeo uliokuwa na mianya mingi inayosababisha madeni hewa, baadhi ya viongozi wa vyama kukopa fedha nyingi kupita uwezo wa vyama wa kuzalisha tumbaku na kadhalika. Kwa sasa Serikali imebadili mfumo huo na kuelekeza wagavi wa pembejeo hizo kuzifikisha moja kwa moja kwenye vyama vya msingi tofauti na utaratibu wa awali wa kupitisha pembejeo kwenye vyama vikuu.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Aidha, ili kuwa na uhakika wa soko kilimo cha tumbaku nchini huendeshwa kwa mkataba kati ya wanunuzi na wakulima. Hivi sasa bei hupangwa kabla ya msimu wa kilimo kuanza ili mkulima ajue bei na kiasi anachotakiwa kuzalisha. Tatizo la soko na bei mara nyingi huwakumba wale wakulima wanaozalisha tumbaku bila kuwa na mikataba ambapo hujikuta tumbaku yao ikikosa soko au wakipewa bei ya chini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kukabiliana na changamoto zinazomkabili mkulima wa tumbaku. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha mfumo wa upangaji wa bei ya tumbaku ambapo wakulima upendekeza bei yenye tija kwao na kuiwasilisha kwa wanunuzi kupitia vikao vya Halmashauri ya Tumbaku yaani *Tobacco Council*. Bei hiyo hujadiliwa na hatimae kufikia muafaka. Mfumo huu wa upangaji wa bei umeanza kutumika rasmi msimu wa mwaka 2015/2016. Sanjari na maboresho ya mfumo huu Serikali inaendelea na jitihada za kuongeza wanunuzi wa tumbaku kutoka China ili kuongeza ushindani kumwezesha mkulima kupata bei nzuri. Aidha, Serikali itapitia tozo za pembejeo zinazoingia nchini na kuangalia uwezekano wa kuziondoa ili kumpunguzia mkulimba gharama ya uzalishaji.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri amekiri kwamba mfumo uliopo una matatizo katika kumhudumia mkulima. Lakini Serikali inashiriki kikamilifu katika kupanga bei katika mfumo mzima. Sasa kwa kuwa Serikali inashiriki kwa kupitia wakala wake bodi au council, je, Serikali haioni kwamba inawajibika kubeba sehemu ya hasara anayopata mkulima?

Kwa kiasi gani mmefaulu kupata wanunuzi zaidi kutoka China ili soko liwe la haraka na wakulima wanufaike?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, *Tobacco Council* au Halmashauri ya Tumbaku inawakutanisha wadau mbalimbali wa sekta ya tumbaku. Serikali yenyewe haihusiki moja kwa moja katika kupanga bei lakini imeweka tu utaratibu ambao wadau wenyewe wanaweza kukaa kukutana kwa uhuru wao na kupanga bei. Hata hivyo, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba bei ya tumbaku inaendelea kuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba tokea mwaka 2013 Bunge hili lilipitisha Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika, utaratibu mpya wa Vyama vya Ushirika ni utaratibu ambao pamoja na mambo mengine unawaruhusu wakulima wa mazao mbalimbali kuendesha shughuli zao kwa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuwa na uhuru zaidi. Lakini vilevile mpango ule umeunda Tume ya Ushirika ambayo inakuwa karibu na Vyama vya Ushirika ili kuwezesha kuondoa kero zilizopo. Tunafikiri kwamba utaratibu huu uteleta ufanisi zaidi katika kilimo cha tumbaku pamoja na mazao mengine ikiwa ni pamoja na kusaidia katika suala la bei.

Lakini nitumie tu fursa hii kuwawelezea vilevile Waheshimiwa Wabunge kwamba pamoja na changamoto nyingi zilizopo kwenye sekta ndogo ya tumbaku, tunafikiri sekta ndogo ya tumbaku ni eneo ambalo limeanza kuonesha mifano ya kufanikiwa. Hii ni kwa sababu ndiyo sekta ndogo ya pekee ambayo mkulima anakuwa na uhakika wa kuza zao lake tokea siku ya kwanza anapoanza kuweka mbegu shambani kwa sababu ni kilimo cha mkataba. Kwa hiyo, tukiondoa changamoto zilizopo tunafikiri ni eneo ambalo bado inawezekana kupata mafanikio makubwa. Lakini vilevile tungependa kutumia fursa hii kuwaweleza wakulima...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ufupishe jibu lako tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia. Kuwafahamisha kwamba kufanikiwa kutumia mfumo wa mkataba utasaidia tu kama kila mtu akiheshimu mkataba. Kwa mfano, mwaka huu tayari wakulima wanafahamu inatakiwa wazalishe tumbaku kiasi gani, tunaomba wale ambao hawako kwenye mkataba usizalishe tumbaku kwa sababu ukizalisha hautaweza kupata mnunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha pili cha swali ni kwamba ni kiasi gani na kwamba tumefikia wapi na kuwapata wanunu kutoka China.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajitahidi kuongea na wafanyabiashara kutoka China, tumefika hatua nzuri sana kilichobakia sasa ni wao kumaliza taratibu za nchi mwao ili nao waweze kuingia kwenye mfumo rasmi wa kununua tumbuku ili kuondoa ukiritimba ambao mpaka sasa hivi nchi nzima kampuni zinazonunua tumbaku ni nne tu.

Kwa hiyo, tunafikiri kampuni zikiwa nyingi maana yake tunaondoa monopoly na hivyo bei itakuwa nzuri nashukuru sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Usalama wa Maisha na Wale mavu wa Ngozi

MHE. MGENI JADI KADIKA aliuliza:-

Kwa muda mrefu wale mavu wa ngozi (albino) wamekuwa wakiishi kwa hofu katika nchi yao kutokana na kuuawa na kukatwa viungo vyao kwa imani za kishirikina ikiwemo kwa ajili ya kushinda uchaguzi au kujipatia mali:-

Je, Serikali ina mpango wa kuwalinda na kuwahakikishia usalama wa maisha yao watu hao wenyewe ulemavu wa ngozi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyowahi kujibiwa katika swali la msingi namba 99 na swali namba 60 katika mikutano tofauti ya Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu usalama wa ndugu zetu wenyewe ulemavu wa ngozi, Serikali kupitia Jeshi la Polisi na wadau wengine imekuwa ikichukua hatua za maksudi kukomesha mauaji hayo ikiwa ni pamoja na kuwasaka na kuwakamata watuhumiwa pamoja na kuwafikisha mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya pia juhudini za kuanzisha vituo vya kuwashudumia watu wenyewe ulemavu wa ngozi ambavyo vimesaidia kuimarisha ulinzi. Pia Jeshi la Polisi kwa kutumia falsafa ya Polisi Jamii inatoa elimu kwa umma juu ya madhara ya vitendo vya ukatili na mauaji na kujerui yanayofanywa na baadhi ya watu kwa msukumo wa imani potofu ya ushirikina. Aidha, Jeshi la Polisi limekuwa likifanya operesheni maalum za mara kwa mara zikiwamo za kukamata waganga wa jadi wanaopiga ramlili chonganishi ambazo ni kichocheo kikubwa cha ukatili dhidi ya wale mavu wa ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Jeshi la Polisi ikishirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama za Vijiji, Kata, Wilaya na Mikoa imeanzisha vikosi kazi hususan kwenye Mikoa na Wilaya zilizojitokeza kukithiri kwa matukio haya ili kuratibu na kusimamia kwa karibu ulinzi wa ndugu zetu wenyewe ulemavu wa ngozi. Vikosikazi hivyo hufanya kazi kwa kukusanya taarifa za kiintelejensia na kuzifanya kazi.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri aliyonijibui Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni kesi ngapi zilizolipotiwa kwa kipindi hiki cha mwaka wa uchaguzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni kwa nini kesi zinacheleweshwa wale walemaavu hawapi haki zao kwa haraka?

Na je, ni mikoa mingapi inayoongoza kwa mauaji ya maalbino? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kadika umeuliza maswali matatu, Naibu Waziri tafadhalii jibu maswali mawili.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanzu kuhusu Mikoa ambayo inaongoza ni Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Shinyanga na Kigoma.

Swali lake la pili anauliza kwamba ni kesi ngapi, takwimu halisi zilizotokea baada ya kumalizika uchaguzi naomba nimpatie baadaye lakini ninachowenza kusema ni kwamba toka mauaji haya yameanza mwaka 2006 mpaka mwaka jana takribani watu wanakadirwa kwenye 40 mpaka 43 wameweza kufariki, lakini watuhumiwa karibu 133 na katika hao watuhumiwa ambao wamehukumiwa kwa adhabu ya kifo ni 19 tayari ambao wameonekana wana hatia. Kwa hiyo, hizi takwimu za baada ya uchaguzi mpaka saa hivi, hizi naomba nikupatie baadaye. (Makofi)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa matatizo yaliyoulizwa na Mheshimiwa Mgeni kwenye swali namba 106 yanafanana kabisa na matatizo yaliyoko Jimbo la Geita Vijijiini. Takribani wanawake wazee wanne kwa mwezi wanauwawa kwa kukatwa mapanga kwa imani ya kishirikina na Jeshi la Polisi halijawahi kufanikiwa kuwakamata wakataji mapanga hao kwa kuwa jiografia ya kutoka Geita kwenda eneo husika ni mbali.

Je, Serikali inajipangaje kupeleka gari maalum na kuunda Kanda Maalum kwa ajili ya kuokoa akina mama wanaokatwa mapanga kwenye Jimbo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linajitahidi sana kuweza kukabiliana na mauaji haya, lakini kama ambavyo nimezungumza wakati nikijibu maswali wiki iliyopita kuhusiana na changamoto ambazo zinakabili Jeshi la Polisi. Naomba nichukue fursa hii kuweka sawa kidogo takwimu wakati nilikuwa najibu swali la Mheshimiwa Selasini juzi, nilieleza kwamba moja katika changamoto inakabili Jeshi letu la Polisi ni kwamba idadi ya polisi tulionao ni kidogo na kiukweli kihalisia takwimu zinaonyesha kwamba ukiangalia takwimu za kidunia polisi mmoja anatakiwa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ahudumie kati ya watu 400 mpaka 450 takriban na siyo 300 mpaka 350. Sisi hapa nchi yetu polisi mmoja kwa upande wa Tanzania Bara anahudumia watu kwenye 1000 mpaka 1200. Kwa hiyo utaona ni tofauti kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa changamoto hizi na changamoto nyingine ambazo tumekuwa tukikabiliana nazo hatua kwa hatua kama hii ya usafiri, nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Musukuma kwamba tumekuwa na changamoto ya usafiri kwa muda mrefu lakini tumepata magari takribani magari 387 ambayo yameweza kugawiwa katika maeneo mbalimbali. Tutaangalia eneo hilo kama halijafika gari tuone ni jinsi gani na uzito wa hali yenye ilivyo tushauriane tuone ni nini tutakachofanya ili tuweze kukabiliana na tatizo hilo. Lakini mengine ni changamoto ambazo tunaenda nazo kadri ya uwezo wa bajeti unavyoruhusu.

Na. 107

Uhaba wa Magari na Mafuta katika Vituo vya Polisi Wilaya ya Magharibi

MHE. HAFIDH ALI TAHIR aliulliza:-

Bunge la Jamhuri ya Muungano hupitisha Bajeti ya Serikali kwa kila Wizara kwa mwaka ikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani:-

(a) Je, inakuwaje Wilaya yenyе vituo saba vya polisi ina gari moja tu na inapatiwa lita tano hadi saba tu za mafuta kwa siku?

(b) Je, Serikali iko tayari kuziongezea mafuta na magari Wilaya za Magharibi A na B zenyе vituo vya polisi vya Fumba, Mbweni, Mazizini, Mwanakwerekwe, Kijitoupele, Fuoni, Airport na Mfenesini ambazo ni gari moja tu kila Wilaya ili kukongeza ufanisi na kuendana na kasi ya hapa kazi tu hasa ukizingatia kuwa Zanzibar inajiardaa na marudio ya Uchaguzi Mkuu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Wilaya ya Magharibi A na B hazina magari na mafuta ya kutosha kwa shughuli za polisi. Hali hii ni changamoto kwa vituo vingi vya polisi hapa nchini, hata hivyo, mgawo wa vitendea kazi yakiwemo magari huzingatia jiografia ya

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wilaya. Hali ya uhalifu na idadi ya watu wanaohudumiwa na kituo husika na siyo idadi ya vituo vidogo vya Polisi vilivyopo katika Wilaya husika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, inakusudia kuwasilisha bajeti mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuboresha hali ya vyombo vya usafiri, mafuta na vilainishi ili kukidhi mahitaji halisi ya Jeshi la Polisi hapa nchini, vikiwemo Vituo vya Polisi alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jawabu zake, lakini swali langu lilikuwa na msisitizo ukizingatia kuwa Zanzibar inajiandaa na marudio ya Uchaguzi Mkuu, ndiyo sababu swali langu kubwa lilikwenda huko. Kurudiwa kwa Uchaguzi Zanzibar siyo jambo geni, mwaka 1961 Uchaguzi ulifutwa na ukarudiwa mwaka 1963. (Makofii)

Sasa kwa tokeo hili Mheshimiwa Waziri swali langu la kwanza, huoni kwamba kuna haja ya kuweka umaksudi wa kupatia usafiri Wilaya nilizozitaja wakati huu tukielekea katika uchaguzi ili yale mazombi yanayozungumzwa yapunguke kufanya kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili, namwomba Waziri aniambie kwamba kwenye Bajeti ijayo ameahidi kwamba atatupatia magari Wilaya alizozitaja, Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ukubali hii ni ahadi na nikungoje kwenye bajeti? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie kwamba nilzungumza vilevile kuhusiana na hili suala la magari ambalo kwa bahati mbaya kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamelipotosha kwa makusudi ama hawajalielewa. Lakini naomba nichukue fursa hii kwa kueleza tu kwa ufupi ni kwamba Jeshi la Polisi na ninyi Wabunge ni mashahidi mara nyingi mmekuwa mkihoji, vituo vyangu havina magari, Jimbo langu kwenye kituo fulani hakuna magari, na ndiyo kwa kuzingatia hilo Serikali kupitia Jeshi la Polisi, likaandaa mkakati kabambe wa kupunguza hiyo hali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulimaliza kwa wakati mmoja, siyo rahisi kwa sababu katika nchi tuna zaidi ya vituo 4,500, kwa hiyo, kupata gari 4,500 kwa mpigo ili kila kituo kiweze kupata gari ni jambo ambalo ni gumu. Kwa hiyo kulikuwa kuna mpango wa kwanza wa kuweza kupata gari 777 kupitia mkopo wa Exim Bank ya India, ambapo kati ya hizo tuliweza kupata gari 104, lakini pia Serikali iliweza kutoa gari takribani 203 kwa hiyo kufanya jumla ya idadi ya gari ambazo zilipatikana kuwa ni 387. Kati ya gari hizo, gari 37 zilipelekwa Zanzibar na nimhakikishie Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir kwamba gari hizi bado hazijagawiwa katika Wilaya, nina hakika kwamba wakati mgao utakapokuwa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

umefanyika, basi Wilaya hizo ambazo zimezungumzwa vituo vya Wilaya yake ya Magharibi A na Magharibi B vitapata gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swalii lake la pili, alizungumzia kuhusiana na hali ya usalama kwa ujumla. Mimi nataka nimhakikishie tu kwamba pamoja niichukue fursa hii, kuwaeleza Wananchi wa Zanzibar kwamba Jeshi la Polisi ama Serikali itahakikisha inalinda usalama wa raia kama ambavyo majukumu yake ya msingi yanavyotaka. Kwa hiyo, wasiwe na wasiwasi wajitokeze kwa wingi kushiriki uchaguzi utakaporudiwa na hakuna wasiwasi wowote kila mtu ambaye atakuwa na haki ya kupiga kura, apige kura kwa usalama na amani. (Makofij)

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ninaomba niulize swalii dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa shida ya ulinzi iliyopo Dimani inafanana sana na Jimbo la Ukonga, nina Kata 13, sina kituo kikubwa cha Polisi, na ni eneo la pembezoni ikiwepo Msitu wa Kazimzumbwi, lakini hata kituo cha Sitakishari ambacho kinahudumia Jimbo la Segerea na Ukonga hakuna gari, sasa nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, atatujengea Kituo cha Polisi Ukonga au apeleke gari Segerea Sitakishari ili ihudumie wakati mipango mingine inaendelea?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasilishe, ahsanteni.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ule umuhimu wa magari ambayo nimekuwa nikiuzungumza umeongezeka uzito wake, sasa niweke tu wazi kwamba katika yale magari ambayo tumeyapata, magari mengi ni kwa ajili ya doria, operation na matumizi ya kawaida ya polisi. Hayo magari yanayoitwa ya washawasha sidhani hata 24 sujui kama yanafika.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waitara nadhani utakubaliana na mimi na Wabunge wengine kwamba, Jeshi la polisi linahitaji magari zaidi, ikiwemo katika Kituo chako ulichozungumza, mimi naomba hili nilichukue tuone tutalifanya kazi vipi.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, wabheja sana. Kwa kuwa Jimbo la Kishapu halikupata mgao wa magari mapya ya polisi katika awamu hii na Jimbo hili lenye watu sharp na askari wanaofanya kazi zao kwa u-sharp, lina magari mawili mabovu yenye umri wa zaidi ya miaka mitano.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, nilipata ahadi kuwa mwezi wa pili tutapata magari mapya ya polisi, uko tayari kunihakikishia Jimbo sharp litapata magari

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mapya ili Wananchi waweze kupata huduma hasa za kiusalama wanapohitaji kuliko hivi sasa polisi wangu wa Kishapu wanavyohangaika? Wabheja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nchambi wakati Naibu Waziri akija, hayo maneno wabheja siyo lugha ya Kibunge, kwa hiyo nayafuta kwenye record karibu Mheshimiwa Naibu Waziri. (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Nchambi kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano ya hapa kazi tu huwa haina desturi za kutoa ahadi ambazo hazitekelezeki. Kwa hiyo, kama ni ahadi ambayo imetolewa, basi nitaifuatilia hiyo ahadi yenyewe halafu tuone hatua zilizofikiwa zimefikiwaje na kama imekwama imekwama vipi, halafu tutaonana mimi na yeye tuone ni jinsi gani ya kufanya.

NAIBU SPIKA: Tuendelee Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Mheshimiwa Halima Ali Mohamed, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 108

Tatizo la Ugonjwa wa Moyo, Kisukari na Vidonda vya Tumbo

MHE. HALIMA ALI MOHAMMED aliuliza:-

Takwimu zinaonyesha kuwa kuna kasi kubwa ya ongezeko la wagonjwa wa maradhi ya moyo, kisukari na vidonda vya tumbo (*ulcers*):-

Je, Serikali ina mkakati gani kukabiliana na tatizo hili?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO aliijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Halima Ali Mohammed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeshuhudia kasi kubwa ya ongezeko la magonjwa ya moyo, magonjwa ya kisukari na magonjwa ya vidonga vya tumbo, ambayo ni magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Hii imechangiwa na mabadiliko ya mfumo wa maisha kama ulaji usiyo sahihi, kutokufanya mazoezi, kutokula matunda na mboga mboga kwa wingi, uvutaji wa sigara na tumbaku na unywaji wa pombe uliyokithiri.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya utafiti wa STEPS uliyofanyika mwaka 2012 yalionesha kuongezeka kwa viashiria yaani *indicators* vinavyosababisha magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Aidha, utafiti pia ulionesha karibu asilimia 9 ya Watanzania, wanaugua ugonjwa wa kisukari na wengi wao kwa bahati mbaya hawajijui. Kwa kutambua ongezeko hili Wizara yetu imeanzisha sehemu ya kushughulikia huduma ya magonjwa haya yaani kitengo cha Non Communicable Diseases, Mental Health and Substance Abuse chini ya Kurugenzi ya Tiba pale Wizarani. Miongozo na mikakati mbalimbali imekwisha kutengezezwa ikiwa ni pamoja na mkakati wa Kitaifa wa kukabiliana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza yaani magonjwa ya kisukari, moyo na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu kwa jamii ni kubadili mtindo wa maisha yaani *life style* kwa kula vyakula vinavyofaa, kupunguza unywaji wa pombe na uvutaji wa sigara na tumbaku na kuwa na tabia ya kufanya mazoezi ili kuepuka uwezekano wa kupata maradhi haya.

MHE. HALIMA ALI MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa ya Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tafiti zinaonyesha kwamba wanawake wanaathirika zaidi na maradhi ya moyo kuliko wanaume.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia wanawake hawa ambao ndiyo walezi wa familia hasa wale waliopo kule vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti uingizwaji wa vyakula vibovu ambavyo havina kiwango katika nchi yetu? Ahsante (Makofii)

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza Serikali ina mkakati gani wa kupunguza kiasi cha magonjwa haya kwa wanawake ambao wanaathirika zaidi kuliko wanaume.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti ya upatikanaji wa magonjwa haya, kwa jinsia kwa maana ya baina ya wanawake na wanaume ni ndogo sana na kwa maana hiyo, mkakati wa kupambana na kuenea kwa magonjwa haya hauwezi kutofautishwa kwa jinsia. Hivyo mkakati wetu utakuwa ni wa pamoja na tayari Wizara ya Afya imeanza kutekeleza mkakati huo, kwanza kwa kutia umuhimu wa kipekee kwenye kuimarisha Kitengo cha NCD yaani Kitengo cha Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza pale Wizarani chini ya Kurugenzi ya Tiba.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitengo hiki tayari kimeishaaza mkakati wa kuandika mkakati wa kupambana na magonjwa haya na mkakati huu utawafikia hao akinamama wa vijiji na watu wote kwa ujumla wake kuanzia ngazi ya huduma za afya kule vijiji, kwa maana ya ngazi ya zahanati, ngazi ya vituo vya afya na ngazi ya hospitali za Wilaya, Mikoa na hata ngazi ya Kanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, ni kweli kumekuwa na hisia kwamba kuna vyakula visivyo na viwango vinaingia nchini mwetu kutoka nchi za mbali. Serikali kwa kushirikiana kwa maana ya Wizara yetu Wizara ya Afya, ambayo ina kitengo cha TFDA (*Tanzania Food and Drugs Authority*) ambacho kipo chini ya Wizara yetu ya Afya, pamoja na Kitengo cha Viwango (*TBS*), wanaendelea kushirikiana kwa pamoja, kukagua mizigo yote ambayo inaingia nchini kwa njia za halali.

Lakini pia vyombo vingine vya kusimamia Sheria kama Majeshi ya Polisi na Uhamiaji, wataendelea kuwa makini kwenye mipaka yetu yote, katika njia zilizo halali na hata zile ambazo siyo halali kudhibiti uingizwaji wa vifaa hivi ikiwemo vyakula na dawa ambavyo havijapitishwa kwa viwango vinavyostahili, kwa mujibu wa Sheria za nchi yetu. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Wizara ya Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa Risala Saidi Kabongo Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 109

Kuongezeka na Kuboresha Vyanzo vya Maji Arusha

MHE. RISALA S. KABONGO aliuliza:-

Vijiji vya Ngiresi, Sokoni II na Oldadai Kata ya Sokoni II Jimbo la Arumeru Magharibi vinakabiliwa na tatizo la ukosefu wa maji ya bomba, kwa muda mrefu licha ya kwamba vijiji hivyo kuna vyanzo vingi vya maji na mabomba yanayopeleka maji Arusha Mjini:-

(a) Je, Mamlaka ya Maji Jiji la Arusha inashindwa kutekeleza maombi ya wananchi wa vijiji hivyo ya kupatiwa maji kutoka kwenye mabomba kwa utaratibu wa kulipia?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza na kuboresha vyanzo vya maji katika Jiji la Arusha na Halmashauri zake kutokana na ongezeko kubwa la wakazi wake?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Risala Saidi Kabomgo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika kuondoa tatizo la maji Jiji la Arusha, imepata mkopo wa dola za Kimarekani milioni 210.96 kutoka Benki ya Maendeo ya Afrika (AfDB) ili kutekeleza mradi wa upanuzi wa mtandao maji safi na maji taka sambamba na kuboresha vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu mkubwa utawezesha Jiji la Arusha pamoja na viunga vyake, ikiwa ni pamoja na vijiji vyote vilivyopo umbali wa kilometra 12 kando kando ya bomba kuu, vikiwemo vijiji vya Ngilesi, Sokoni II na Oldadai ili kupata huduma ya majisafi na majitaka. Jumla ya gharama za ujenzi ni dola za Marekani milioni 233.92 sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 476.44.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa mkopo huu nafuu umesainiwa na Mamlaka ya Maji Arusha, kwa sasa inaendelea na taratibu za kupata Mhandisi Mshauri wa kusimamia mradi pamoja na Wakandarasi wa Ujenzi. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2016/2017 na kukamilika mwaka 2019/2020. Mradi huu ukikamilika utaboresha vyanzo vya maji na utaongeza upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Arusha na Halmashauri zake ambazo zimekumbwa na ongezeko kubwa la wakazi.

MHE RISALA S. KABONGO: Mheshimiwa, Naibu Spika nakushukuru. Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako.

Kwa kuwa, mradi huu ni Mkubwa na ni wa miaka mitano; je, Serikali inavipa vipaumbele gani vijiji hivi vya Oldadai na Sokoni II na Ngilesi, kwa kuwa wamekuwa na kero kubwa na ya muda mrefu ya kupata maji?

Eneo la pili, nitaomba Mheshimiwa Waziri, atakapopata nafasi baada ya Bunge hili, aweze kutembelea maeneo haya na kujionea hali halisi katika vyanzo hivi ambavyo vinatunza maji yanayosaidia katika Mkoa wa Arusha. Ahsante. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, la pili nadhani lilikuwa ni ombi, swali ni moja tu liloulizwa.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ni kweli tumepeata ufadhili wa mradi mkubwa ambao utekelezaji wake utachukua miaka mitatu. Jana tulikuwa na Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, amekuja ofisini kwangu pamoja na Meya, pamoja na Mbunge na tumekubaliana kwamba, tutatengeneza mpango wa muda mfupi ili hivyo vijiji

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

unavyovisema tuweze kuvitafutia angalau wapate maji wakati tunatekeleza huu mradi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kulikuwa na Mradi wa Vijiji Kumi, tumekubaliana kwamba Jiji la Arusha litakabidhi kwenye mamlaka yetu ya Arusha ili kusudi waweze kuunganisha kwenye mtandao baadhi ya maeneo ambayo Arusha hayapati maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana pia kwamba na mimi nitakuja kuangalia utekelezaji wa mpago huu. (Makofii)

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Suala la Arumeru Magharibi linafanana sana na tatizo ambalo lipo Mikumi, je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa kero ya maji katika Kata ya Mikumi, Ruaha, Uleling'ombe na maeneo ya Tindiga?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri katika majibu yake ametoa taarifa kwamba tunaingia katika progamu ya pili kupitia sera ya mwaka 2002 ya kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2020 asilimia 85 ya Watanzania wote watakuwa wanapata maji katika vijiji na asilimia 95 katika miji.

Mheshimiwa Mbunge, kwa upande wa Jimbo lako la Mikumi na Kata zake, tutahakikisha kwamba tunazipa kipaumbele kuhakikisha zinapata maji katika hii progamu ya pili. Na ninakuomba sana baada ya Bunge hili tuwasiliane ili tuweze kupata taarifa iliyo nzuri zaidi tuanze utekelezaji.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa tatizo la Arumeru Mashariki linafanana kabisa na tatizo la maji la Lushoto.

Je, ni lini Serikali itaondoa adha hii kwa wananchi wa Lushoto?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Wilaya ya Lushoto mlalo wake wa ardhi ni mzuri kuruhusu ujenzi wa mabwawa. Tumeweka mpango wa kujenga mabwawa katika awamu hii ya programu ya pili ambayo yatasaidia kwenye *irrigation* pamoja na kuhakikisha kwamba tunapata maji ya kunywa kwa wananchi wa Jimbo lake.

Na. 110

Kuanza kwa Mradi wa Bomba la Maji Ziwa Victoria

MHE. RICHARD M. NDASSA aliuliza:-

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, ni lini mradi wa ujenzi wa bomba la maji ya Ziwa Victoria kutoka Magu - Sumve - Malya utaanza?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (*EIB*) na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza (*MWAUWASA*) inatekeleza miradi ya maji safi na maji taka kwa Jiji la Mwanza pamoja miradi ya maji safi katika miji mitatu ya Magu, Misungwi na Lamadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mji wa Magu mradi huu unakadiriwa kugharimu kiasi cha Euro milioni 5.3 na Mkandarasi anatarajiwa kuanza ujenzi wa mradi ifikapo mwezi Julai, 2016. Idadi ya wananchi watakaonufaika na mradi huu inakadiriwa kuwa wananchi 73,363 ifikapo mwaka 2040.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miji ya Sumve na Malya, Serikali inaendelea kufanya uchunguzi wa awali ili kubaini gharama za eneo la kuitisha mradi. Kazi ya upimaji pamoja na usanifu itakamalika mwezi Aprili, 2016 na ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2016/2017.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza naomba nisahishe jina langu hapa inasomeka Ngassa, siyo Ngassa ni Ndassa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini naomba Serikali itambue kwamba suala la maji ni suala kila Mtanzania, kila mwananchi anahitaji maji na ndiyo maana unaona Wabunge wote wanasema kuhusu maji.

(a) Swali langu, kwa sababu Serikali katika mwaka 2000 na 2004 iliamua, maamuzi magumu yenyeye tija, kuyatoa maji ya Ziwa Victoria kuyapeleka Kahama, Shinyanga. Je, Serikali ina mpango gani mrefu wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria katika Mikoa tisa ili maji hayo yawanufaishe Watanzania na mikoa hiyo ni Mwanza, Mara, Kagera, Simiyu, Singida na Dodoma. Serikali ina mpango gani kwa sababu mahitaji ya maji ni makubwa na maji ya Ziwa Victoria yapo hayana kazi nyagine. Je, Serikali ina mpango mkakati gani wa kuhakikisha kwamba maji yanafika katika maeneo hayo?

(b) Mheshimiwa Waziri wa Maji, wananchi wa Jimbo la Sumve katika Kata ya Nkalalo na Mabomba wanashida kubwa ya maji, naomba nikuombe

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

pamoja na maelezo haya utembelee tuende ukajionee mwenyewe jinsi wananchi wa Tanzania wa Jimbo la Sumve wanavyopata taabu ya maji katika Jimbo langu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza jana kwamba tumeleta mapendeleko ya mwongozo kwa kutengeneza mpango wa miaka 2016/2017 na nilisema katika sekta ya maji tumetoa ahadi kwamba katika miji yote ya Mikoa inayozungukiwa na Ziwa Victoria tutahakikisha tunachukua maji ya kutosha kuyafikisha kwenye maeneo husika kwa kiwango ambacho tumeshasema kwenye llani, kwamba Miji Mikuu ya Mikoa ipate asilimia 95 ikifika 2020 na ipate asilimia 100 ikifika 2025.

Kwa hiyo, naomba nilihakikishie Bunge hili kwamba azma hiyo ambayo pia Mheshimiwa Rais wetu ameahidi tutakwenda kufanya, tutaomba Waheshimiwa Wabunge muweze kutuunga mkono katika kupanua vyanzo vya upatikanaji wa fedha hasa kuongeza Mfuko wa Maji ili tuweze kutekeleza miradi yote hii ambayo kila Mbunge ameomba Serikali iweze kufanya, ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbarouk

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, jina langu naitwa Mussa Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ilianzisha mpango wa maji safi na salama vijiji katika mradi uliofadhliliwa na World Bank na mradi ule umekwama. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha katika Halmashauri ya Jiji la Tanga ili kuondoa kero ya maji katika Kata za Mabokweni, Chongoleani, Kilale na Marungu?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ilianzisha mradi wa vijiji 10 kupitia programu ya Benki ya Dunia na mradi huo ungali unaendelea. Katika mradi huo tulikuwa na miradi 1,855 kama nilivyotoa taarifa ya awali kwamba katika miradi hiyo miradi 1,143 imekamilika na miradi 454 inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo la fedha ndiyo lililofanya hii miradi isikamilike kwa wakati lakini nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika eneo lako la Tanga kufuatia juhudhi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukusanya fedha, fedha zimeanza kutoka na nikupe tu taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba wiki iliypita tumeletewa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kuendelea kulipa miradi hiyo mingi ambayo ilikuwa imesimama na siyo Tanga tu, ni karibu Mikoa yote miradi ilikuwa imesimama.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nikuhakikishie kwamba Serikali inatoa fedha kuhakikisha miradi hiyo inakamilika ili katika programu ya pili tuanze kuweka tena miradi mingine. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa sasa aulize swali lake.

Na. 111

Kuweka Mizani katika Barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi ili Kuilinda Iweze Kudumu kwa Muda Mrefu

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA aliuliza:-

Barabara ya Mbeya – Chunya - Makongorosi imejengwa kwa kiwango cha lami kwa asilimia 80. Je, ni lini Serikali itaweka mizani katika barabara hiyo ya lami ili kuilinda iweze kudumu muda mrefu?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Jimbo la Lupa kama ifuatavyo:-

Barabara ya Mbeya – Chunya – hadi Makongorosi yenyе urefu wa kilometra 117 ni barabara kuu inayohudumiwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakala wa Barabara Mkao wa Mbeya. Barabara hii imejengwa kwa kiwango cha lami, sehemu ya barabara kati ya Mbeya hadi Chunya ambayo ni kilometra 72 na imekamilika hivi karibuni. Aidha, Serikali inafanya maandalizi ili kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Chunya hadi Makongorosi ambayo ni kilometra 45.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatambua kuwa katika Wilaya ya Chunya kuna shughuli nyingi za kiuchumi kama vile uchimbaji wa madini, kilimo na mazao ya misitu ambayo huchangia kwa kiwango kikubwa upitishaji wa magari yenyе mizigo mizito na hivyo kuna umuhimu wa kuweka mizani kwenye barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itajenga mizani katika barabara ya Mbeya - Chunya hadi Makongorosi wakati wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Chunya - Makongorosi. Aidha, katika kipindi hiki ambacho ujenzi wa mizani ya kudumu haujafanyika, Serikali kupitia TANROADS itaendelea kudhibiti

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

uzito wa magari katika barabara hiyo kwa kutumia mizani ya kuhamishika (mobile weighbridge).

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Napenda kumshukuru sana Naibu Waziri amejibu vizuri sana na amejibu kitaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imesema Chunya ina mazao mengi ambayo yakibebwa ndiyo yanaharibu barabara, sasa napenda nimwambie Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba wanaosomba tumbaku, magari yanayobeba tumbaku au mbao au mkaa yanabeba lumbesa, yanakuwa mara mbili, yakifika Mbeya yanagawa kwa sababu kuna mizani kule ndiyo yawe magari mawili na Serikali hapa imesema kwamba itadhibiti hiyo kwa kuweka mobile weighbridges.

Je, ni lini itaweka kwa sababu Chunya sasa hivi sijaiona *mobile weighbridge* hata moja? Hilo ni swali la kwanza

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili nashukuru Serikali imesema kwamba ujenzi wa barabara hiyo kuanzia Chunya kwenda Makongorosi karibu utaanza, napenda nimwambie Naibu Waziri kwamba Mheshimiwa Rais akiwa Makongorosi aliwaahidi wananchi wa Makongorosi kwamba atawapa kilomita nne za lami pale Makongorosi na kwamba barabara hiyo ya Chunya Makongorosi itaanza kujengwa Makongorosi kuja Chunya.

Je, hiyo barabara itanza lini kujengwa? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema kwenye jibu la msingi la swali la msingi kwamba weighbridge itaanza hivi karibuni. Naomba kuchukua nafasi hii kumhakikisha Mheshimiwa Mwambalaswa kama yeye alivyo-concerned na uharibifu wa barabara hiyo na sisi ambao ndiyo wenye dhamana hiyo tuko concerned kwa kiwango kikubwa, ninamhakikisha hiyo weighbridge inatafutwa hivi karibuni itaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la pili naomba kumjulisha Mheshimiwa Mwambalaswa kwamba mara fedha zitakapopatikana barabara hii itaanza kujengwa na suala la ianzie wapi whether ianzie Makongorosi au ianzie Chunya nadhani ni muhimu tuwaachie wataalamu na ahadi ya kilomita Nne nayo katika eneo la Makongorosi itaangaliwa kwa umakini wake. (*Makofii*)

Na. 112

Uhakika wa Fidia kwa Wananchi Waliopisha Barabara

MHE. DUA W. NKURUA aliuliza:-

Katika ujenzi wa barabara ya Mangaka - Mtambaswala na Mangaka - Nakapanya, wapo wananchi ambao walishafanyiwa tathmini ya fidia ya kupisha ujenzi huo hawajalipwa na wengine wamepunjwa.

Je, Serikali italeta lini wataalamu wa kuhakiki fidia hizo ili kila mwananchi apate haki yake?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dua William Nkurua, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ujenzi wa barabara ya Mangaka - Mtambaswala na Mangaka - Nakapanya, Serikali ilitenga fedha shilingi milioni 3,023.528 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi waliokwisha fanyiwa tathmini ya mazao yao kati ya mwaka 2009 na 2012. Aidha, baada ya uthamini kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali mwaka 2013, fidia ililipwa mwaka 2014 kwa kufuata taratibu na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wananchi ambao mali zao hazikufanyiwa tathmini katika kipindi hicho hawakulipwa fidia. Tathmini ya fidia kwa mali za wananchi hao imefanyika mwezi Oktoba 2015 na taarifa ya uthamini imekamilika na imewasilishwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa hatua ya kuidhinishwa ili malipo yaweze kufanyika.

MHE. DUA W. NKURUA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika wale ambao walifanyiwa tathmini ya awamu ya kwanza, wapo ambao mpaka sasa hawakulipwa, Majina yao yalirukwa katika Kijiji cha Misawaji, lakini pia wapo ambao walifanyiwa tathmini kwamba nyumba zao zitabomolewa nusu lakini zimebomolewa zote na hivi ninavyokwambia wamechanganyikiwa kabisa.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuma watu tumuoneshe watu ambao wameathirika ili wapate haki yao?

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa barabara kutoka Masasi mpaka Mangaka imekamilika, hadi sasa magari yenyé uzito mkubwa kutoka Songea kuelekea Masasi yanatumia hiyo barabara.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni umuhimu wa kuleta mizani katika Mji wa Mangaka ili kuokoa barabara ambayo Serikali imetumia gharama kubwa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana nae kwamba tutatuma watu waende wakalichunguze hilo suala na hatimaye tuweze kulipatia ufumbuzi stahiki. Ninachoomba kumhakikishia tu ni kwamba Serikali hii inafuata sheria na yeote mwenye haki ya kulipwa fidia atalipwa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili nadhani anafahamu kwamba hizo barabara anazoziongelea bado hazijakamilika na hivi karibuni nimepiata katika eneo lake ingawa kwa bahati sikumjulisha kwa sababu ilikuwa ni dharura wakati natokea Jimbo la Namtumbo. Ninamhakikishia mara barabara hizi zitakapokamilika na umuhimu utakapoonekana kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kuweka mizani, Serikali itafanya maamuzi stahiki. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Keissy.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa barabara ya kutoka Sumbawanga kwenda Mpanda takriban kilometra 50 zimeshatengenezwa na magari makubwa ya mahindi zaidi ya tani 60, 70 yanapita kuelekea Mpanda. Nimeshamwomba Waziri wa Ujenzi kupeleka gari ya mizani ili kudhibiti uharibifu wa barabara kabla wakandarasi hawajakabidhi kwa sababu barabara inaanza kuharibika kabla haijakabidhiwa. Je, ni lini Serikali itapeleka gari ya mizani ili kudhibiti barabara hiyo isiendelee kuharibika?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Keissy na wananchi wa Sumbawanga hadi Mpanda kwamba barabara ile kwanza tutaikamilisha kuijenga. Tutakapoona umuhimu wa kuweka mizani kutoptana na tathmini ya wataalam tutakaowapeleka kufanya shughuli hiyo tutaweka mizani hiyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge kule nyuma ujitalbulishe tafadhali.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Naitwa Alex Raphael Gashaza, Mbunge wa Jimbo la Ngara.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa kuwa barabara ya Murugarama – Rulenge – Nyakahura yenyе kilometa 85 ni barabara ambayo iliahidiwa na Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mwaka 2008 kwamba itaweza kujengwa kwa kiwango cha lami na miaka miwili iliopita wananchi wa Jimbo la Ngara walikuwa wakielezwa kwamba tayari upembuzi yakinifu wa barabara hii umeanza.

Naomba kumuuliza Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ni lini mkandarasi atakuwepo site kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii? (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata taarifa kutoka kwa Waziri mwenyewe wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano juu ya upatikanaji wa fedha za kulipa madeni ya wakandarasi, kama jana mlimsikia alisema ni karibu shilingi bilioni 419 zimeshatolewa. Kwa hiyo, katika lile deni la shilingi trilioni 1.268 sasa tumeshuka tuko kwenye shilingi bilioni 800 na zaidi. Naomba kuchukua nafasi hii kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba mara fedha zitakapopatikana kwa mradi huo, barabara yake itashughulikiwa kama ilivyoahidiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Na. 113

Mkoa wa Shinyanga na Simiyu Kuunganishwa kwa Barabara za Lami

MHE. GIMBI D. MASABA aliuliza:-

Mkoa wa Shinyanga na Simiyu inaunganishwa kwa barabara ya vumbi, tofauti na mikoa mingine ambayo imeunganishwa kwa barabara za lami.

(a) Je, Serikali itaunganisha lini mikoa hiyo kwa barabara ya kiwango cha lami kwa kumalizia kilometa 102 zilizobaki katika barabara ya Lamadi - Mwigumbi kuititia Bariadi?

(b) Je, Serikali itaona umuhimu wa kuunganisha makao makuu ya Wilaya za Mkoa wa Simiyu kuunganishwa kwa barabara za kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gimbo Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mweshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mwigumbi - Maswa - Bariadi - Lamadi yenyе urefu wa kilometa 171.8 kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ikiwa na lengo la kuunganisha Mikoa ya Simiyu, Shinyanga, Mara na Mwanza na kwa barabara ya lami. Sehemu ya barabara hii kuanzia Bariadi - Lamadi yenyе urefu wa kliometra 71.8 tayari imejengwa kwa kiwango cha lami na imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, TANROADS ililia saini mkataba wa ujenzi na mkandarasi CHICO kutoka China kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya pili ya barabara hiyo kuanzia Mwigumbi - Maswa ambazo ni kilometra 50.3 kwa gharama ya shilingi bilioni 61.462. Hadi sasa mkandarasi yuko katika eneo la mradi na anaendelea na kazi za kujenga kambi, kuleta mitambo na wataalam kwa ajili ya kutelekeza mradi huo. Aidha, kwa sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kiwango cha lami wa sehemu ya Maswa - Bariadi ambazo ni kilometra 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kuwa kukamilika kwa barabara hii inayoendelea kujengwa kutawezesha Makao Makuu ya Wilaya za Busega, Bariadi na Maswa zilizoko katika Mkoa wa Simiyu kuunganishwa kwa barabara za lami. Wilaya nyingine zilizobaki zitaungwanishwa kwa barabara za lami kwa awamu kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masaba swalı la nyongeza.

MHE. GIMBI D. MASABA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı la kwanza, kwa vile nchi yetu ina uhaba wa majengo ya shule, zahanati na vituo vya afya, je, Serikali iko tayari kumuagiza mkandarasi ambaye sasa hivi yuko site kujenga majengo ya kudumu ili baada ya mradi kukamilika majengo hayo yaweze kutumika kwa ajili ya matumizi ya shule, zahanati na vituo vya afya? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı la pili, kwa kuwa barabara za Mkoa wa Simiyu zinaunganishwa na barabara za vumbi na kwa sasa hazipitiki kutokana na mvua zinazoendelea.

Je, Serikali iko tayari kutenga fedha kutoka kwenye Mfuko wa Barabara ili kuweza kutengeneza barabara hizo na ziweze kupitika kwa urahisi tofauti na ilivyo sasa? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, mkandarasi aliyeo site mkataba wake ulishasainiwa. Hata hivyo,

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nawaagiza TANROADS Mkoa wa Simiyu waangalie uwezekano katika mkataba huo kama inaweza ikafanyika variation au kama kifungu hicho kipo wahakikishe majengo yanayojengwa na mkandarasi huyo yaweze kuangalia matumizi ya baadaye ambayo Mheshimiwa Mbunge ameomba. Kama itashindikana, Serikali itatafuta njia nyingine kupitia Wizara husika ya Afya. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa swali la pili, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mfuko huo anaoungelea ndiyo tunaoutumia kujenga na kukarabati barabara zote nchi nzima. Naomba akubali mfumo tulio nao ndiyo huo, hatuna mfuko maalum kwa ajili ya barabara hii peke yake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kuniona niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka mmoja ulio mbele yetu, miundombinu si kipaumbele.

Kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Magufuli wakati akiomba kura aliahidi ujenzi wa barabara za lami nchini kote ikiwemo Jimbo langu la Babati Mjini ambako aliahidi ujenzi wa kilometra 20 za lami. Naomba nifahamu, ni lini ahadi hii itatekelezwa kwa wananchi wa Babati?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi zote ambazo zimetolewa kwanza na Chama Tawala kupitia Ilani yake ya mwaka 2015 - 2020 Serikali hii ina wajibu wa kuzitekeleza. na tutaitekeleza

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hiyo anayoiiongelea namuomba awasiliane na TANROADS mkoa ili kuangalia vipaumbele vya sasa vilivvopo katika mkoa ule. Kama barabara hiyo ni moja kati ya vipaumbele vya mkoa, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaitekeleza katika kipindi hiki kama ambavyo iliahidiwa katika kipindi cha kampeni.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Martha Mlata.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Na mimi kama swali la msingi lilivyoongea kuhusu Mkoa wa Simiyu kuunganishwa na mikoa mingine, ni wazi kwamba Mkoa wa Simiyu bado hauunganishwa na Mkoa wa Singida amba unapitia katika Daraja la Sibiti – Mkalama - Nduguti - Iguguno. Nataka nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, je, anafahamu kwamba Daraja la Mto Sibiti ndilo kiunganishi kikubwa katika Mkoa wa Simiyu na Singida na mpaka sasa mkandarasi hayupo site? Ahsante.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba Daraja la Sibiti ni muhimu katika mawasiliano kati ya Mkao wa Simiyu na Singida na ndiyo maana kazi kubwa inafanywa sasa kutohakikisha mawasiliano yanakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mkandarasi, kwa kuwa fedha za kulipa madeni ya wakandarasi tumeanza kupata ambapo huyu naye ni mmoja kati ya wakandarasi wanaotakiwa kulipwa ili waendelee na kazi. Mara fedha zitakapopatikana, mkandarasi atarudi site ili aweze kukamilisha kazi ambayo alisaini kuifanya.

Na. 114

Serikali Kuanzisha na Kumiliki Bureau de Change

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha na kumiliki Bureau de Change zake yenyewe badala ya kuacha huduma hiyo kuendelea kutolewa na watu au taasisi binafsi?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbuge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haina mkakati wa kufungua au kuanzisha Bureau de Change zake kwa sababu imejitoa kuhusika moja kwa moja na biashara ya fedha kama vile benki na Bureau de Change kutohakikisha mabadiliko ya mfumo katika sekta ya fedha nchini unaotekelizwa kuanzia mwaka 1991. Sekta binafsi imeachiwa jukumu la kuanzisha na kuendesha biashara ya fedha nchini chini ya usimamizi wa Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imebaki na jukumu la kuweka mazingira mazuri na salama ya uwekezaji katika sekta zote, ikiwemo sekta ya fedha ili kuiwezesha sekta binafsi kuanzisha, kuendesha na kutoa huduma bora za kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka sheria na taratibu za kusaidia nguvu na juhudzi za wananchi katika kuanzisha benki au taasisi za fedha katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na maduka ya kubadilisha fedha za kigeni.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo, Serikali inategemea kuwa wananchi watatumia fursa hii ya mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyopo nchini na kuanzisha huduma za kubadilisha fedha za kigeni katika maeneo yenyе uhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuitia Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kusimamia kwa ukaribu zaidi maduka ya kubadilisha fedha za kigeni nchini ili yaweze kutoa huduma bora na inayokidhi matakwa ya sheria na kanuni za biashara ya fedha. Hivi karibuni Benki Kuu imetoa kanuni mpya kwa lengo la kuimarisha usimamiaji wa maduka hayo. Maduka yote ya kubadilisha fedha za kigeni yanatakiwa kufunga mashine za *EFDs* ili kuiwezesha *TRA* na *BoT* kupata taarifa za moja kwa moja juu ya miamala inayofanywa kwenye maduka hayo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bakar swali la nyongeza.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Serikali imebaki katika kuweka mazingira mazuri, lakini naona kwamba mazingira mazuri hayo si kweli sana kwa sababu hayaonekani maana wananchi wanalamika sana. Kwa sababu ukienda Bureau de Change hii ina rate hii, ukienda Bureau de Change nyingine ina rate tofauti na zimetapaka sehemu zote kama sisimizi. Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha *rates* hizo zinalingana? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kuwa Serikali imejitoa katika biashara hii ya kumiliki Bureau de Change lakini huo ulikuwa ni uamuvi wa zamani na tujue kwamba sasa hivi dunia imebadilika, ni dunia ya sasa. Je, atakubaliana nami kwamba sasa umefika wakati wa Serikali kumiliki huduma hii ili kuwaondolea wananchi wake matatizo ambayo wanakubaliana nayo? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru kwa kuuliza maswali mazuri ya nyongeza ambayo yanakidhi haja na yanaakisi kinachoendelea katika maduka yetu ya kubadilisha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu la swali lake la kwanza kwamba *rates* ni tofauti sana kutoka duka moja kwenda duka lingine, nakubaliana naye na hii yote ni kuonesha kwamba tuko ndani ya soko huria na kila mtu anatakiwa ku-charge anavyoona inafaa. Pia kiuchumi, sisi wachumi tunafahamu kwamba bei ya bidhaa yoyote ile hutegemea na demand na supply. Kwa hiyo, kama demand ya bidhaa hiyo ni kubwa bei zitakuwa tofauti kutoka kwa muuzaji mmoja kwenda kwa muuzaji mwengine. (Makof)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, Serikali iweze kurudi kwenye kuendesha biashara kama hizi na kwamba huo ulikuwa ni uamuzi wa zamani, naamini uamuzi ule ulikuwa ni sahihi na bora. Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba tangu mwaka 1991 Serikali ilishajitoa kuendesha mabenki haya. Tunaendelea kusisitiza, sisi kama Serikali tutaendelea kutunga sera na sheria mbalimbali za kusimamia maduka haya ili yaweze kutoa huduma zilizo bora kwa wananchi wetu.

Na.115

Fursa Zitokanazo wa Mgodi wa Stamigold - Biharamulo

MHE. OSCAR R. MUKASA aliuliza:-

Mgodi wa Stamigold, Biharamulo uko kijiji Mavota katika Wilaya ya Biharamulo na wananchi wa Kijiji cha Mavota kwa sasa hawana fursa hata kidogo ya kufanya uchimbaji mdogo mdogo licha ya kwamba mgodi huo upo kijiji kwao, hali ambayo imekuwa chanzo kikubwa cha migogoro inayosababisha uvunjifu wa amani:-

- (a) Je, Serikali iko tayari kuwa na mazungumzo ya kimkakati na wananchi wa Kijiji cha Mavota kuitia Mbuge wao kwa manufaa ya uwekezaji na wanakijiji wa Mavota?
- (b) Kama Serikali haiko tayari kufanya mazungumzo hayo, je, ni kwa sababu zipi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo tayari kuwa na mazungumzo na wananchi wa Kijiji cha Mavota kwa lengo la kuwawezesha wananchi hao kutumia fursa zilizopo katika Mgodi wa Stamigold karibu na Mavota. Mgodi huo kwa sasa unamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 kuitia STAMICO ambapo Stamigold kampuni tanzu ya STAMICO ndiyo inayofanya shughuli za uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu yatakayozingatiwa ni pamoja na kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji hao wadogo, kuwaelimisha namna ya kupata mitaji ya uchimbaji ikiwa ni pamoja na kutumia fursa za kuomba ruzuku Serikalini. Kadhalika, pamoja na kuwapa elimu na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuwahamasisha kuunda vikundi vya uchimbaji ili waweze kusaidiwa kwa pamoja. Aidha, Mgodi wa Biharamulo utawapatia mafunzo ya utaalamu wa kuchimba madini pamoja na kuwafundisha kanuni za usalama, afya na utunzaji wa mazingira katika migodi yao. Lakini pia watapewa mafunzo kwa vitendo katika mgodi wa Stamigold pale itakapohitajika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mgodi huo uko tayari na ulishaanza kuwasaidia wananchi wa Kijiji cha Mavota. Kati ya tarehe 26 na 30 Juni, 2015, Mavota Gold Mine Group kilipewa ushauri wa namna bora ya kuendesha shughuli za uchimbaji na utafiti wa dhahabu katika eneo walilomilishwa leseni. Kikundi hicho kilimilikishwa leseni ya uchimbaji mdogo yenye Namba PL 001493WLZ iliyotolewa tarehe 23 Februari, 2015. Eneo hilo lina ukubwa wa hekta 9.43.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgodi umetoa fursa za ajira kwa vijiji vya jirani. Vijana wenge ajira za muda mrefu kutoka vijiji vya jirani ni 15 na wafanyakazi wenge mikataba ya muda mfupi ni 54.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mgodi umetoa fursa za kibashara kwa vikundi vitatu kutoka vijiji vya Mavota pamoja na Mkukwa ambapo wanavikundi hushirikiana kutafuta mazao ya kuuza mgodini kwa kuwasilisha mazao hayo kila wiki. Mazao hayo ni pamoja na viazi vitamu, mihogo, mboga za majani pamoja na matunda. Kutokana na kufanya biashara na Stamigold kati ya kipindi cha Julai 2014 na Disemba 2015, vikundi vyote vitatu vimeweza kujipatia zaidi ya shilingi milioni 200.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mukasa swali la nyongeza.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri yenye kuakisi nia ya Wizara na Serikali kushirikiana nasi, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la msingi, imeelezwa vizuri kabisa kwamba uvunjifu wa amani ni moja ya matokeo hasi ya kukosekana kwa fursa hizi za wananchi wa Mavota kushiriki kwenye uchumi uliowazunguka. Kwa sababu suala la uvunjifu wa amani si suala la kusuburi, ni la haraka, je, Serikali na Wizara iko tayari kutoa kauli inayothibitisha uharaka wao katika kuja kuzungumza na wananchi wa Mavota?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua ambazo Serikali imechukua kupitia Wizara yetu ni pamoja na kuhakikisha kwamba uchimbaji salama na makini unafanyika kwenye eneo hilo.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu huo, ofisi yetu iko tayari kwenda kuzumgumza na wananchi kuwahakikishia amani zaidi kwenye shughuli za uchimbaji eneo la Mavota.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa maswali yetu lakini nina matangazo kadhaa hapa, nitayasoma kabla hatujaendelea.

Tangazo la kwanza linahusu wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, tunaanza na wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Kundi la kwanza ni wageni watano wa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbewe, ambao ni viongozi wa Baraza la Vijana la CHADEMA wakiongozwa na Ndugu Patrobas Katambi, Mwenyekiti wa BAVICHA, karibuni sana. (Makofii)

Kundi lingine ni wageni 18 wa Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. (Makofii)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Godbless Lema ambao ni Meya wa Jiji la Arusha, Ndugu Kalisti Lazaro na Diwani wa Kata ya Baraza, Ndugu George Mbitika, karibuni sana. (Makofii)

Wageni wawili wa Mheshimiwa January Makamba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni wapiga kura wake, karibuni sana. (Makofii)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa kutoka Jimbo la Biharamulo Magharibi ambao ni watoto wake, karibuni sana. (Makofii)

Wageni kumi wa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa William Olenasha ambao ni wanafunzi kumi wa St. John's University, karibuni sana. (Makofii)

Mgeni wa Mheshimiwa Margaret Sitta, Mbunge wa Urambo, Ndugu Mark Kefa Kijo ambaye ni mijukuu wake, karibu sana. (Makofii)

Wageni 11 wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Jimbo la Ushetu, karibuni sana. (Makofii)

Wageni watano wa Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ambao ni viongozi kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (SSRA), wakiongozwa na Mkurugenzi wa Utafiti, Sera na Tathmini, Ndugu Ansgar Mushi, karibuni sana. (Makofii)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wanafunzi 40 kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Dodoma, ambapo 20 wanasoma Shahada ya Uzamili ya Mipango na Utawala wa Mazingira na wengine 20 ni wanafunzi wa Shahada ya Kwanza ya Mipango ya Rasilimali Watu. Wameongozwa na Mhadhiri wa Chuo Kikuu hicho, Dkt. Godrich. Naona kama idadi haijatimia, hapa mmeandikwa 40, hapo hata kumi hamjafika. (Makofii)

Wanafunzi 40 wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kutoka Dar es Salaam. Karibuni sana. Tunaishia hapo kwa upande wa wageni. (Makofii)

Tangazo lingine, nimeombwa niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa mama Salome Andrew Komba, kwa niaba ya familia ya aliyekuwa Mbunge wa Nyasa, Marehemu Kapteni John Damiano Komba, anawaalika Waheshimiwa Wabunge wote katika misa ya kumbukumbu ya kutimiza mwaka mmoja tangu Marehemu Kapteni John Komba afariki. Misa hiyo itafanyika siku ya Jumapili tarehe 28 Februari, 2016, kuanzia saa 2.45 asubuhi katika Parokia ya Bikira Maria Mama wa Huruma, Mbezi Beach na baadaye nyumbani kwa marehemu, Mbezi Beach. Tangazo limeletwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mengine mawili. Tangazo la kwanza ni Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa atatoa ufanuzi kuhusu Watanzania ambao walidhalilishwa nchini India katika Mji wa Bangalore, halafu akimaliza, nitamkaribisha Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ili aweze kutangaza Baraza lake la Mawaziri Kivuli. Mheshimiwa Waziri.

WABUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Naomba tukae. Mheshimiwa Waziri, karibu.

KAULI ZA MAWAZIRI

Taarifa ya Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa Kuhusu Wanafunzi wa Kitanzania Waliodhalilishwa Bangalore – India

WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilikuwa nimetoa taarifa ya awali kuhusu matukio huko Bangalore katika Jimbo la Karnataka - India, ambako wanafunzi wa Kitanzania walipigwa na mmoja wao msichana alidhalilishwa kwa kuvuliwa nguo na kutembezwa hadharani barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa tulizopata, zinathibitisha kwamba kweli kitendo hicho kilitokea na kilifuatia uendeshaji mbaya wa gari na mwanafunzi kutoka Sudan ambaye aligonga pikipiki tatu na baada ya hapo akamgonga mama wa Kihindi aliyefariki pale pale barabarani.

Baada ya tukio hilo, huyo mwanafunzi wa Sudan alikimbia. Wananchi wa India waliokuwa jirani walichoma gari lake na punde kidogo gari lingine lilifuata likiwa na wanafunzi wanne wa Tanzania, mmoja msichana na watatu wavulana. Walilisimamisha gari lile na kuwavuta wale wanafunzi nje na wakamchukua yule msichana na kumvua nguo na kuanza kumtembeza barabarani uchi. Wale wavulana walipigwa na gari lao lilichomwa moto. Katika gari ile walikuwa na simu zao na documents zao mbalimbali nazo ziliteketea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo polisi walikuja lakini hawakutoa ushirikiano wa kutosha. Hata hivyo, waliweza kuwapeleka wale wanafunzi hospitali na kule hospitali walionekana wana majeraha makubwa, wakatibiwa lakini ikabidi waondoke kwa sababu walikuwa hawana pesa za kutosha kugharamia matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, Ubalozi wetu India, kama nilivyosema jana, uliandika Dokezo la Kidiplomasia kwa Serikali ya India kulaani kitendo hicho na kuitaka Serikali ya India ichukue hatua za kisheria na za haraka kupeleleza kufuatia matukio hayo. Kwa upande wetu kama Wizara, jana tulimuita Balozi wa India aliyepo hapa nchini na kumueleza jinsi Serikali na wananchi wa Tanzania walivyofadhaika na kuchukizwa na kitendo hicho. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi alituambia kwamba na yeze amejulishwa na Serikali yake kuhusiana na suala hilo na Serikali ya India na Waziri mwenyewe wa Mambo ya Nchi za Nje wa India alitoa taarifa rasmi kule New Delhi, kwanza kuomba radhi kwa Tanzania na Watanzania waliopo India kwa kitendo hicho kilichotokea. Pia akaagiza Serikali yake ichukue hatua za kisheria na kupeleleza na kuwakamata wale waliohusika na wote sasa wamekamatwa na wamepelekwa mahakamani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali ya India iliagiza kwamba wanafunzi wa Tanzania wapewe ulinzi maalum kule wanakoishi na waweze kusindikizwa wanapokwenda masomoni au madarasani. Tatu, Serikali ya India ilimtaka Balozi wetu afuatane na Maafisa Waandamizi wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya India kwenda Bangalore ili kukutana na wanafunzi wa Tanzania na wengine wa Afrika lakini pia kukutana na jumuiya ya maeneo ambayo Watanzania wanaishi kwa sababu vitendo hivi vinaashiria ubaguzi na kuweka mahusiano mazuri kati ya wanafunzi na wenyeji katika maeneo ya mji huo na hasa maeneo yale ambapo wanaishi. Hilo limetokea, Balozi wetu amefuatana na maafisa hao kwenda Bangalore na mikutano hiyo imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana pia nilieleza kwamba kuna mwanafunzi mmoja ambaye alifariki karibu na maeneo hayo hayo. Taarifa za awali zilikuwa zinatatanisha, tukadhani kifo hicho kilitokana na tukio hilo la kuvamiwa wanafunzi wetu lakini si kweli.

Mwanafunzi huyo Mtanzania, alikuwa anaendesha pipipiki bila kofia, akagonga nguzo ya taa na kufariki pale pale. Ubalozi wetu unashughulikia mazishi na mwili wake utarudishwa Tanzania mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo taarifa ambayo ilitokana na swali la jana nimeona ni vema nilijulishe Bunge lako Tukufu. Ahsanteni sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, namkaribisha Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mboge, Mbunge wa Hai na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ili aweze kutangaza Baraza lake la Mawaziri Kivuli.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 15(2) inayosema kuwa na nanukuu; "Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni atateua Wabunge wa Chama chake au Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambao watakuwa wasemaji wakuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara zilizopo za Serikali."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutimiza matakwa ya Kanuni tajwa hapo juu, naomba sasa kuwasilisha rasmi kwa Bunge na kwa Tanzania kwa ujumla, majina ya Waheshimiwa Wabunge watakaokuwa Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni na kwa Wizara za Serikali zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaanza na Ofisi ya Rais (TAMISEMI), atakayekuwa Waziri Kivuli na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani ni Mheshimiwa Japhary Michael na Naibu wake atakuwa ni Mheshimiwa Joseph Mkundi. (Makofi)

Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Msemaji Mkuu na Waziri Kivuli atakuwa Mheshimiwa Ruth Mollel. (Makofi)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano, Waziri Kivuli na Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani atakuwa Mheshimiwa Ally Saleh Abdallah Ally na Naibu wake atakuwa Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul. (Makofi)

Ofisi ya Waziri Mkoo, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu, Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani atakuwa Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, akisaidiwa na Naibu Mawaziri wawili ambao ni Mheshimiwa Yussuf Kaiza Makame na Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma. (Makofi)

Fedha na Mipango, Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani Bungeni ambaye atakuwa ni Waziri Kivuli ni Mheshimiwa Halima Mdee na Naibu wake atakuwa ni Mheshimiwa David Silinde. (Makofi)

Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani ambaye atakuwa Waziri Kivuli wa Wizara hii ni Mheshimiwa Eng. James Francis Mbatia na Naibu wake atakuwa ni Mheshimwa Willy Qambalo. (Makofi)

Wizara ya Nishati na Madini, Msemaji Mkoo atakuwa ni Mheshimiwa John John Mnyika na Naibu wake atakuwa ni Mheshimiwa John Heche. (Makofi)

Waziri wa Mambo ya Nje, Afrika Mashariki na Mawasiliano ya Kimataifa Msemaji Mkoo wa Kambi yetu atakuwa ni Mheshimiwa Peter Msigwa na Naibu wake atakuwa ni Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali. (Makofi)

Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Waziri Kivuli ambaye ni Msemaji Mkoo wa Kambi atakuwa ni Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Naibu wake atakuwa ni Dkt. Immaculate Sware Semesi. (Makofi)

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Msemaji Mkoo wa Kambi atakuwa ni Juma Hamad Omar na Naibu wake atakuwa ni Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara. (Makofi)

Wizara ya Mambo ya Ndani, Msemaji Mkoo ambaye atakuwa Waziri Kivuli, atakuwa ni Mheshimwa Godbless Lema na Naibu wake atakuwa ni Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim. (Makofi)

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Msemaji Mkoo wa Kambi atakuwa ni Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare na Naibu wake atakuwa ni Mheshimiwa Salma Mohamed Mwasa. (Makofi)

Wizara ya Maliasili na Utalii, Msemaji Mkoo wa Kambi yetu atakuwa ni Mheshimiwa Esther Matiko na Naibu wake atakuwa ni Mheshimiwa Cecilia Parezzo. (Makofi)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wizara ya Viwanda Biashara na Uwezeshaji, Msemaji Mkoo wa Kambi atakuwa ni Mheshimiwa Antony Calist Komu na Naibu wake atakuwa ni Mheshimiwa Cecil Mwambe. (Makofii)

Wizara ya Elimu, Teknolojia na Ufundji, Msemaji Mkoo wa Kambi atakuwa ni Mheshimiwa Susan Lyimo akisaidiana na Mheshimiwa Naibu Waziri Kivuli Mheshimiwa Dkt. Ally Suleiman Yussuf. (Makofii)

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ni Dkt. Godwin Mollel ambaye atakuwa Msemaji wa Kambi akisaidiana na Mheshimiwa Zubeda Sakuru kama Naibu Waziri Kivuli. (Makofii)

Wizara ya Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo, Msemaji Mkoo wa Kambi yetu ambaye atakuwa ni Waziri Kivuli ni Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na Naibu wake atakuwa ni Mheshimiwa Devotha Ninja. (Makofii)

Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Msemaji Mkoo wa Kambi ambaye atakuwa ni Waziri Kivuli ni Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali na Naibu wake atakuwa ni Mheshimiwa Peter Lijualikali. (Makofii)

Wizara ya Katiba na Sheria, Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani ambaye atakuwa ni Waziri Kivuli ni Mheshimiwa Tundu Antipas Lissu akisaidiana na Mheshimiwa Abdallah Mtolea ambaye atakuwa Naibu wake. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ndiyo Baraza letu, tunaomba wale wote wanaohusika watoe ushirikiano kwa Baraza hili kadiri itakavyowezekana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (Makofii)

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. RAMADHAN I. ABDALLAH - KATIBU MEZANI: Kamati ya Mipango, majadiliano yanaendelea.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Kamati ya Mipango.

KAMATI YA MIPANGO

(Majadiliano yanaendelea)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, dakika kumi. Mheshimiwa Naibu Waziri jana ilikuwa upewe dakika kumi sasa unapewa leo, unayo hoja ama huna?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namwachia dakika zangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kama Naibu Waziri hana hoja asubuhi hii basi Bunge litarejea ili Waziri aendelee.

(Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mwongozo wa Spika.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nitaruhusu Mwongozo mmoja...

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mwongozo wa Spika.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mwongozo wa Spika.

MBUNGE FULANI: Miongozo ipo Kikanuni.

NAIBU SPIKA: Nasema hivi nitaruhusu Mwongozo moja lakini tukumbuke kwamba hii Kanuni kuhusu Mwongozo ni kuhusu mambo yaliyotokea leo ambayo unataka Kiti kitoe maelezo kama jambo liliofanyika ni sawasawa ama siyo sawasawa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Ndiyo

NAIBU SPIKA: Naomba tukumbuke hilo kwa sababu kuna muda tumesimama wengi...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: La leo Mheshimiwa.

NAIBU SPIKA: Mpaka haionekani kama kuna jambo lolote ambalo limefanyika sawasawa.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Ni la leo Mheshimiwa Naibu Spika.

NAIBU SPIKA: Natoa Mwongozo mmoja Mheshimiwa Mnyika.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Aah. Mwongozo wa Spika.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni kuhusu utaratibu.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mnyika, naomba usubiri kidogo. Mheshimiwa Susan, utaratibu unatajwa wakati gani? Soma Kanuni vizuri ni muda gani unasema Kuhusu Utaratibu ni lazima kuwe na mtu anaongea, haendi sawasawa ndiyo unaomba utaratibu. Huwezi kuomba utaratibu wakati hamna mtu anayeongea.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wa Kiti.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mnyika endelea.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mapema leo tumekabidhiwa Orodha ya Shughuli za leo za Mkutano Pili, Kikao cha Tisa, ambapo katika ukurasa wa kumi na moja sehemu ya tano inaonyesha hoja ya Waziri Mkuu ya Kuliahirisha Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina dhamira ya kuwahisha shughuli, naomba Mwongozo wako kwa sababu katika Bunge la Kumi kulitolewa pendekeso na ukafanyika uamuzi na Waziri Mkuu akakubali kwamba katika kila Mkutano wa Bunge Serikali itakuwa inawasilisha Bungeni, na hii ilitokana na Wabunge wengi sana kuwa na malalamiko juu ya masuala ya maji, taarifa kwa Wabunge wote ya miradi mbalimbali ya maji katika maeneo mbalimbali ya Wabunge wote. Aliyekaimu shughuli za Serikali Bungeni wakati huo Mheshimiwa Mwandosya alikubali Azimio hilo na likapitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa sababu huu ni Mkutano wa Pili wa Bunge na unakwenda kuahirishwa na hakuna taarifa kama hiyo ambayo imewasilishwa na Serikali, kama hali hii ikiruhusiwa Bunge litakuwa linadharauliwa na Serikali katika mambo mbalimbali.

Naomba Mwongozo wako ili Waziri Mkuu kabla ya kuahirisha Bunge aweze kutimiza matakwa haya ambayo yalishakuwa ya Kibunge.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nitatoa Mwongozo baadaye nikishalifua tilia jambo hilo na kujua linapaswa kwendaje. Katibu.

NDG. RAMADHAN I. ABDALLAH - KATIBU MEZANI: Kamati ya Mipango, majadiliano yanaendelea.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nilisema nitatoa Mwongozo mmoja na nimeshautoa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni matakwa ya Kanuni.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hizi Kanuni kama zingekuwa zinasema namna ambavyo kila mtu anataka, Bunge lingekuwa haliwezi kuendeshwa. Ndiyo maana Kanuni hizi hizi tunazotumia ndizo zilizotoa fursa kwa Spika au kiti kuona namna bora ya uendeshaji na namna bora ya uendeshaji kwa shughuli tulizonazo leo ni hiyo ya kutoa mwongozo mmoja ili tuweze kuendelea na shughuli. (Makofi)

MHE. GODBLESS J. LEMA: Kuhusu Utaratibu.

MBUNGE FULANI: Unampa nani?

MBUNGE FULANI: Yeye mwenyewe.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hamna mtu anayeongea ili kuwe na Kuhusu Utaratibu. Tuendelee Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Kaa chini.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Spika na wewe mwenyewe, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha vizuri majadiliano kuhusu Mapendelekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa lakini pia Mwongozo wa kuandaa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017, hotuba ambayo niliwasilisha tarehe 1 Februari, 2016.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutambua michango iliyotolewa na Kamati ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa MtWARA Vijiji lakini pia aliyekuwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mombasa. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza au kwa maandishi. Waheshimiwa Wabunge 121 wamechangia kwa kuzungumza na 30 wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijiji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa kunipatia dakika zake kumi ili niweze kuzitumia kutoa majumuisho hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nianze na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ambao ulisitisizwa sana. Kwa kuwa tulichowasilisha ni Mapendekezo ya Mpango na Waheshimiwa Mawaziri wenye dhamana ya kusimamia sekta mbalimbali walipata nafasi ya kutoa maelezo yao basi nitakuwa na machache sana juu ya sekta moja moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla tumepokea ushauri mzuri ambao naomba kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba tutautumia kuandaa Rasimu ya Mpango wenyele lakini pia kuandaa mapendekezo ya kiwango na ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017. Taarifa zote mbili zitawasilishwa kwa Wabunge tarehe 11 Machi, 2016, ambayo itakuwa ni siku ya kazi, siku ya Ijumaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze mambo makubwa ambayo yalisisitizwa sana na Waheshimiwa Wabunge.

Kwanza, Waheshimiwa Wabunge wameshauri tuweke nguvu kubwa katika ukusanyaji wa mapato kutoka katika vyanzo vyaa sasa na vyanzo vipyaa ili kuongeza bajeti ya maendeleo na kuhakikisha fedha inatolewa kama ilivyo pangwa.

La pili ilisisitizwa kwamba ni lazima sasa tuongeze uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme, tatu, ujenzi wa reli ya kati na matawi yake yote nchini kwa kiwango cha standard gauge na nne, Serikali ipeleke fedha zaidi kutekeleza programu na miradi ya maji mijini na vijiji kwa matumizi ya binadamu, mifugo, viwanda na umwagiliaji lakini ikiwa ni pamoja na dhamira ya Serikali ya kupunguza adha kubwa kwa akina mama. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo tumepokea ni kwamba ni lazima katika Mpango ujao tuendeleze jitihada za kujenga na kuimarisha miundombinu ya bandari, reli, barabara, viwanja vyaa ndege na kuboresha huduma husika ikiwa ni pamoja na usafiri katika maziwa makuu na bahari kwa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kununua meli mpya na kukarabati zilizopo. Pia tumeshauriwa kwamba Mpango ujao usisitize kutenga na kupima ardhi kwa ajili ya kilimo cha mazao na ufugaji ili kuepuka migogoro na kulipa fidia ya ardhi kwa ajili ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ilisisitizwa kwamba tuwekeze zaidi katika kilimo cha mazao, mifugo, uvuvi na misitu ili kiweze kutupatia chakula cha kutosheleza mahitaji ya ndani na kuuza ziada nje lakini pia kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya malighafi za viwandani na masoko ya Kikanda na Kimataifa. Tulipokea ushauri pia kwamba Shirika letu la Ndege (ATCL) lifanyiwe mageuzi makubwa yaani *restructuring* na kununua ndege mpya kwa kuhusisha taasisi zinazohusika na utalii ili kuwa na National Airline endelevu na yenyе ufanisi. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, ilisisitizwa pia kwamba ujenzi wa viwanda uanze kwa kufufua viwanda vilivyopo na vile vinavyotumia malighafi zinazopatikana hapa nchini hususan viwanda ambavyo vitatumia ngozi lakini pia viwanda vya nyama, maziwa, matunda, asali, mbao, pamba, korosho, mafuta ya mbegu, uchakataji wa samaki na kuongeza thamani ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwagine tulioupokea na ulisemwa sana ni kwamba viwanda vidogo vipewe msukumo pamoja na kulinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani mkali kutoka nje. Lakini pia elimu inayotolewa iwiante na mahitaji ya viwanda hususan rasilimali watu yenyе uwezo na ujuzi na ilisisitizwa sana elimu ya ufundi na ufundi stadi. Jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge walisisitiza ni kwamba sera ya elimu msingi bila malipo iende sambamba na uboreshaji wa miundombinu ya elimu, hususan ujenzi wa madarasa, vifaa vya maabara, upatikanaji wa madawati na kuhakikisha kwamba walimu wa sayansi wanakuwepo. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokea ushauri kwamba katika Mpango ujao ni muhimu kuongeza kasi ya kuboresha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara nchini. Pia kupiga vita rushwa, urasimu, kuboresha miundombinu na kuharakisha maamuzi. Yalisemwa mengi, naomba niseme moja la mwisho ambalo ilisisitizwa sana nalo ni kwamba Mpango wa Maendeleo 2016/2017 ujielekeze katika miradi inayogusa maisha ya watu na hasa makundi ya watu maskini na wale wenye mahitaji maalum. Baadhi ya maeneo yaliyosisitizwa ni barabara za vijijini, nyumba za walimu, zahanati na vituo vya afya lakini pia programu ya kuwawezesha wachimbaji wadogo na maeneo yenyе uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza baadhi ya maeneo makubwa ambayo yalisisitizwa sana na Waheshimiwa Wabunge, naomba uniruhusu nianze kufanua baadhi ya hoja ambazo zilijitokeza na naomba nianze na zile zinazohusu uchumi jumla.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja moja ilikuwa kwamba kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi kwa takribani asilimia 7 haigusi maisha ya wananchi wengi hasa wanaoishi vijijiini. Ni kweli kuwa uchumi wa Taifa umekua kwa kasi kubwa. Kwa zaidi ya muongo mmoja na nusu sasa uchumi wa Taifa letu, kwa maana ya *real GDP growth* umefika wastani wa asilimia saba kwa mwaka. Tanzania ni mionganoni mwa nchi kumi ambazo uchumi wake unakua kwa kasi kubwa katika Bara la Afrika. Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita 2010 - 2014, uchumi wa Taifa ulikua kwa wastani wa asilimia 6.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha umaskini kikipimwa kwa mahitaji ya msingi (*basic needs poverty*), kimepungua kwa takribani asilimia 6.2 kutoka asilimia 34.4 mwaka 2007 mpaka asilimia 28.2 mwaka 2012. Hili lilitokana kwanza na kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi lakini pia juhudhi za Serikali katika kuboresha upatikanaji wa huduma muhimu hususan maji, afya, elimu na ujenzi wa miundombinu. Umaskini ukipimwa kwa kutumia kigezo cha chakula (*food poverty*) nao ulipungua kutoka asilimia 11.8 mwaka 2007 hadi asilimia 9.7 mwaka 2012. Hata hivyo, ni ukweli pia ulio bayana kwamba kiwango cha umaskini bado ni kikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama pia vigezo vya umaskini ambavyo siyo wa kipato, takwimu zilizopo zinaonesha ulipungua. Hili linadhishirishwa na Watanzania ambao sasa wana kaya ambapo nyumba zao zimejengwa kwa kutumia saruji na mabati, kaya zinatumia umeme, kaya zinamiliki nyumba zao, wananchi wana simu za mkononi, radio luninga, baiskeli, pikipiki lakini pia kumiliki ardhi na mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nieleze changamoto mbili kubwa ambazo zinasababisha kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi tuliyonayo isijidhirishhe katika kasi kubwa zaidi ya kupunguza umaskini.

Changamoto ya kwanza ni kwamba sekta zinazokua haraka ambazo ni ujenzi, mawasiliano, huduma za fedha na bima, hajajiri watu wengi. Sekta ya kilimo ambayo ndiyo mwajiri wa Watanzania walio wengi imekua kwa kasi ndogo ya wastani wa asilimia 3.6 kwa mwaka. Sababu zake ni nydingi ikiwemo tija ndogo, teknolojia ya kale lakini pia matatizo ya mitaji, kutegemea mvua, shida za masoko na hata tozo na kodi za kero mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili, ni kasi ya ongezeko la idadi ya watu ambayo ni kubwa bado takribani asilimia 2.7 kwa mwaka. Ukuaji halisi wa uchumi wa Taifa kwa ujumla, ukizingatia kasi ya ongezeko la idadi ya watu, maana yake ni kwamba uchumi wa Taifa unakua kwa asilimia nne tu ambayo inapatikana kwa kuchukua wastani wa ukuaji kwa uchumi asilimia 6.7 ukatoa kasi ya ongezeko la idadi ya watu ambayo ni asilimia 2.7. Mbaya zaidi kwa kuwa wastani wa ukuaji katika sekta ya kilimo ni takribani asilimia 3.6 tu

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maana yake ni kwamba kama unazingatia ukuaji wa idadi ya watu, sekta ya kilimo kiuhalisia inakua kwa asilimia 0.9 peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hizi ndiyo sababu za msingi kwa nini kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi haijaonekana sana kwa maana ya kupungua kwa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi kubwa ya ukuaji wa idadi ya watu inapeleka familia nyingi hasa vijiji kuwa na idadi kubwa ya wategemezi na kushindwa kuweka akiba ya kutosha kwa ajili ya kumudu mahitaji yao ya maisha lakini pia huduma za jamii na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii maana yake nini? Ili tuweze kuhakikisha kwamba kasi ya ukuaji wa uchumi inagusa wananchi wengi, moja, inabidi kuongeza kasi zaidi ya ukuaji wa uchumi. Hakuna nchi popote ulimwenguni ambapo umaskini umepungua bila kuwa na kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi wake. Kwa Tanzania tunakadiria kwamba siyo asilimia saba tena, tunatakiwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa Taifa uende hata kufika asilimia 10 na zaidi. Hili litawezekana kama tutajielekeza kuongeza tija katika kilimo, kwa maana ya kutumia mbegu bora, mbolea, upatikanaji wa mikopo, kujikita katika kilimo cha umwagiliaji lakini pia ujenzi wa maghala na kuhamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vyta kuchakata mazao na kulenga kukuza kilimo cha mazao yenye thamani kubwa na masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja alishawishi kwamba kati ya mazao yenye thamani kubwa ni pamoja na mirungi na bangi. Nafikiri yako mazao mengi ambayo yana thamani kubwa na hayana madhara kama haya yanayopendekezwa. Ningeshauri tujielelekeze huko zaidi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa pili ni kupunguza kasi ya ongezeko la idadi ya watu. Hapa kikubwa ni kuweka mikakati ya kusaidia kuhakikisha kwamba wasichana wengi na hususan kutoka familia maskini, wanaendelea na masomo ya sekondari na elimu ya juu. Mkakati wa kutoa elimu bure ni muhimu sana kwa kipindi cha muda wa kati na muda mrefu kwa ajili ya kupuguza kasi ya ongezeko la watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa tatu, ni kupanua fursa za ajira katika shughuli na huduma zenyne mahusiano ya karibu na zile sekta nilizozitaja ambazo uchumi wake unakua haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kwamba matumizi ya dola kwa malipo ya bidhaa na huduma hapa nchini ni vyema yakadhibitiwa. Utafiti ambao Benki Kuu imefanya unaonesha kuwa ni asilimia 3.2 tu ya wafanyabiashara wote ndiyo wanaoweka bei kwa dola na ni asilimia

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

0.1 tu ya wafanyabiashara ndiyo wanaodai kulipwa kwa dola peke yake. Utafiti huo unabainisha kwamba ukiacha mahoteli ambayo wameruhusiwa, kubadilisha fedha za kigeni, maeneo sugu ambayo bei zinatajwa kwa dola ni pamoja na nyumba za kupanga na baadhi ya taasisi za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya dola sambamba na shilingi tunatambua kwamba yanaweza kuchochea utoroshwaji wa fedha za kigeni lakini pia mitaji kwa maana ya *capital flight* kwenda katika mabenki nje ya nchi. Kwa kawaida wanakuwa wanakimbia usumbufu katika kupata fedha za kigeni. Pia kama unadhibiti dola kupita kiasi mara nyingi inasababisha dola iuzwe kwa bei kubwa zaidi mitaani yaani kwenye *black market*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inatambua shilingi ya Tanzania ndiyo fedha halali kwa malipo ya bidhaa na huduma hapa nchini yaani ndiyo *legal tender*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tamko la Serikali la Agosti, 2007, liliagiza kuwa bei zote nchini zitangazwe katika shilingi. Maana yake ni kwamba shilingi ya Tanzania haipaswi kukataliwa na mtu ye yote kwa malipo halali hapa nchini na mtu hapaswi kulazimishwa kufanya malipo yoyote kwa dola.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kikubwa kwa kuzingatia kwamba idadi ya wafanyabiashara ambao wanadai dola, kama nilivyoeleza hapo awali ni ndogo na kwa kuzingatia faida ambazo wananchi wenzetu wanaofanya biashara wanapata kwa kuwa na akiba zao za dola wenye ambayo inawarahisishia kufanyabiashara, lililo kubwa ni kusimamia sheria lakini pia Benki Kuu kuendelea kusimamia *Bureau de Change* na kuzitaka zitumie *Electronic Fiscal Devices* ili tuweze kupata taarifa sahihi za miamala yao na kodi stahiki iweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ilijitokeza ni kwamba Serikali ina mkakati gani kudhibiti kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola. Ni kweli thamani ya shilingi imeshuka kwa kasi katika kipindi cha karibuni, kwa mfano, mwezi Januari, 2015, dola moja ya Kimarekani ilikuwa inabadilishwa kwa shilingi za Kitanzania 1,782.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Disemba, 2015, dola hiyo hiyo moja ya Kimarekani ilikuwa inabadilishwa kwa shilingi 2,148.5. Kushuka huku kwa thamani kuna sababu nyingi, mojawapo ni kuimarika kwa dola dhidi ya sarafu nyingine duniani wala siyo kwa shilingi peke yake. Hii imetokana na uchumi wa Marekani kuwa mzuri na kuwavutia wawekezaji wengi kukimbilia kuwekeza zaidi katika dola.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli pia kwamba katika miezi ya karibuni tumeona bei ya dhahabu katika soko la dunia ikiporomoka sana pia baadhi ya mazao ambayo tunauza katika masoko ya nje hasa pamba nayo pia yaliteremka. Hii maana yake mahitaji yetu ya kuweza kununua bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi yalikuwa hayawezi kukidhiwa na mauzo yetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyingine mwaka 2015 ulikuwa na changamoto mbalimbali ambapo tulishuhudia misaada ya kibajeti ambayo inaingia kwetu katika fedha za kigeni ilichelewa kutufikia na mingine haikuja kabisa. Vilevile palikuwepo na ongezeko la mahitaji ya dola kwa ajili ya malipo ya gawio nje ya nchi kwa baadhi ya makampuni binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunafanya nini? Hatua za kuimarisha thamani ya shilingi ni pamoja na kuongeza mauzo yetu nje ya nchi na hili ni lazima tulifanye kwa kutafuta bidhaa ambazo zina soko kubwa, zina thamani zaidi katika masoko ya nje lakini pia lazima tupanue wigo wa bidhaa ambazo tunauza nje ya nchi yaani export diversification. Tunahitaji kudhibiti biashara ya fedha za kigeni ambazo haziambatani na shughuli za kiuchumi kwa maana ya currency swaps. Vilevile tunahitaji kupunguza ujazi wa fedha katika uchumi ili kudhibiti miamala ambayo inafanyika katika soko la fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojiteza ilikuwa kwamba Serikali haikutenga asilimia 35 ya bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Miaka Mitano. Hili siyo kweli hata kidogo na wengine walidai kwamba Serikali wakati mwingine haijawahi kutenga hata senti moja kutekeleza miradi ya maendeleo.

Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Serikali ilipanga kutenga bajeti ya maendeleo kwa wastani wa asilimia 35. Kuanzia mwaka 2011/2012, Serikali iliweza kutenga fedha kama ifuatavyo: Shilingi trilioni 3.8 mwaka 2011/2012, shilingi trilioni 4.5 mwaka 2012/2013 na shilingi trilioni 4.6 mwaka 2014/2015 na mwaka huu unaoendelea zilitengwa shilingi trilioni 5.9 na mwaka ujao kama nilivyosema wakati nawasilisha hoja yangu tunatarajia kwamba bajeti ya maendeleo itafikia shilingi trilioni 6.02.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kuwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Serikali ilitenga fedha za maendeleo kwa wastani wa asilimia 27 kwa hiyo, miaka yote mitano ikilinganishwa na lengo la asilimia 35.

Kwa hiyo, ukiliangalia tu hivi, unaweza ukasema kwamba hatukufikia asilimia 35. Hii siyo kweli kwa sababu kwa jinsi mfumo wa bajeti ulivyo, yapo

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

matumizi ambayo yanahesabiwa kwamba yako kwenye matumizi ya kawaida lakini kiuhalisia ni matumizi ya maendeleo. Mathalani fedha kwa ajili ya elimu na afya, hizi tunawekeza kwa ajili ya kesho lakini tunapoandika vitabu vya bajeti zinahesabika kuwa upande wa *recurrent* lakini hizi kwa kweli tunawekeza ni fedha za maendeleo. Hata zile za kulipia deni la Taifa, nazo zinahesabika ni *recurrent* lakini kwa kweli tumekopa kwa ajili ya maendeleo na hivyo hizi ni fedha ambazo kiuhalisia ni kwa ajili ya *development*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ukijumlisha matumizi yote haya pamoja na yale ya asilimia 27 niliyosema, wastani wa bajeti ya maendeleo kwa mwaka inafika asilimia 48 ya bajeti ya Serikali kwa kipindi hicho cha Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Pia ni vizuri nikiri kwamba kutokana na matumizi ya lazima, kwa mfano, kugharamia Bunge la Katiba, Uchaguzi Mkuu, kununua chakula cha hifadhi sambamba na ukusanyaji wa mapato kutofikia malengo na wahisani kupunguza misaada yao ya kibajeti, kuna kipindi haikuwezekana kutoa fedha zote za maendeleo kama ilivyokuwa imepangwa awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihamie kwenye baadhi ya hoja ambazo zinahusu mwongozo wa bajeti. Hoja moja kubwa iliyojitokeza ilikuwa kwamba uamuzi wa kufuta utaratibu wa kubakiza mapato (*retention*) usitekelezwe kwa kuwa ni kinyume cha Sera ya Ugatuaji Madaraka D by D na kwamba itaathiri shughuli mbalimbali kama uhifadhi wa mbuga za wanyama, huduma katika viwanja vyetu vya ndege na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba Sheria ya Bajeti, Na.11 ya 2015, kifungu cha 58(a)-(c) kinaelekeza kwamba mapato yote ya Serikali yakusanywe na kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na Bunge hili ndilo lililopitisha sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa *retention* ulianza zamani kidogo katika miaka ya 1996/1997 kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kukusanya mapato na kuziruhusu taasisi zinazokusanya maduhuli kubakiza sehemu ya fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya ukusanyaji. Pia ilikuwa ni kuipunguzia Serikali mzigo wa kupata fedha zaidi kutoka kwa taasisi hizo kwa ajili ya matumizi ya taasisi nyingine ambazo hazipo kwenye huo utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu unahuishaa baadhi tu ya Wizara na Taasisi za Serikali ikiwa ni pamoja na Wizara ya Nishati na Madini; Maliasili na Utalii; Mambo ya Nje; Ushirikiano wa Kimataifa; Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Viwanda, Biashara na Uwekezaji; Jeshi la Polisi; Idara ya Zima Moto; Jeshi la Magereza; Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Ujenzi, uchukuzi na Mawasiliano; Maji na Umwagiliaji; Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Ofisi ya Waziri Mkuu; Uhoniaji; Mfuko wa Mahakama; Ofisi ya Mkaguzi na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto. Nirudie kusitiza kwamba Serikali inakusudia kusitisha utaratibu huu kuanzia mwaka ujao wa fedha kama Sheria ya Bajeti inavyoelekeza. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya sababu ni kuwa taasisi zinazohusika zimeacha jukumu lao la msingi na kuegemea zaidi kwenye mapato. Pia ni dhahiri kuwa wakati taasisi ambazo zipo kwenye mfumo wa *retention* zinapata fedha nyingi bila kujali uhala wa fedha ambaa unakabili Wizara, Idara na Taasisi ambazo hazipo kwenye mfumo huu. Vilevile tumeshuhudia kwamba taasisi nyingi sasa nazo zinadai ziingie kwenye utaratibu huo. Siyo hivyo tu, pamoja na kubakiza sehemu ya mapato wanayokusanya bado tunashuhudiwa kwamba wanaendelea kulipwa mishahara kwa asilimia 100 kutoka kwenye Mfuko wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisitiza kwamba utaratibu huu sasa tunaufuta kuanzia mwaka ujao wa fedha lakini uamuzi huu hautahusu mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika maeneo yao na wala haitagusa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie kwa sababu hili halikueleweka ilivyo. Wakati nasoma hotuba yangu nilieleza bayana kwamba uamuzi huu hautahusu mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na ni kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali ya Mitaa, Na.9 ya 1982 lakini pia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii haitaguswa na utaratibu huu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majadiliano ilijitokeza hoja kwamba tufute utaratibu huu, lakini kuna ukiritimba Wizara ya Fedha katika utaoaji wa mapato. Kati ya Februari na Juni, 2016, tutakaa na wadau wote wanaohusika na *retention* ili tukubaliane utaratibu mpya wa kutoa fedha hizo. Tukishafanya makubaliano, tutaoa Waraka ambaa utaelekeza utaratibu mpya. Tunaamini kabisa uamuzi huu utasaidia sana katika ukusanyaji wa mapato kwa ufanisi, lakini pia utatusaidia katika kutunza hesabu na kutoa taarifa kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyokuwa moto ni uamuzi wa Serikali wa kuondoa fedha za taasisi zote za umma kutoka kwenye benki za biashara kwenda Benki Kuu. Hoja ilikuwa kwamba utaratibu huu utakuwa na madhara ya kiuchumi. Kwa kipindi kirefu mashirika ya umma yamekuwa yakinanza fedha zao katika mabenki ya biashara na kufanya matumizi kupitia benki hizo. Hata hivyo, kutohana na utaratibu huo, kumekuwa na ugumu wa kupata taarifa za mapato na matumizi ya mashirika hayo kwa wakati na kwa uhakika.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wa Serikali kufuatilia usahihi wa matumizi ya mashirika ya umma ili kujihakikishia kuwa wanaelekeza fedha hizo katika vipaumbele, umekuwa finyu sana. Hiyo ilisababisha baadhi ya mashirika kutochangia ipasavyo katika mapato ya Serikali. Vilevile baadhi ya taasisi zimekuwa zikiweka fedha katika akaunti za mabenki ya biashara kwa muda mrefu bila kuzitumia wala kuziwekeza na badala yake fedha hizo zimekuwa zikiwekezwa na mabenki husika ikiwa ni pamoja na kununulia hati fungani na dhamana za Serikali kwa riba kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la msingi ni kuwa fedha ambazo sasa tunatoa maelekezo kwamba zifunguliwe akaunti Benki Kuu bado zitabaki kuwa ni fedha za mashirika husika. Mashirika hayo yataendelea kufanya maamuzi kuhusu matumizi ya fedha hizo ikiwa ni pamoja na kuziwekeza kulingana na vipaumbele na miongozo ya Serikali. Lengo letu ni kuhakikisha kuwa tunapata taarifa sahihi za makusanyo yote yanayokusanywa na taasisi ya umma kama nilivyosema; kuhakikisha kwamba mashirika ya umma yanachangia ipasavyo kwenye mapato yasiyo ya kodi lakini pia kuhakikisha kuwa hakuna fedha zinakaa kwenye akaunti za mashirika bila mipango ya matumizi yake. Hatua hiyo pia itatuwezesha kupunguza utegemezi wa baadhi ya mabenki kwa fedha za mashirika na hivyo kufanya yajielekeze zaidi kufanya biashara na wananchi mijini na vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisitize tu kwamba akaunti zitakazofunguliwa Benki Kuu zitatumika kukusanya mapato yote ya mashirika ya umma kama *holding account* wakati akaunti za matumizi (*operational accounts*) zitaendelea kuwa katika mabenki ya biashara ili kuyawezesha mashirika kufanya miamala yake. Mwaka 2014/2015, hii ilikuwa ni moja ya ushauri wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwamba Serikali iondoe fedha za mashirika ambazo hazizalishi kutoka katika mabenki ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wasiwasi kwamba hatua hiyo italeta madhara ya kiuchumi, tarehe 22 Januari, mashirika yote yalikuwa na kiasi cha shilingi bilioni 435 kwenye akaunti za hundi (*current account*). Baada ya uamuzi huo, hadi kufikia tarehe 22 Januari, kiasi cha shilingi bilioni 238 kwa mashirika 15 kulishahamishiwa Benki Kuu na hakukuwa na athari zozote za kibenki zilizojitokeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nytingine muhimu sana ilihu kujenga reli ya katika kwa kiwango cha *standard gauge*. Nilishalieleza mwanzo na jana Waziri mwenye dhamana ya sekta hii alilitolea maelezo. Naomba nitoe maelezo upande wa ugharamiaji wa ujenzi wa reli hiyo. Kwanza, utafiti ambao umekwishafanyika, umebaini kuwa ili mradi huu uweze kuwa *commercially viable*, itahitajika reli yote na matawi yake kwenda nchi jirani yajumuishwe. Kwa hiyo, matawi ya kwenda Burundi - Rwanda - Congo kutokea Burundi na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Rwanda, ili mradi huu uwe *viable commercially*, inahitajika haya matawi yawe yamejumuishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kama Tanzania itaamua vinginevyo, kama nilivyosikia baadhi ya Wabunge wakisema kwamba sisi tuhangaike tu na reli yetu ya kati humu ndani...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, samahani kidogo, naomba umalize, una dakika tano za kuhitimisha.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kama tutaaamua vinginevyo, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tutakuwa tumekosa fursa kubwa kwa kuwa mzigo wa kusafirisha kwenye reli yetu ya kati kutoka ndani na matawi yake hautatosha kuweza kurudisha gharama ya kujenga reli hiyo. Pia nchi yetu itakosa fursa ya kunufaika na maendeleo mengine ambayo yapo katika nchi jirani na hasa soko na mizigo kutoka kwenye nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank*) na *World Economic Forum* ambao wamekuwa mstari wa mbele kugharamia *feasibility studies* na kutafuta *financing* kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, kwa hakika wataona ugumu sana kuendelea na initiative hii ambayo inaungwa mkono na *African Union* lakini pia *Southern Africa Infrastructural Development Initiative* ikiwa pamoja na *Development Bank of Southern Africa* ambayo inaratibu ufuatiliaji wa fedha za kujenga reli hii ya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya kujenga reli ya kati inakadirwa kuwa kati ya dola bilioni 7,000 mpaka bilioni 9.5 kama itajengwa kwenye tuta jipya. Kama itajengwa kwenye tuta liliopo itagharimu nusu ya fedha hizo. Kwa uchumi wetu ambapo tuna *GDP* ya dola bilioni 53 au shilingi trilioni 100 na zaidi, uchumi wetu bado ni mdogo kuweza kubeba mzigo huu. Mfuko wa Reli ni mdogo sana, kwa mwaka ni takribani shilingi bilioni 50 na kama tukiamua kwamba tunaweza kujenga reli yetu ya kati kwa hela hizo tu, itatuchukua takribani miaka 320 kujenga reli hiyo.

WABUNGE FULANI: Aaaaaah!

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Ndiyo namba zilivyo. Hata kama tungeweza kutumia mapato yetu yote ya kodi kwa mwaka ambazo ni takribani dola trilioni 12 itatulazimu kujinyima kabisa fedha zote hizo kwa mwaka 1.3 ili ziweze kufikia hizo trilioni 16 au dola bilioni 8. Hata tukiamua kwamba tunajenga kwa miaka minne maana yake itabidi kila mwaka tutenge shilingi trilioni 4 kwa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ajili ya kujenga reli hiyo. Kwa namba hizi, nataka kuonyesha tu jinsi ilivyo kazi ngumu kujenga reli yetu ya kati kwa kutumia bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijahitimisha, napenda kurejea kwa kusisitiza masuala muhimu ambayo yamebeba uzito wa pekee kwa Taifa letu kama yalivyoelekezwa kwenye mwongozo. Kwa kifupi, Maafisa Masuuli waandae bajeti ya mwaka ujao kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Na.11 ya 2015; ni lazima kuimarisha ukusanyaji wa mapato; ni lazima kusimamia matumizi ya Serikali na kuondokana na matumizi yasiyo na tija na ni lazima kulipa na kudhibiti ongezeko la madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliha kishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaendelea kuzingatia maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ili kuboresha maandalizi na utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Nirudie tena kuziomba Wizara na Idara za Serikali wazingatie yale ambayo yameelekezwa kwenye hotuba niliyoitaa na wazingatie Sheria ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nawaomba Waheshimiwa Wabunge kuunga mkono hatua zinazoongozwa na Wizara yangu za kuhakikisha kuwa tunaimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, ya kodi na yasiyo ya kodi na kuelekeza matumizi kwenye maeneo yenye tija kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofii)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, kama Waziri alivyosema anawashukuru sana kwa michango yenu, nichukue fursa hii kuiagiza Serikali ifanyie kazi maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala na mapendekezo yaliyotolewa na Wabunge yatumike kuandaa Bajeti na Mpango wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Mpango huu utaletwa Juni, 2016 wakati wa kuwasilisha Mpango na Bajeti. Katibu!

UCHAGUZI WA WAJUMBE KWENYE TAASISI MBALIMBALI

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Msimamizi wa Uchaguzi ili tuweze kuendelea na zoezi letu, karibu.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Musukuma, samahani, naomba ukae. Katibu endelea.

DKT. THOMAS D. KASHILILLAH – KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako, naomba nitoe maelezo mafupi kabla ya kueleza utaratibu mzima wa zoezi la chaguzi mbalimbali ambazo ziko katika Bunge lako.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowatangazia tarehe 30 Januari, 2016 na kama ilivyo kwenye Orodha ya Shughuli za Bunge leo siku ya Ijumaa tarehe 5 Februari, 2016 kutakuwa na uchaguzi wa Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge (*The Parliamentary Service Commission*) na Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye taasisi mbalimbali za Kibunge duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi zilizopo na mgawanyo kwa kila moja ni kama ifuatavyo:-

(a) Tume ya Utumishi wa Bunge. Tume hii imeanzishwa na Sheria ya Uendeshaji wa Bunge, Sura ya 115 na chini ya sheria hii kuna aina mbili ya wajumbe. Wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao na wajumbe wanaochaguliwa na Wabunge kutoka mionganini mwao.

Kwa mujibu wa kifungu cha 12(2) cha Sheria ya Uendeshaji wa Bunge, wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao ni Spika ambaye ni Mwenyekiti wa Tume; Naibu Spika anakuwa Makamu Mwenyekiti wa Tume, Waziri anayeshughulikia masuala ya Bunge na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Hawa wanaingia kwa nafasi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi zilizo wazi kwa mujibu wa kifungu cha 12(3) cha Sheria hiyo ni wajumbe watano kutoka Chama Tawala ambapo angalau wawili wanatakiwa wawe wanawake na Wabunge wawili kutoka Vyama vya Upinzani ambapo angalau mmoja wao awe mwanamke.

Hadi kufikia muda wa mwisho wa kurudisha fomu yaani Alhamis, tarehe 4 Februari, 2016 saa 10.00 jioni, Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wamerejesha fomu ni kama ifuatavyo:-

Kundi A: Wabunge wa Chama Tawala. Waliochukua fomu na kurejesha ni watano. Ni Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola; Mheshimiwa Fakharia Shomar

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Khamis; Mheshimiwa Mary Pius Chatanda; Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu na Mheshimiwa Salim Hassan Turky. (Makofii)

Kundi B: Wabunge wa Kambi ya Upinzani. Walioresesha ni Mheshimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa. (Makofii)

Kwa mujibu wa taratibu za uendeshaji Bunge, hawa wamepita bila kupingwa. (Makofii/Vigelegele)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitarejesha kwako baada ya kukamilisha ili uwatangaze rasmi kuwa ni wajumbe.

(b) Bunge la Afrika (*Pan-African Parliament*). Kwa mujibu wa Kanuni ya 5 ya Nyongeza ya Tano ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016, nafasi zilizopo ni tano kwa mchanganuo ufuatao:-

Kundi A: Wabunge Wanawake nafasi moja; Wabunge kutoka Zanzibar nafasi moja; Wabunge kutoka Tanzania Bara nafasi mbili na Wabunge wa Vyama vya Upinzani nafasi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 5(a) inafafanua kwamba, tofauti na Kundi A ambalo ni maalum kwa Wabunge wanawake tu, makundi mengine yote yaani kundi la Wabunge kutoka Zanzibar; Tanzania Bara na Vyama vya Upinzani, Wabunge wa jinsia zote wanaweza pia kugombea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia muda wa mwisho wa kurudisha fomu yaani Alhamis, tarehe 4 Februari, 2016, saa 10.00 jioni, Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wameresesha fomu ni kama ifuatavyo:-

Kundi A: Wabunge wanawake nafasi moja, aliyechukua na kurejesha ni mmoja. Ameresesha Mheshimiwa Mboni Mohamed Mhita. (Makofii/Vigelegele)

Kundi B: Wabunge wa Zanzibar nafasi moja, aliyechukua fomu na kurejesha ni mmoja, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma. (Makofii/Vigelegele)

Kundi C: Wabunge wa Tanzania Bara, nafasi zilizopo ni mbili. Waliochukua fomu na kurejesha ni wawili, ni Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile na Mheshimiwa Stephen Julius Masele. (Makofii)

Kundi D: Wabunge wa Vyama vya Upinzani. Aliyechukua fomu na kurejesha ni mmoja, ni Mheshimiwa David Ernest Silinde. (Makofii)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 5 ya uendeshaji bora na Kanuni za Bunge wajumbe hawa wamepita bila kupingwa. (Makofi)

(c) Jukwaa la Wabunge wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Africa (SADC Parliamentary Forum).

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya SADC Parliamentary Forum, Ibara ya 7 inaelekeza kwamba, kila Bunge la nchi mwanachama litawakilishwa na Spika na Wabunge wengine watano. Aidha, Ibara ya 7(2)(b) inaelekeza kwamba Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake katika Bunge la Nchi husika anakuwa ni Mjumbe wa SADC Forum kwa nafasi yake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hivi karibuni Umoja wa Wabunge Wanawake umemchagua Mheshimiwa Margaret Sitta kuwa Mwenyekiti wake. Kwa hiyo, anaingia katika nafasi hii bila kupingwa. (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi zilizobaki na mgawanyo wake ni: Wabunge wa Zanzibar nafasi moja; Wabunge wa Tanzania Bara nafasi mbili na Wabunge wa Vyama vya Upinzani nafasi moja. Hadi kufikia muda wa mwisho wa kurudisha fomu siku ya Alhamis, tarehe 4 Februari, 2016, saa 10.00 jioni, Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wamerejesha fomu ni kama ifuatavyo:-

Kundi A: Wabunge wa Zanzibar, nafasi moja. Aliyechukua fomu na kurejesha ni Mheshimiwa Jamal Kassim Ali. (Makofi)

Kundi B: Wabunge wa Tanzania Bara, nafasi mbili. Waliochukua fomu na kurejesha ni wawili, Mheshimiwa Esther Michael Mmasi na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi. (Makofi)

Kundi C: Wabunge wa Vyama vya Upinzani, nafasi moja. Aliyechukua fomu na kurejesha ni mmoja, Mheshimiwa Ally Saleh Ally. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni na uendeshaji wa Bunge wajumbe hawa wamepita bila kupingwa. (Makofi)

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Utendaji ya Bunge ya Jumuiya ya Madola Kanda ya Tanzania (*Tanzania Branch*). Kwa mujibu wa Katiba ya Bunge la Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika, kila Bunge linatakiwa kuchagua wajumbe 12 wa Kamati ya Utendaji. Mchanganuo wa wajumbe hao ni kama ifuatavyo:-

Wabunge Wanawake nafasi tatu; Wabunge kutoka Tanzania Zanzibar nafasi mbili; Wabunge kutoka Tanzania Bara nafasi nne na Wabunge wa Vyama vya Upinzani nafasi tatu.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Hadi kufikia mwisho wa kurudisha fomu siku ya Alhamis, tarehe 4 Februari, 2016, saa 10.00 jioni, Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wamerejesha fomu pamoja na nafasi zilizopo ni kama ifuatavyo:-

Kundi A: Wabunge wanawake nafasi zilizopo ni tatu, waliochukua fomu na kurejesha ni watatu. Nitawataja, Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Maria Ndila Kangoye na Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu. (*Makofi*)

Kundi B: Wabunge wa Tanzania Zanzibar, waliochukua fomu na kurejesha ni wawili, nafasi zilizopo ni mbili. Nitawataja, Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali na Mheshimiwa Salum Rehani. (*Makofi*)

Kundi C: Wabunge wa Tanzania Bara, nafasi zilizopo ni nne. Waliochukua fomu na kurejesha ni wanne, Mheshimiwa Joseph Hasunga; Mheshimiwa Josephat Kandege; Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni na Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni. (*Makofi*)

Kundi D: Wabunge wa Vyama vya Upinzani, nafasi zilizopo ni tatu. Waliochukua fomu na kurejesha ni watatu, Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi; Mheshimiwa Juma Hamad Omar na Mheshimiwa Tundu Lissu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni, Wabunge hawa wamechaguliwa bila kupingwa. (*Makofi*)

(e) Umoja wa Wabunge Duniani (*Inter- Parliamentary Union*). Nafasi zilizopo ni tano kwa mchanganuo ufuatao:-

Wabunge wanawake nafasi moja; Wabunge kutoka Tanzania Zanzibar nafasi moja; Wabunge kutoka Tanzania Bara nafasi mbili na Wabunge wa Vyama vya Upinzani nafasi moja.

Hadi kufikia mwisho wa muda wa kurejesha fomu siku ya Alhamis, tarehe 4 Februari, 2016, saa 10.00 jioni, Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wamerejesha fomu na nafasi zao ni kama ifuatavyo:-

Kundi A: Wabunge wanawake nafasi moja. Aliyechukua na kurejesha ni Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe. (*Makofi*)

Kundi B: Wabunge wa Tanzania Zanzibar. Aliyechukukua fomu na kurejesha ni mmoja, nafasi iliyopo ni moja, Mheshimiwa Juma Othman Hijja. (*Makofi*)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kundi C: Wabunge wa Tanzania Bara. Nafasi zilizopo ni mbili, waliochukua fomu na kurejesha ni wawili, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa na Mheshimiwa Peter Serukamba. (Makofi)

Kundi D: Wabunge wa Vyama vya Upinzani. Nafasi iliyopo ni moja, Mbunge aliyechukukua fomu na kurejesha ni mmoja, Mheshimiwa Susan Anselim Lyimo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa nao wamepita bila kupingwa kwa mujibu wa Kanuni. Naomba nirejeshe kwako ili utangaze rasmi kuwa Wabunge wote waliochaguliwa katika makundi yote ni Wajumbe wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Tume na katika Vyama vya Kibunge Duniani. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Matiko, naomba ukae.

Matokeo ya uchaguzi, Tume ya Utumishi wa Bunge. Waliochaguliwa ni:

Kundi A: Wabunge wa Chama Tawala ni Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola; Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis; Mheshimiwa Mary Pius Chatanda; Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu na Mheshimiwa Salim Turky. (Makofi/Vigelegele)

Kundi B: Wabunge wa Vyama vya Upinzani. Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya na Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa. (Makofi/Vigelegele)

Hongereni sana Waheshimiwa Wabunge mlionchaguliwa kuwa kwenye Tume ya Utumishi ya Wabunge. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, matokeo ya uchaguzi Bunge la Afrika (Pan-African Parliament) waliochaguliwa ni:-

Kundi A: Wabunge wanawake ni Mheshimiwa Mboni Mohamed Mhita. (Makofi/Vigelegele)

Kundi B: Wabunge wa Zanzibar ni Mheshimiwa Asha Abdullah Juma. (Makofi/Vigelegele)

Kundi C: Wabunge wa Tanzania Bara, Mheshimiwa Dkt. Faustine E. Ndugulile na Mheshimiwa Stephen Julius Masele. (Makofi/Vigelegele)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kundi D: Wabunge wa Vyama vya Upinzani, Mheshimiwa David Ernest Silinde. (*Makofi/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge mtakaokwenda kutuwakilisha katika Bunge la Afrika, hongereni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, matokeo ya chaguzi Jukwaa la Wabunge wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC- Parliamentary Forum*). Waliochaguliwa ni:-

Kundi A: Wabunge wa Zanzibar ni Mheshimiwa Jamal Kassim Ali. (*Makofi/Vigelegele*)

Kundi B: Wabunge wa Tanzania Bara, Mheshimiwa Esther Michael Mmasi na Mheshimiwa Seleman Jumanne Zedi. (*Makofi/Vigelegele*)

Kundi C: Wabunge wa Vyama vya Upinzani ni Mheshimiwa Ally Salehe Ally. (*Makofi/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge ambao mtakwenda kutuwakilisha kwenye *SADC-Parliamentary Forum*, hongereni sana. (*Makofi*)

Nakumbushwa hapa kwamba na Mheshimiwa Magreth Simwanza Sitta kwa nafasi yake na yeye anakuwa ni mjambe kwa nafasi yake. Hongereni sana Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, matokeo ya uchaguzi Kamati ya Utendaji ya Bunge ya Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Parliamentary Association*) waliochaguliwa ni:-

Kundi A: Wabunge wanawake ni Mheshimiwa Amina S. Mollel; Mheshimiwa Maria Ndila Kangoye na Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu. (*Makofi/Vigelegele*)

Kundi B: Wabunge wa Zanzibar ni Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali na Mheshimiwa Salum M. Rehani. (*Makofi*)

Kundi C: Wabunge wa Tanzania Bara ni Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga; Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni; Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege na Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni. (*Makofi*)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kundi D: Wabunge wa Vyama vya Upinzani ni Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi; Mheshimiwa Juma Hamad Omar na Mheshimiwa Tundu Antiphas M. Lissu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge mtakaokwenda kutuwakilisha katika Bunge la Jumuiya ya Madola, hongereni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, matokeo ya uchaguzi Umoja wa Mabunge Duniani (*IPU*) waliochaguliwa:-

Kundi A: Wabunge wanawake ni Mheshimiwa Dkt. Pudenciana W. Kikwembe. (*Makofi*)

Kundi B: Wabunge wa Zanzibar ni Mheshimiwa Juma Othman Hija. (*Makofi*)

Kundi C: Wabunge wa Tanzania Bara ni Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa na Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba. (*Makofi*)

Kundi D: Wabunge wa Vyama vya Upinzani ni Mheshimiwa Susan A.J. Lyimo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge mtakaokwenda kutuwakilisha katika Umoja wa Mabunge Duniani, hongereni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo machache hapa, nimetaarifiwa kwamba wajumbe 12 wa Commonwealth Parliamentary Association wanapaswa kukutana na kuchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti. Nadhani mtayakumbuka majina ya wale walioshinda, wanapaswa kukutana ili wachague Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti ili waweze kuendelea na kazi.

Tangazo lingine, Wabunge wanawake wote wa CHADEMA wanapaswa kukutana katika chumba namba 229, jengo la utawala, leo saa saba mchana mara baada ya kuahirisha Bunge. Tangazo linatoka kwa Katibu Mkuu wa BAWACHA, Mheshimiwa Grace Tendega.

Tangazo lingine, kwa niaba ya Wabunge wa Singida na CCM Mkoa wa Singida, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, anawakaribisha Wabunge wote kwenye sherehe ya CCM kuadhimisha miaka 39 ya CCM itakayofanyika kesho tarehe 6 Februari, 2016 katika uwanja wa Namfua - Singida kuanzia saa sita. Tangazo limeletwa hapa na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba. (*Makofi*)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 28, nasitisha Bunge mpaka saa kumi jioni ambapo tutaendelea na shughuli zetu zilizobaki.

(Saa 6.17 Mchana Bunge *lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni*)

(Saa 10.00 Jioni Bunge *lilirudia*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu.

DKT. THOMAS D. KASHILILLAH – KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya Mkutano huu zimekamilika.

NAIBU SPIKA: Katibu.

DKT. THOMAS D. KASHILILLAH – KATIBU WA BUNGE: Hoja ya Kuahirisha Bunge.

HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

HOTUBA YA WAZIRI MKUU YA KUAHIRISHA MKUTANO WA PILI WA BUNGE KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kutujalia afya njema na uwezo katika yote tuliyoyatenda yaliyo mema katika kipindi chote tulichokaa hapa. Tumekuwepo hapa kwa takriban siku 11 katika shughuli za Mkutano wa Pili wa Bunge lako Tukufu. Ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehema kwa kutufikisha salama siku hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekutana hapa tukiwa tumeshuhudia uundwaji wa Serikali unaoendelea ambapo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya uteuzi wa Baraza jipya la Mawaziri ambao ni Waheshimiwa Wabunge wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nitumie nafasi hii ya awali kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Mawaziri wote, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wote Serikalini ambao wameteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika Serikali hii ya Awamu ya Tano. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano huu tulianza kufanya kazi ya chaguzi za Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge. Vile vile, tumefanya chaguzi za Wenyeviti wa Bunge na wajumbe wa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutuwakilisha katika taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa. Kwa vile orodha ni ndefu, napenda nitumie nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa na kwa ujumla wao wote waliogombea nafasi hizo na kushinda. Ni matarajio yangu kwamba tutatumia nafasi hizo vizuri katika kuleta ushirikiano, mshikamano na kufanya kazi pamoja kama wawakilishi wa wananchi na kutekeleza majukumu yetu kama Wabunge ndani ya Bunge hili. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maafa na ajali mbalimbali. Tarehe 27 Januari, 2016 wakati Bunge lako Tukufu likiendelea na vikao, Waheshimiwa Wabunge walipewa taarifa ya kusikitisha ya kuzama kwa Kivuko cha Kilombero ambapo katika tukio hilo watu walipoteza maisha na wengine kujeruhiwa. Aidha, mali za abiria zimepotea. Wakati huohuo, mvua zinazoendelea kunyesha nchini katika baadhi ya maeneo zimesababisha mafuriko, vifo, uharibifu wa mali ikiwemo mazao na miundombinu. Katika baadhi ya maeneo, mvua hizi zimesababisha njaa na athari nyingine kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maafa ya mvua na mafuriko, wapo wananchi waliofariki na wengine kupata ulemavu katika ajali mbalimbali za vyombo vya usafiri. Nitumie fursa hii kuwapa pole wote waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki katika matukio yote hayo. Aidha, napenda kuwatachia afya njema wote waliopata majeraha. Kwa wale wote waliopoteza maisha, tunawaombea kwa Mungu roho zao zilale mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo taarifa za uharibifu mkubwa wa miundombinu katika maeneo kadhaa nchini. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itafanya kila liwezekanalo kurekebisha miundombinu hiyo ya barabara iliyoharibika. Tunatambua gharama kubwa inayohitajika lakini ni wajibu wetu kama Serikali kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma muhimu hasa za mawasiliano katika eneo moja au jingine kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunahitimisha Mkutano wetu wa Pili wa Bunge tukiwa tumefanya shughuli mbalimbali ndani ya Bunge letu. Katika mkutano wetu, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kuuliza maswali ya kawaida na yale ya papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Jumla ya maswali 115 ya msingi na maswali 307 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano huu, moja ya ajenda iliyochukua nafasi kubwa ni hoja ya Serikali ya kujadili hotuba ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hoja hiyo tuliihitimisha vizuri na kwa mafanikio makubwa. Kazi kubwa iliyoko mbele yetu ni kutekeleza yale tuliyokusudia kama wajibu wetu sisi Wabunge wote.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza tena Waheshimiwa Wabunge wote kwa kushiriki vizuri katika mjadala wa hotuba ile. Nichukue tena nafasi hii kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba michango na maoni yote ya Waheshimiwa Wabunge yatazingatiwa katika utekelezaji wa hotuba ile. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano huu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kujadili na kuidhinisha Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha wa 2016/2017. Vilevile, Bunge limejadili na kutoa maoni na ushauri katika mwongozo wa kuandaa mpango na bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa, naomba nimshukuru Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara za kisekta kwa ufanuzi mzuri walioutoa wakati wa kuhitimisha hoja hii. Aidha, napenda kutumia fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mizuri, maoni na ushauri wao ambao Serikali itauzingatia katika kukamilisha maandalizi ya mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami pia uniruhusu nitoe maelezo mafupi ya msisitizo katika maeneo machache yaliyopata michango mingi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja ya Serikali ya Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Waheshimiwa Wabunge wengi wamesisitiza sana kuhusu umuhimu wa Serikali kuongeza uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kuimarisha udhibiti wa matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Waheshimiwa Wabunge wameishauri pia Serikali kuweka kipaumbele cha ujenzi wa reli mpya ya kati; kujenga uchumi wa viwanda; kuanza na kusimamia ujenzi na mitambo ya kuchakata gesi asilia (LNG) na Kiwanda cha Mbolea Mkoani Lindi; kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme vijiivji; ujenzi wa bandari ya Bagamoyo na Mtwara; kutatua changamoto zinazowakabili wakulima na wafugaji pamoja na wachimbaji wadogo wa madini. Vile vile, kuweka mikakati thabit ya utekelezaji wa miradi ya sekta za elimu, afya, maji na huduma kwa wenyewe ulemavu na pia kuzingatia utawala bora. Serikali inatambua kuwa maeneo haya ni muhimu sana katika kujenga uchumi imara na endelevu na pia kuondoa umaskini. Hivyo, itazingatia sana ushauri huu mzuri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wote. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa Tanzania kwa umahiri wake mkubwa na umakini alionunesha ikiwa ni mwanzo mzuri wa kuongoza Serikali ya Awamu ya Tano. Mheshimiwa Rais ameonesha kasi kubwa na dhamira ya dhati ya kuwatumikia Watanzania katika kujenga uchumi imara, unaokua na endelevu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi watakulaliana nami kwamba Serikali ya Awamu ya Tano katika kipindi chake cha mwanzo wa siku 100, imeonesha dhahiri nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba makusanyo na mapato yetu yanaongezeka. Jitihada hizo za kuongeza makusanyo ya mapato ya Serikali zimefafanuliwa vizuri zaidi kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango. Serikali itaendelea na mikakati yake ya kuongeza mapato yake na kudhibiti mianya ya ukwepaji kodi. Ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge, wafanyabiashara na wananchi wote wataunga mkono dhamira hiyo njema ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi, tayari Serikali imeanza kuchukua hatua thabiti ya kudhibiti matumizi yasiyo na tija katika Wizara, Idara za Serikali Zinazojitegemea na Taasisi zote za Umma, Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kwamba Serikali inasimamia kwa umakini matumizi ya fedha za umma ili zitumike ipasavyo kwa malengo yaliyokusudiwa. Hatua hizi zitaimarishwa zaidi katika mwaka ujao wa fedha. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali, hoja nyingi za msingi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu Mpango wa Taifa, zimefafanuliwa vizuri na Waheshimiwa Mawaziri wa kisekta na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Naomba niwaahidi kuwa tutayazingatia sana katika mchakato wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/2017, kwa kadri itakavyowezekana. Waheshimiwa Wabunge watashirikisha kikamilifu katika mchakato huo kupitia Kamati mbalimbali za Bunge. Serikali itafarijika sana kupata maoni na ushauri zaidi ili tuweze kuboresha mipango yetu ya muda mfupi na muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya chakula kwa mwaka 2015/2016, katika maeneo mengi ya nchi imeendelea kuwa ya kuridhisha kufuatia mavuno mazuri yaliyopatikana msimu wa kilimo wa 2014/2015. Takwimu za Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi zinaonesha kuwa kwa msimu uliopita nchi ilikuwa na ziada ya chakula licha ya kuwepo kwa maeneo machache ambayo hayakuwa na chakula. Kutokana na uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa 2014/2015, kuwa tani milioni 15.5 na mahitaji ya chakula kwa mwaka 2015/2016 kuwa tani milioni 12.9 hivyo nchi imejitosheleza kwa chakula kwa ziada ya tani milioni 2.5 sawa na asilimia 120. Napenda kuwahakikisha Watanzania kuwa Serikali itaendelea kuhudumia maeneo yote yenye uhaba wa chakula.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Taifa kuwa na ziada ya asilimia 120 ya chakula, tathmini ya hali ya chakula nchini inaonesha kuwa kuna halmashauri 69 katika mikoa 18 nchini yenye maeneo yenye dalili za upungufu wa chakula. Maeneo hayo yapo katika Mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Lindi, Singida, Tabora, Arusha, Geita, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Tanga, Simiyu, Mwanza, Morogoro, Iringa, Njombe, Mtwara na Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na hali ya uhaba wa chakula katika maeneo hayo, Serikali inaendelea kutoa chakula katika maeneo hayo ambapo jumla ya tani 23,871.6 za chakula zilitengwa kwa ajili hiyo. Hadi kufikia tarehe 17 Januari, 2016, jumla ya tani 11,860.8 zilikuwa zimechukuliwa toka Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kwenda kwenye Halmashauri za Wilaya zenye upungufu wa chakula kwa ajili ya usambazaji. Natoa wito kwa halmashauri ambazo hazijachukua mgao wao kufanya hivyo mara moja ili wananchi katika maeneo hayo wasizidi kuathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na utoaji wa chakula cha msaada, Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, inaendelea kutoa mahindi katika maghala ya Songea na Sumbawanga kwa ajili ya kuuzwa kwa wafanyabishara wa nafaka walioidhinishwa na mikoa yenye uhaba wa chakula. Lengo ni kuongeza upatikanaji wa chakula na kukabiliana na kasi ya kupanda kwa bei ya vyakula katika maeneo hayo. Chini ya utaratibu huo, vibali vimeshatolewa kwa wafanyabiashara wa mikoa 17, vya kununua jumla ya tani 77,166. Hadi kufikia tarehe 18 Januari, 2016 jumla ya tani 56,817.5 kati ya tani 64,817.3 zilizokuwa zimelipiwa kutoka NFRA tayari zilikuwa zimechukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza na kuimarisha uhakika na usalama wa chakula hapa nchini, Serikali imelenga kujenga maghala 275 kwa awamu katika sehemu zenye uzalishaji mkubwa wa zao la mahindi ambapo hadi sasa jumla ya maghala 125 yanaendelea kujengwa na kukarabatiwa katika maeneo hayo. Aidha, Serikali kwa kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula inaendelea kujenga maghala ya kimkakati kwa ajili ya kuhifadhi akiba ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa ghala moja lenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 limeshajengwa Wilayani Mbozi, Mkoani Mbeya. Aidha, Serikali imepata mkopo wenye masharti nafuu kutoka Serikali ya Poland ambao utawezesha kujenga vihenge vya kisasa (*silos*) vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 160,000 na maghala yenye uwezo wa kuhifadhi tani 90,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali, nawataka Viongozi wa Mikoa, Wilaya na Watendaji katika Halmashauri zote nchini kuwahamasisha wananchi kutumia vizuri mvua zinazonyesha nchini kote kulima kwa bidii ili kuweza kuvuna na kuijiwekea akiba ya chakula cha kutosha kwa ajili ya kaya zao wakati wote wa mwaka. Aidha, niwahamasishe

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wafanyabiashara na wadau wengine kusaidia Serikali kuchukua chakula kutoka maeneo yenyе ziada na kupeleka katika maeneo yenyе upungufu. Ni imani yangu kwamba tukizingatia maelekezo haya pamoja na juhudи za Serikali zilizooneshwa, tatizo la uhaba wa chakula nchini litapungua kama siyo kumalizika kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kushughulikia migogoro ya wakulima na wafugaji. Migogoro ya ardhi hapa nchini ina sura nne: Migogoro kati ya wakulima na wafugaji; mgogoro kati ya wananchi na wawekezaji; migogoro kati ya wananchi na Serikali na migogoro kati ya mamlaka moja na mamlaka nyingine ndani ya Serikali. Migogoro hii imeenea nchi nzima kutokana na sababu mbalimbali ikiwepo kuongezeka kwa utambuzi wa thamani ya ardhi na matumizi ya rasilimali ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi kwa kutumia Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Na. 5 ya mwaka 1999 na Sheria ya Matumizi ya Ardhi, Na. 6 ya mwaka 2007, hadi kufikia mwezi Juni, 2015 jumla ya vijiji 620 katika wilaya 81 kwenye mikoa 22 zimeweza kutenga hekta milioni 1.9 kwa ajili ya wafugaji. Wito wangu kwa wananchi na wadau wa kilimo na ufugaji, nawaomba kutunza na kuendeleza maeneo haya ili yaweze kutumika kwa mujibu wa malengo yaliyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu hatua ambazo Serikali imechukua kukabiliana na migogoro ya wakulima na wafugaji iliyotokea katika Mikoa ya Morogoro (Wilaya za Mvomero na Kilombero) na Manyara (Wilaya ya Kiteto). Katika kushughulikia tatizo hili, jumla ya vijiji 53 vimeainisha maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo kilimo na ufugaji. Aidha, jumla ya mashamba pori nane yameainishwa na orodha yake imewasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua za kufutiwa hati miliki na hatimaye kufanya utaratibu wa kuyatumia kwa ufugaji. Ni matarajio yangu kuwa maeneo haya yatapunguza kwa kiasi kikubwa matatizo ya uhaba wa malisho hapa nchini. Wito wangu, niwatake Viongozi wa Vijiji kusimamia vizuri matumizi ya maeneo haya yatakayotolewa kwa ajili ya malisho ili tatizo hili la kukosa maeneo ya malisho lisijirudie tena. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna mgogoro wa wafugaji na wakulima katika Bonde Oevu la Kilombero ambao umetafutiwa ufumbuzi kwa kuweka alama (branding) mifugo yote katika eneo hili ambapo jumla ya mifugo 52,780 ilipata usajili wa wilaya. Aidha, jumla ya mifugo 24,586 imeondolewa katika eneo la Bonde la Kilombero. Kwa kuzingatia hatua zilizochukuliwa na Serikali, wananchi wanapaswa kufuata sheria na kuhakikisha mifugo hairudi tena katika

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maeneo yaliyokatazwa na kwamba maeneo haya yanahifadhiwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa wafugaji na wakulima katika maeneo ya Kiteto ni wa muda mrefu na kwa bahati mbaya sana umeleta madhara makubwa kwa maisha ya wanadamu na uharibifu wa mali. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Tume iliyoundwa na aliyekuwa Waziri Mkuu (mstaafu) Mheshimiwa Mizengo Peter Kayanza Pinda, ikiongozwa na Baba Askofu Amos Muhamadi, imekamilisha hatua muhimu ya kuleta maelewano na maridhiano katika pande zilizoathirika na mgogoro huo. Kwa sasa hali imeendelea kuimarika na tunaendelea kufuatilia kuhakikisha inakuwa shwari kwa muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tarehe 29 Januari 2016, nimekutana na viongozi wa Serikali, Halmashauri ya Wilaya na chama kutoka Wilaya ya Kiteto hapa Dodoma ambapo nilipata fursa ya kupokea taarifa ya Tume niliyoitaja hivi punde. Nimeagiza Tume kuendelea na hatua iliyobakia ili kurejesha utulivu na amani kwa wananchi wa Kiteto. Hata hivyo, nimepanga kufanya ziara Wilayani Kiteto katika siku chache zijazo ili niweze kukutana na wananchi walioathirika na mgogoro huu na ikiwa ni pamoja na kujionea hali halisi wilayani humo ili tuweze kutatua migogoro yote. Wito wangu kwa Ndugu zangu wa Kiteto ni kuwaomba waendelee kuvumilia wakati jitihada za Serikali katika kutatua migogoro hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa elimu msingi bila malipo. Tangu Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli atoe maelezo ya utekelezaji wa elimu msingi bila malipo, kumekuwa na umuhimu wa kutoa elimu na ufanuzi zaidi juu ya utekelezaji wa agizo la elimu bila malipo kwa Watanzania kuanzia darasa la awali hadi kidato cha nne katika shule za umma. Hii ni hatua ya Serikali katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na fursa ya elimu bora kwa wote pia kuwapunguzia mzigo wazazi na walezi kugharamia au kuchangia upatikanaji wa elimu msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango huu, Serikali imedhamiria kuhakikisha kuwa mwanafunzi atasoma kuanzia darasa la awali hadi kidato cha nne bila ya wazazi na walezi kulipa ada ya shule, gharama za mitihani na michango mbalimbali. Hata hivyo, yapo majukumu ambayo yataendelea kutekelezwa na wazazi na walezi wote ambayo ni pamoja na kununua sare za shule na michezo, madaftari, kalamu na chakula kwa wanafunzi wa shule za kutwa waliojiwekea utaratibu huo. Maeneo mengine ni kulipia nauli ya kwenda na kurudi shule na mahitaji mengine kama kununua godoro, shuka na vifaa vya usafi binafsi. Mzazi au mlezi anao wajibu wa kugharamia matibabu ya mtoto wake.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote tushirikiane katika juhudzi za kuunga mkono uamuzi huu wa Serikali kuhusu elimu bila malipo. Aidha, nawaomba wote kwa ujumla wetu kushirikiana kuwaelimisha wananchi wetu kuhusu utaratibu huu na wajibu wa kila mmoja wetu kama mzazi au mlezi kuhusu utekelezaji wa zoezi hili. Nia yetu ni kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata fursa ya kupata elimu bora kwa mtoto mwenye umri wa kwenda shule na wote walioko katika shule za msingi na sekondari. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kama tulivyokwishesema, suala la ada elekezi linafanyiwa kazi na likikamilika, wananchi watajulishwa kuhusu utaratibu huo. Vikao vya pamoja, Serikali na wadau vitaanza hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mpango huu, Serikali imetenga shilingi bilioni 131.4 kuanzia Disemba, 2015 hadi Juni, 2016, kuhudumia wanafunzi wa bweni kwa chakula, kufidia gharama za ada za mitihani, ada ya shule na kutoa fedha za uendeshaji wa shule (*capitation grants*). Aidha, kupitia Waraka wa Elimu, Na. 5 wa mwaka 2015, Serikali imefuta michango yote iliyokuwa inachangishwa shuleni kwa idhini ya Kamati na Bodi za shule. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua toka tuanze utekelezaji wa zoezi hili zipo changamoto zilizojitokeza. Kwa mfano, baadhi ya shule zenye wanafunzi wachache kupata fedha kidogo sana kwa kuwa ugawaji wa fedha unazingatia idadi ya wanafunzi. Pia zipo changamoto katika kutoa chakula cha mchana kwa wanafunzi wa kutwa na uendeshaji wa hosteli ambazo wazazi na walezi au jamii walikuwa wanachangia fedha za chakula. Serikali inaendelea kuzifanya kazi changamoto hizo zilizojitokeza katika kutekeleza mpango huu ikiwemo uelewa wa jamii na wadau kuhusu mpango mzima kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Serikali imeendelea kutoa huduma ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2015/2016 kwa kuzingatia Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Na. 9 ya mwaka 2004 (Kama iliyvorekebishwa), Kanuni za Utoaji Mikopo za mwaka 2008 na Mwongozo wa Utoaji Mikopo na Ruzuku kwa mwaka wa masomo 2015/2016. Hadi kufikia mwishoni mwa Januari 2016, Serikali ilikuwa imetoa mikopo yenyeye thamani ya shilingi bilioni 207.9 kwa wanafunzi 122,786 wa elimu ya juu, wakiwemo wanafunzi wa mwaka wa kwanza 53,850 ambaao ni asilimia 98.9 ya wanafunzi 55,254 walioomba mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Taifa liendelee kuwa na wataalamu wa kutosha katika nyanja muhimu, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele kwa kutoa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wanaodahiliwa katika programu za kipaumbele ikiwemo sayansi za tiba, ualimu wa sayansi na hisabati, uhandisi wa mafuta ya gesi, uhandisi umwagiliaji, sayansi za kilimo, wanyama na ardhi. Aidha, Serikali inaendelea kufanya kazi mikakati ya kuimarisha urejeshaji wa mikopo pamoja na kuwa na vyanzo endelevu vya kupata fedha za kudumu ili kukidhi ongezeko la wanafunzi wenyewe mahitaji ya mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama nchini kwa ujumla ni shwari. Hata hivyo, katika kipindi hiki, nchi yetu imekuwa ikikabiliana na changamoto ya ongezeko kubwa la wakimbizi hususan katika Mkoa wa Kigoma. Kambi zetu zilizoko Mikoa ya Kigoma, Katavi, Tabora na Tanga zinahifadhi wakimbizi wapatao 218,895 kutoka Mataifa ya Burundi (156,377), Congo-DRC (62,176), Somalia (150) na mataifa mchanganyiko (192) kutoka nchi za Rwanda, Uganda, Sudani ya Kusini na Ethiopia. Kwa ujumla katika kipindi hiki, wamepokelewa wakimbizi zaidi ya 122,267 kutoka Burundi pekee. Aidha, hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2015, kambi mpya ya wakimbizi ya Nduta imepokea wakimbizi 38,994. Wengi kati yao wamehamishiwa kutoka Kambi ya Nyarugusu na wachache wakiwa wameingia moja kwa moja kutokea Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia ujio wa wimbi kubwa la wakimbizi kutoka Burundi, kumejitokeza matukio ya uhalifu wa kutumia silaha za moto ndani na nje ya kambi ya wakimbizi ya Nyarugusu. Aidha, kutokana na upekuzi na ukaguzi kwa wakimbizi unaofanywa kwa pamoja na vyombo vya dola sanjari na taarifa za kiintelijensia, imebainika kuwepo kwa askari waasi waliokimbia pamoja na raia wa kawaida ambao wanajaribu kuwashawishi vijana kujisajili ili kuijunga na vikundi vya waasi. Nitoe wito kwa wananchi na wakimbizi kushirikiana na vyombo vyetu vya usalama kwa kutoa taarifa za uhalifu hususan umiliki haramu wa silaha za moto kwenye makambi na katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango endelevu wa usafi wa mazingira nchini. Mtakumbuka kuwa Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, aliamua maadhimisho ya miaka 54 ya Uhuru ya terehe 9 Desemba, 2015 yafanyike kwa kufanya usafi wa mazingira katika maeneo ya umma na maeneo yanayowazunguka. Kwa ujumla, wananchi, taasisi za umma na binafsi ziliitikia agizo hilo na kushiriki kikamilifu katika zoezi hilo. Nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati wananchi, taasisi za umma na binafsi kwa kushiriki katika zoezi hilo kikamilifu. Mlionesha moyo wa uzalendo na ari kwa nchi yetu, nawapongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, usafi ni dhana muhimu katika kulinda afya za binadamu na kudhibiti magonjwa mbalimbali ya mlipuko ikiwemo kipindupindu. Ili kufanikisha lengo hili, kunahitajika juhudzi za makusudi na za pamoja katika

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

usimamizi wa sheria, kanuni na taratibu tulizojiwekeea. Hivyo, Serikali imeamua kufanya zoezi la usafi wa mazingira kuwa endelevu kuititia Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Serikali imetoa Waraka unaoelekeza kuwa kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi iwe siku maalum ya kufanya usafi wa mazingira. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuendelea kusisitiza katika kila ngazi yaani viongozi na wananchi kutimiza wajibu wako kwa kuhakikisha zoezi hili linakuwa endelevu. Aidha, napenda kuwahimiza Viongozi wa Mkoa, Wilaya na Halmashauri kusimamia usafi wa mazingira katika maeneo yote ya utawala. Zoezi hili ambalo litakuwa linafanyika kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi, kila Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya nchini awe na mikakati ya kudumu ya usafi ikiwa ni pamoja kuhakikisha kuwa kuna Sheria Ndogo za Usafi wa Mazingira na zitatekelezwa ipasavyo.

Aidha, Halmashauri zote nchini zihakikishe kuwa uchafu uliokusanywa katika maeneo mbalimbali unazolewa na kupelekwa katika maeneo mahsus ya dampo. Simamieni kikamilifu wakandarasi waliopewa zabuni hizo na kuona wanatimiza wajibu wao kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoona usafi wa mazingira ni jukumu la kila mwananchi na linapaswa kuwa endelevu. Rai yangu kwa Watanzania wote ni kujenga tabia ya kuhakikisha kuwa mahali pa kazi na mazingira yanayokuzunguka yanakuwa safi wakati wote. Kufanya hivyo, kutasaidia sana kuimarisha usafi wa mazingira na kuboresha afya. Hali kadhalika kupunguza milipuko wa magonjwa mbalimbali ikiwemo kipindupindu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu kwa wananchi ni kuona kuwa zoezi la usafi ni la kila mmoja na kuepuka kuchafua mazingira kwa makusudi ikiwemo kuepuka tabia ya kutupa taka hovyo wanapokuwa katika vyombo vyaa usafiri na pia kutofanya biashara katika maeneo yasiyoruhusiwa ili kuzuia kutupwa taka hovyo. Serikali inawaagiza wamiliki wa mabasi ya safari ndefu kuhakikisha kuwa kwenye mabasi yao kunakuwa na vikapu vyaa kutunzia taka kwa abiria walioko ndani ya basi hilo. Agizo hili lisimamiwe na yejote atakayekuwa anatupa takataka kuititia dirishani, hatua kali zichukuliwe dhidi yake na basi hilo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji wote wa Serikali wakiwemo wa mitaa, kata na vijiji watimize wajibu wao na kuhakikisha kuwa maeneo wanayoyasimamia yanakuwa katika hali ya usafi. Nitumie fursa hii kuwahimiza wananchi, taasisi na jumuiya zote kuhakikisha kwamba wanaweka mazingira katika hali ya usafi na pia kushiriki katika siku ya usafi kama iliyopangwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhusiano wa Kimataifa. Nchi yetu imeendelea kuwa kivutio kikubwa katika mahusiano baina ya nchi na nchi, Jumuiya za

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kikanda na Kimataifa. Hii inatokana na viongozi wetu ambao wamekuwa katika mstari wa mbele kudumisha mahusiano yetu katika medani za Kimataifa. Yapo mambo mengi yaliyofanyika na yanayoendelea kufanyika kama mwendelezo wa kudumisha ushirikiano katika Jumuiya hizi za Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na juhudini za viongozi wetu kutangaza nchi yetu Kimataifa, ni hivi karibuni tu Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliteuliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Bwana Ban Ki-moon kuwa mmoja wa Wenyeviti wa Jopo la Ushauri la Ngazi ya Juu kuhusu Afya ya Mama na Mtoto Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni heshima kubwa kwa nchi yetu kwa kuwa itaiweka Tanzania kuwa mionganini mwa mataifa yenye kuheshimika duniani. Aidha, uteuzi huu ni chachu ambayo inaleta matumaini mapya katika kukabiliana na changamoto za afya ya mama na mtoto hususan katika nchi zinazoendelea kama Tanzania. Nitumie fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa uteuzi huo. Tunamuombea kheri na baraka tele katika kutekeleza jukumu hilo kubwa la Kimataifa kwa maendeleo ya watu wetu. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha utendaji Serikalini na maadili. Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi imedhamiria kurejesha nidhamu na maadili ya watendaji wa Serikali na watumishi wa umma katika kutoa huduma kwa wananchi wa maeneo mbalimbali. Katika kuhakikisha watumishi wa umma na Watanzania wote wanafanya kazi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuja na kauli mbiu ya "Hapa Kazi Tu". Tafsiri ya falsafa hii ni kuwataka Watanzania wote katika nafasi mbalimbali walizopo kufanya kazi kwa bidii na kujiepusha na vitendo vya uzembe, urasimu na kutenda kazi kwa mazoea. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 chini ya Ibara ya 22 inaaishisha kuwa, kila mtu anayo haki ya kufanya kazi. Vilevile, Ibara ya 25 inafafanua kuwa kufanya kazi ndiyo njia pekee ya kumwezesha Mtanzania kupata utajiri na ndiyo chimbuko la ustawi wa wananchi na ndiyo kipimo cha utu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati akihutubia Mkutano wa Kwanza wa Bunge letu Tukufu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa maneno yake alisema, napenda kunukuu:-

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

"Serikali nitakayoiunda nataka iwe inawahudumia wananchi kwa haraka na siyo kwa kuwasumbuasumbua na kuwazungushazungusha. Natoa rai kwa watumishi wa Serikali hasa ambao ni wazembe na wavivu, kujandaa. Wamevumiliwa kwa muda mrefu sasa basi. Kwa sababu watumishi wa aina hiyo hawatavumiliwa katika Serikali nitakayoiongoza. Lughu za "Hiyo ni changamoto, tutaishughulikia" au "Mchakato unaendelea" hazitavumiliwa katika Serikali ya Awamu ya Tano. Mimi nataka watu wa kazi tu. Hatuwezi kulea watu ambao wanalipwa mishahara lakini hawafanyi kazi wanazotakiwa kufanya au wamegeuza ofisi za umma kuwa ni mahali pa kuchuma bila kufanya kazi." Mwisho wa kunukuu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza maneno ya Mheshimiwa Rais na kutimiza matakwa ya Kikatiba, kila Mtanzania anapaswa kushiriki na kujituma kwa uaminifu katika kazi halali za uzalishaji mali. Aidha, kila mwananchi anapaswa kuwa na nidhamu ya kazi na kuhakikisha anafikia malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kuwakumbusha watumishi wa umma kuwa wamepeva dhamana ya kuwahudumia wananchi kwa niaba ya Serikali. Hivyo, wanawajibika kuhakikisha wanawahudumia wananchi kwa haki, weledi, uadilifu na kwa taaluma zao. Ni lazima wahakikishe kuwa wanatatua kero za wananchi. Siyo sahihi wananchi kuwasilisha kero zao kwa Viongozi wa ngazi za Kitaifa hasa wakati wa ziara ilhali Viongozi wa Mikoa na Wilaya wapo katika maeneo hayo kwa wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kuwa wapo watumishi wanaotekeleza vyema majukumu yao lakini pia wapo watumishi ambao hawazingatii maadili ya kazi zao na pia wanafanya kazi kwa uzembe. Serikali haitaacha kuchukua hatua za nidhamu kwa watumishi wote wasiozingatia kikamilifu sheria, kanuni na taratibu katika utumishi wa umma. Aidha, kwa kuzingatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais, viongozi na watumishi wote wa umma lazima tufanye kazi kwa kuzingatia weledi na kujiamini. Kila mtu anapaswa kujitathmini kama dhamana aliyopewa anaitendea haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu sasa ni wakati wa kufanya mabadiliko ya dharti katika utendaji na uadilifu. Kwa maana hiyo napenda kusisitiza mambo yafuatayo:-

(i) Kila kiongozi na mamlaka ya nidhamu ni lazima kuwajibika kusimamia utendaji na maadili ya kazi. Hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa wakati na kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi. Tusione haya hata mara moja, tuchukue hatua. (Makofii)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(ii) Wananchi wahudumiwe ipasavyo na kwa weledi, haki, uadilifu na heshima. Mambo haya yakizingatiwa hakuna mwananchi atakayesafiri kutoka kijiji, wilayani au mkoani kutafuta huduma Makao Makuu ya Wizara, Ofisi ya Waziri Mkuu au Ikulu.

(iii) Madawati ya malalamiko yawepo katika ofisi za umma. Aidha, tayari maelekezo yametolewa ya watumishi wa umma kuzingatia utaratibu wa kuva vitambulisho vyenye majina yao ili waweze kutambulika kwa urahisi kwa wananchi wanapotoa huduma zao. Agizo hili litekelezwe kama ambavyo limetamkwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais ametumia dhana ya "kutumbua jipu" kama dawa ya kusimamia uwajibikaji hasa kwa wale wenye dalili ya kukosa maadili ya utumishi wa umma. Tafsiri ya dhana hii ya "kutumbua jipu" inalenga katika kuwarejesha watumishi wa umma na walioko Serikalini katika mstari wa utendaji. Nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote kama tulivyokuwa na kwa umoja wetu tuumunge mkono Mheshimiwa Rais katika vita hii kubwa yenye jina la "utumbuaji majipu". Tukiwa pamoja kwa kushirikiana tutaweza kuibadilisha nchi yetu kuwa nchi ya maadili na yenye sifa ya juu katika utendaji wa utumishi wa umma. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba nisisitize kuwa Serikali ya Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli inaongozwa na Katiba, Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi. Vile vile inaheshimu na kuthamini haki za watumishi wa umma wa ngazi zote na inatambua mchango mkubwa unaotolewa na watumishi wa umma katika kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Kamwe, Serikali haitamuonea mtumishi ye yote wala kumnyanyasa endapo tu atakuwa anatenda yale yanayopaswa. Pia haitamvumilia mtumishi mzembe na asiyetimiza wajibu wake. Serikali itaendelea kuchukua hatua za kurejesha nidhamu kwa watumishi wa umma ili kuwezesha nchi yetu kuwa na utumishi wenye kuzingatia uadilifu uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Uzoefu nilioupata katika muda mfupi tuliokaa pamoja hapa Bungeni, nimegundua kuwa tuna Waheshimiwa Wabunge mahiri waliobobea katika nyanja mbalimbali. Wapo wasomi wa ngazi zote, wazee kwa vijana ambao wana uzoefu na utaalam mkubwa. Ni imani yangu kuwa tutatumia utaalam na uwezo mkubwa tulionao katika kujenga nchi yetu na kuwasaidia Watanzania kutoka hapa tulipo hadi hatua ya mbele katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi walio tuchagua wanatutegemea. Nawaomba tutangulize uzalendo katika kila jambo tunalofanya kwa manufaa ya Taifa letu na watu wake. Tufike mahali ambapo kwa elimu tulionayo, busara

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tulizonazo na hekima tulizonazo kuacha kabisa ushabiki wa kisiasa badala yake tutazame mbele katika kuwaletea wananchi maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kurejea tena nilivyosema hapo awali kwamba, baada ya kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu kwa mafanikio makubwa, kazi kubwa iliyo mbele yetu ni kuijenga nchi yetu kwa umoja na mshikamano. Nawaomba sana tuweke maslahi ya Watanzania na Taifa letu mbele. Tudumishe amani na utulivu. Tupuuze sera zozote za kudhoofisha utaifa wetu kama Watanzania na kutugawa kwa misingi yoyote ile, iwe ya kidini, ya kikabila, ya kisiasa, rangi au kwa itikadi ya namna yoyote ile. Dhamira yetu sote iwe ni kukuza uchumi wa nchi yetu na kuondoa umaskini ili kuwaletea wananchi wetu maendeleo na maisha mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jukumu la kila mmoja wetu kuhakikisha kuwa Tanzania inapiga hatua mbele. Tufanye kazi kwa bidii kuunga mkono kaulimbiu yetu ya "Hapa Kazi Tu". Aidha, tutumie juhudhi, maarifa na ubunifu zaidi katika kila jambo. Naamini kuwa kwa ushirikiano katika Bunge hili na wananchi kwa ujumla, tutaweza kutimiza matarajio ya wananchi waliotuchagua na matarajio ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii tena, kuwashukuru wote waliosaidia kufanikisha Mkutano huu. Nikushukuru wewe Naibu Spika, nimshukuru pia Mheshimiwa Spika kwa kutuongoza vizuri kwa weledi mkubwa. Kipekee nimshukuru Katibu wa Bunge na timu yake lakini pia niwashukuru Wenyeviti wa Bunge ambao wamekalia Kiti kwa mara ya kwanza lakini kwa weledi mkubwa, hongereni sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia niwashukuru wataalam wote wakiwemo Waandishi wa Habari kwa kazi nzuri waliyofanya kufanikisha Mkutano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuwatachia wote safari njema mnaporejea kwenye maeneo yenu ya kazi na katika Majimbo yenu. Naamini kwamba Mwenyezi Mungu atatulinda na kutuweka salama sote kama tulivyo hadi tukutane tena Mkutano ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 19 Aprili, 2016, saa tatu asubuhi, litakapokutana katika Mkutano wa Tatu kwenye ukumbi huu hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

HOTUBA WAZIRI MKUU WAKATI WA KUHITIMISHA MKUTANO WA PILI WA BUNGE KAMA ILIVYOWASILISHWA BUNGENI

I: UTANGULIZI

(a) Masuala ya Jumla

Mheshimiwa Spika,

1. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kutujalia afya njema na uwezo katika kutenda yote yaliyo mema. Tumekuwepo hapa kwa takriban siku 11 katika shughuli za Mkutano wa Pili wa Bunge lako Tukufu. Ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa Rehema kwa kutufikisha salama siku ya leo.

2. Tumekutana hapa tukiwa tumeshuhudia uundwaji wa Serikali unaoendelea ambapo Mheshimiwa Dkt John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya uteuzi wa Baraza jipya la Mawaziri ambao ni Waheshimiwa Wabunge wenzetu. Niruhusu nitumie nafasi hii ya awali kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote ambao wameteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika Serikali ya Awamu ya Tano.

(b) Chaguzi Mbalimbali

Mheshimiwa Spika,

3. Katika Mkutano huu, tumeweza kufanya Chaguzi za Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge. Vilevile, tumefanya chaguzi za Wenyeviti wa Bunge letu na Wajumbe wa kutuwakilisha katika Taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa. Kwa vile orodha ni ndefu, napenda nitumie nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa na kwa ujumla wao wote waliogombea nafasi hizo na kushinda. Ni matarajio yangu kwamba tutatumia nafasi hizo vizuri katika kuleta ushirikiano, mshikamano na kufanya kazi pamoja kama Wawakilishi wa Wananchi na kutekeleza majukumu yetu kama Wabunge ndani ya Bunge hili.

(c) Maafa na Ajali

Mheshimiwa Spika,

4. Tarehe 27 Januari, 2016 wakati Bunge lako Tukufu likiendelea na Vikao, Waheshimiwa Wabunge walipewa taarifa ya kusikitisha ya kuzama kwa Kivuko cha Kilombero, ambapo katika tukio hilo watu walipoteza maisha na wengine kujeruhija. Aidha, mali za abiria zimepotea. Wakati huo huo, mvua zinazoendelea kunyesha nchini katika baadhi ya maeneo zimesababisha

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mafuriko, vifo, uharibifu wa mali ikiwemo mazao na miundombinu. Katika baadhi ya maeneo, mvua hizi zimesababisha njaa na athari nyingine kwa jamii.

5. Pamoja na maafa ya mvua na mafuriko, wapo wananchi waliofariki na wengine kupata ulemavu katika ajali mbalimbali za vyombo vyatya usafiri. Nitumie fursa hii kuwapa pole wote waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki katika matukio yote hayo. Aidha, napenda kuwatakia afya njema wote waliopata majeraha. Kwa wale wote waliopoteza maisha tunawaombea Roho zao zilale mahali pema peponi - Amina.

6. Kuhusu uharibifu wa miundombinu, tunazo taarifa za uharibifu mkubwa wa Miundombinu katika maeneo kadhaa. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itafanya kila liwezekanalo kurekebisha miundo mbinu ya barabara iliyoharibika. Tunatambua ghamama kubwa inayohitajika, lakini ni wajibu wetu kama Serikali kuhakikisha Wananchi wanapata huduma muhimu hasa za mawasiliano kati ya eneo moja na jingine.

(d) Maswali

Mheshimiwa Spika,

7. Leo tunahitimisha Mkutano wetu wa Pili wa Bunge tukiwa tumefanya shughuli mbalimbali ndani ya Bunge letu. Katika Mkutano wetu, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kuuliza maswali ya kawaada na yale ya papo papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Jumla ya maswali **115** ya msingi na **307** ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali.

(e) Mjadala wa Hotuba ya Rais

Mheshimiwa Spika,

8. Katika Mkutano huu moja ya agenda iliyochukua nafasi kubwa ni Hoja ya Serikali ya kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Mafuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hoja hiyo tuliihitimisha vizuri na kwa mafanikio makubwa. Kazi kubwa iliyoko mbele yetu ni kutekeleza yale tuliyokusudia kama wajibu wetu. Napenda kuwapongeza tena Waheshimiwa Wabunge wote kwa kushiriki katika mjadala wa Hotuba hiyo vizuri. Nichukue tena nafasi hii kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba michango ya Waheshimiwa Wabunge na maoni yao yatazingatiwa kwa utekelezaji.

II: MPANGO WA TAIFA WA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika,

9. Katika Mkutano huu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kujadili na kuidhinisha Mapendeleko ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa Fedha 2016/2017. Vilevile, Bunge limejadili na kutoa maoni na ushauri katika mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali katika mwaka wa Fedha, 2016/2017. Kipekee, naomba nimshukuru Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Philip Isdor Mpango(Mb) na Naibu wake Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb.) pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara za Kisikta kwa ufanuzi mzuri walioutoa wakati wa kuhitimisha hoja hii. Aidha, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mizuri, maoni na ushauri ambao Serikali itauzingatia katika kukamilisha maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika,

10. Naomba nami uniruhusu nitoe maelezo mafupi ya msisitizo katika maeneo machache yaliyopata michango mingi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja ya Serikali ya mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Waheshimiwa Wabunge wengi wamesisitiza kuhusu umuhimu wa Serikali kuongeza uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kuimarisha udhibiti wa matumizi ya Serikali. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wameishauri pia Serikali kuweka kipaumbele cha ujenzi wa Reli mpya ya Kati, kujenga uchumi wa Viwanda, kuanza na kusimamia ujenzi na Mitambo ya kuchakata gesi asilia (LNG) na Kiwanda cha Mbolea Mkoani Lindi, kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme Vijijiini, ujenzi wa Bandari Mtwara, kutatua changamoto zinazowakabili Wakulima na Wafugaji pamoja na Wachimbaji Madini.

Vilevile, kuweka mikakati thabiti ya utekelezaji wa Miradi ya Sekta za Elimu, Afya, Maji na huduma kwa wenyewe Ulemavu na pia kuzingatia utawala bora. Serikali inatambua kuwa maeneo haya ni muhimu sana katika kujenga uchumi imara na endelevu na pia kuondoa umasikini. Hivyo, itazingatia sana ushauri huu mzuri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika,

11. Naomba nitumie fursa hii kumpongoza Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa umahiri mkubwa na umakini alionenesha ikiwa ni mwanzo mzuri wa kuongoza Serikali ya Awamu ya Tano. Mheshimiwa Rais ameonesha kasi kubwa na dhamira ya dhati ya kuwatumikia Watanzania katika kujenga uchumi imara, unaokuwa na endelevu. Waheshimiwa Wabunge wengi watakulaliana nami kwamba Serikali ya Awamu ya Tano katika kipindi chake cha mwanzo cha siku 100, imeonesha dhahiri nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba makusanyo ya mapato yetu yanaongezeka. Jitihada hizo za kuongeza makusanyo ya mapato ya Serikali zimefafanuliwa vizuri kwenye Hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango. Serikali itaendelea na mikakati yake ya kuongeza Mapato yake na kudhibiti mianya ya kukwepa kodi. Ni matumaini

yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge, Wafanyabiashara na Wananchi wote wataunga mkono dhamira hiyo njema ya Serikali.

Mheshimiwa Spika,

12. Kuhusu matumizi, tayari Serikali imeanza kuchukua hatua thabitii za kudhibiti matumizi yasiyo na tija katika Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea na Taasisi zote za Umma pamoja Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Lengo la hatua zinazochukuliwa ni kuhakikisha kwamba Serikali inasimamia kwa umakini matumizi ya fedha za Umma ili zitumike ipasavyo kwa malengo yaliyokusudiwa. Hatua hizi zitaimarishwa zaidi katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika,

13. Kama nilivyoeleza awali hoja nyingi za msingi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu Mpango wa Taifa, zimefafanuliwa vizuri na Waheshimiwa Mawaziri wa Kisekta na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Naomba niwaahidi kuwa tutazizingatia katika mchakato wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/2017, kwa kadri itakavyowezekana. Waheshimiwa Wabunge watashirikishwa kikamilifu katika mchakato huo kupitia Kamati mbalimbali za Bunge. Serikali itafarijika sana kupata maoni na ushauri zaidi ili tuweze kuboresha mipango yetu ya muda mfupi na muda mrefu.

III: SEKTA YA KILIMO

Uzalishaji wa Mazao ya Chakula 2014/2015 na Upatikaji wa Chakula 2015/2016

Mheshimiwa spika,

14. Hali ya chakula kwa mwaka 2015/2016 katika maeneo mengi ya nchi imeendelea kuwa ya kuridhisha kufuatia mavuno mazuri yaliyopatikana msimu wa kilimo wa 2014/2015. Takwimu za Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuuvi zinaonesha kuwa albaki kutoka msimu uliopita nchi ilikuwa na ziada ya chakula licha ya kuwepo kwa maeneo machache ambayo hayakuwa na chakula.

Mheshimiwa Spika,

14. Kutokana na uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa 2014/2015 kuwa Tani millioni 15.5 na mahitaji ya chakula kwa mwaka 2015/2016 kuwa Tani milioni 12.9 hivyo nchi imejitoshleza kwa chakula kwa ziada ya **Tani milioni 2.5** sawa na asilimia **120**. Napenda kuwahakikisha Watanzania kuwa Serikali itaendelea kuhudumia maeneo yote yenye uhaba wa chakula.

Mheshimiwa Spika,

15. Pamoja na Taifa kuwa na ziada ya asilimia **120** ya chakula, tathmini ya hali ya chakula nchini inaonesha kuwa kuna Halmashauri **69** katika mikoa **18** nchini yenye maeneo yenye dalili za upungufu wa chakula. Maeneo hayo yapo

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

katika Mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Lindi, Singida, Tabora, Arusha, Geita, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Tanga, Simiyu, Mwanza, Morogoro, Iringa, Njombe, Mtwara, na Pwani.

Mheshimiwa Spika,

16. Ili kukabiliana na hali ya uhaba wa chakula katika maeneo hayo, Serikali inaendelea kutoa chakula katika maeneo hayo ambapo jumla ya **Tani 23,871.6** za chakula zilitengwa kwa ajili hiyo. Hadi kufikia tarehe 17 Januari, 2016, jumla ya **Tani 11,860.8** zilikuwa zimechukuliwa toka Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kwenda kwenye Halmashauri za Wilaya zenyenye upungufu wa chakula kwa ajili ya usambazaji. Natoa wito kwa Halmashauri ambazo hazijachukua mgao wao kufanya hivyo mara moja ili Wananchi katika maeneo hayo wasizidi kuathirika.

Mheshimiwa Spika,

17. Sambamba na utoaji wa chakula cha msaada, Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) inaendelea kutoa mahindi katika maghala ya Songea na Sumbawanga kwa ajili ya kuuzwa kwa wafanyakishara wa nafaka walioihinishwa na mikoa zenyenye uhaba wa Chakula. Lengo ni kuongeza upatikanaji wa chakula na kukabiliana na kasi ya kupanda kwa bei ya vyakula katika maeneo hayo. Chini ya utaratibu huo, vibali vimeshatolewa kwa wafanyakishara wa Mikoa **17**, vya kununua jumla ya **Tani 77,166**. Hadi kufikia tarehe 18 Januari, 2016 jumla ya **Tani 56,817.5** kati ya Tani 64,817.3 zilizokwa zimelipiwa kutoka NFRA tayari zilikuwa zimechukuliwa.

Mheshimiwa Spika,

18. Ili kuongeza na kuimarisha uhakika na usalama wa chakula hapa nchini, Serikali imelenga kujenga maghala **275** kwa awamu katika sehemu zenyenye uzalishaji mkubwa wa zao la mahindi ambapo hadi sasa jumla ya maghala **125** yanaendelea kujengwa na kukarabatiwa katika maeneo hayo. Aidha, Serikali kwa kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) inaendelea kujenga maghala ya kimkakati kwa ajili ya kuhifadhi akiba ya Taifa. Kwa sasa ghala moja lenye uwezo wa kuhifadhi **Tani 5,000** limeshajengwa Wilayani Mbozi Mkoani Mbeya. Aidha, Serikali imepata mkopo wenye masharti nafuu kutoka Serikali ya Poland ambao utawezesha kujenga vihenge vya kisasa (*silos*) vyenye uwezo wa kuhifadhi Tani 160,000 na maghala zenyenye uwezo wa kuhifadhi **Tani 90,000**.

Mheshimiwa Spika,

19. Pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali, ninawataka viongozi wa Mikoa, Wilaya na atendaji katika Halmashauri zote Nchini kuwahamasisha Wananchi kutumia vizuri mvua zinazonesha nchini kote kulima kwa bidii ili kuweza kuvuna na kuijiwekea akiba ya chakula cha kutosha kwa ajili ya kaya zao wakati wote wa mwaka. Aidha, wawahamashe wafanyakishara na

wadau wengine kusaidia Serikali kuchukua chakula kutoka maeneo yenyе ziada na kupeleka katika maeneo yenyе upungufu. Ni imani yangu kwamba tukizingatia maelekezo haya pamoja na juhudи za Serikali zilizooneshwa, tatizo la uhaba wa chakula nchini litapungua, kama siyo kumalizika kabisa.

IV: MIFUGO:

Hatua zilizochukulwa na Serikali katika Kushughulikia Migogoro ya Wakulima na Wafugaji;

Mheshimiwa Spika,

20. Migogoro ya ardhi hapa nchini ina sura nne; migogoro kati ya Wakulima na Wafugaji, mgogoro kati ya Wananchi na Wawekezaji; migogoro kati ya Wananchi na Serikali na migogoro kati ya Mamlaka moja na Mamlaka nyininge ndani ya Serikali. Migogoro hii imeenea nchi nzima kutokana na sababu mbalimbali ikiwepo kuongezeka kwa matumizi ya rasilimali ya ardhi.

21. Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi kwa kutumia Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 na Sheria ya matumizi ya Ardhi Na. 6 ya mwaka 2007, hadi kufikia mwezi Juni 2015 jumla ya Vijiji **620** katika Wilaya **81** kwenye Mikoa **22** zimeweza kutenga Hekta **Milioni 1.9** kwa ajili ya Wafugaji. Wito wangu kwa Wananchi na Wadau wa Kilimo na Ufugaji nawaomba kutunza na kuendeleza maeneo haya ili yaweze kutumika kwa mujibu wa malengo yaliyopangwa.

Mheshimiwa Spika,

22. Nitumie fursa hii pia kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu hatua ambazo Serikali imechukua kukabiliana na migogoro ya Wakulima na Wafugaji iliyotokea katika Mikoa ya Morogoro (Wilaya za Mvomero na Kilombero) na Manyara (Wilaya ya Kiteto). Katika kushughulikia tatizo hili, Jumla ya Vijiji **53** vimeainisha maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo Kilimo na Ufugaji. Aidha, jumla ya Mashamba Pori Manane (8) yameanishwa na orodha yake imewasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua za kufutiwa hati miliki na hatimaye kufanya utaratibu wa kuyatumia kwa ufugaji. Ni matarajio yangu kuwa maeneo haya yatapunguza kwa kiasi kikubwa matatizo ya uhaba wa malisho hapa Nchini. Wito wangu niwatake Viongozi wa Vijiji kusimamia vizuri matumizi ya maeneo yatakayotolewa kwa ajili ya malisho ili tatizo hili la kukosa maeneo ya malisho lisijirudie tena.

Mheshimiwa Spika,

23. Bado kuna mgogoro wa Wafugaji na Wakulima katika Bonde Oevu la Kilombero ambao umetafutiwa ufumbuzi kwa kuweka alama (*branding*) mifugo yote katika eneo hili ambapo jumla ya Mifugo **52,780** ilipata usajili wa Wilaya. Aidha, jumla ya Mifugo **24,586** imeondolewa katika eneo la Bonde la Kilombero.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa kuzingatia hatua zilizochukuliwa na Serikali Wananchi wanapaswa kufuata Sheria na kuhakikisha Mifugo hairudi tena katika maeneo yaliyokatazwa na kwamba maeneo haya yanahifadhiwa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika,

24. Mgogoro wa Wafugaji na Wakulima katika maeneo ya Kiteto ni wa muda mrefu na kwa bahati mbaya sana umeleta madhara makubwa kwa maisha ya Wanadamu na uharibifu wa mali. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Tume iliyoundwa na aliyekuwa Waziri Mkuu (Mstaafu) Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda imekamilisha hatua muhimu ya kuleta maelewanao na maridhiano katika pande zilizoathirika na mgogoro huo. Kwa sasa hali imeendelea kuimarika na tunaendelea kufuatilia kuhakikisha inakuwa shwari kwa muda wote.

25. Vilevile tarehe 29 Januari 2016 nimekutana na Viongozi wa Serikali, Halmashauri ya Wilaya na Chama kutoka Wilaya ya Kiteto hapa Dodoma ambapo nilipata fursa ya kupokea taarifa ya Tume niliyoitaja hivi punde. Nimeigiza Tume kuendelea na hatua iliyobakia ili kurejesha utulivu na amani kwa wananchi wa Kiteto. Hata hivyo, nimepanga kufanya ziara Wilayani Kiteto katika siku chanche zijazo ili niweze kukutana na Wananchi walioathirika na mgogoro huu na ikiwa ni pamoja na kujionea hali halisi Wilayani Kiteto. Wito wangu kwa ndugu zangu wa Kiteto ni kuwaomba waendelee kuvumilia wakati jitihada za Serikali katika kutatua migogoro hiyo inaendelea.

V: UTEKELEZAJI WA ELIMU MSINGI BILA MALIPO

Mheshimiwa Spika,

26. Tangu Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli atoe maaelezo ya utekelezaji wa elimumsingi bila malipo, kumekuwa na umuhimu wa kutoa elimu na ufanuzi zaidi juu ya utekelezaji wa agizo la elemu bila malipo kwa Watanzania kuanzia darasa la awali hadi Kidato cha Nne katika Shule za Umma. Hii ni hatua ya Serikali katika kuhakikisha uwepo wa fursa ya elimu bora kwa wote kwa kuwapunguzia mzigo wazazi na walezi kugharamia au kuchangia upatikanaji wa elimumsingi. Katika mpango huu, Serikali imedhamiria kuhakikisha kuwa mwanafunzi atasoma kuanzia darasa la awali hadi kidato cha Nne bila ya wazazi na walezi kulipa ada ya shule, għarama za mitihani na michango mballimbali. Hata hivyo, yapo majukumu ambayo yataendelea kutekelezwa na wazazi na walezi ambayo ni pamoja na kununua sare za shule na michezo, madaftari, kalamu na chakula kwa wanafunzi wa shule za kutwa. Maeneo mengine ni kulipia nauli ya kwenda na kurudi shule, na mahitaji mengine kama kununua godoro, shuka na vifaa vya usafi binafsi. Mzazi au mlezi ana wajibu wa kugharamia matibabu ya mtoto wake.

Mheshimiwa Spika,

27. Napenda nitumie nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote tushirikiane katika juhudzi za kuunga mkono uamuzi wa Serikali kuhusu elimu bila malipo. Aidha, nawaomba wote kwa ujumla wetu kushirikiana kuwaelimisha Wananchi wetu kuhusu utaratibu huu na wajibu wa kila mmoja wetu kama Mzazi/Mlezi, Serikali na jamii kuhusu utekelezaji wa zoezi hili. Nia yetu ni kuhakikisha Watanzania wanapata fursa ya kupata elimu bora kwa mtoto mwenye umri wa kwenda Shule na wote walioko katika Shule za Msingi na Sekondari. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kama tulivyo kwisha sema suala la ada elekezi inafanyiwa kazi na ikikamilika Wananchi watajulishwa kuhusu utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika;

28. Katika kutekeleza mpango huu, Serikali imetenga fedha shilingi **Bilioni 131.4** kuanzia mwezi Disemba 2015 hadi Juni, 2016, kuhudumia wanafunzi wa bweni kwa chakula, kufidia gharama za ada za mitihani, ada ya shule na kutoa fedha za uendeshaji wa shule (**Capitation Grants**). Aidha, kupitia Waraka wa Elimu Na. 5 wa mwaka 2015 Serikali imefuta michango yote iliyokuwa inachangishwa shuleni kwa idhini ya Kamati na Bodi za Shule.

Mheshimiwa Spika,

29. Tunatambua katika utekelezaji wa zoezi hili zipo changamoto zilizojitokeza. Kwa mfano, baadhi ya shule zenye wanafunzi wachache kupata fedha kidogo sana kwa kuwa ugawaji wa fedha unazingatia idadi ya wanafunzi. Lakini pia zipo changamoto katika kutoa chakula cha mchana kwa Wanafunzi wa kutwa na uendeshaji wa Hosteli ambazo wazazi na walezi au jamii walikuwa wanachangia fedha za chakula. Serikali inaendelea kuzifanyia kazi changamoto hizo zilizojitokeza katika utekelezaji wa mpango huu ikiwemo uelewa wa jamii na wadau kuhusu mpango mzima kwa ujumla wake.

VI: HUDUMA YA MIKOPO KWA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU

Mheshimiwa Spika,

30. Serikali imeendelea kutoa huduma ya mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo 2015/2016 kwa kuzingatia Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Namba 9 ya mwaka 2004 (Kama ilivyorekebishwa), Kanuni za Utoaji Mikopo za mwaka 2008, na Mwongozo wa utoaji Mikopo na Ruzuku kwa mwaka wa masomo 2015/2016. Hadi kufikia mwishoni mwa Januari 2016, Serikali ilikuwa imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi **Bilioni 207.9** kwa wanafunzi **122,786** wa elimu ya juu, wakiwemo wanafunzi wa mwaka wa kwanza **53,850** ambaao ni Asilimia **98.9** ya wanafunzi **55,254** walioomba mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika,

31. Ili Taifa liendelee kuwa na wataalamu wa kutosha katika nyanja muhimu, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele cha kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wanaodahiliwa katika programu za kipaumbele ikiwemo Sayansi za Tiba, Ualimu wa Sayansi na Hesabu, Uhandisi wa Mafuta na Gesi, Uhandisi Umwagiliaji, Sayansi za Kilimo, Wanyama na Ardhi. Aidha, Serikali inaendelea kufanya kazi mikakati ya kuimarisha urejeshaji wa mikopo pamoja na kuwa na vyanzo endelevu nya kupata fedha za kumudu ongezeko la wanafunzi wenye mahitaji ya mikopo.

VII: HALI YA USALAMA NCHINI

Mheshimiwa Spika,

32. Hali ya usalama katika Nchi yetu kwa ujumla ni shwari. Hata hivyo, katika kipindi hiki nchi yetu imekuwa ikitabili ana na changamoto ya ongezeko kubwa la Wakimbizi hususan katika Mkoa wa Kigoma. Kambi zetu zilizoko mikoa ya Kigoma, Katavi, Tabora na Tanga zinahifadhi wakimbizi wapatao **218,895** kutoka mataifa ya Burundi (**156,377**), Congo-DRC (**62,176**), Somalia (**150**) na Mataifa Mchanganyiko (**192**) kutoka nchi za Rwanda, Uganda, Sudani ya Kusini na Ethiopia. Kwa ujumla katika kipindi hiki wamepokelewa wakimbizi zaidi ya **122,267** kutoka Burundi. Aidha, hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2015 kambi mpya ya wakimbizi ya Nduta imepokea wakimbizi **38,994** wengi kati yao wamehamishiwa kutoka Kambi ya Nyarugusu na wachache wakiwa wameingia moja kwa moja kutokea Burundi.

Mheshimiwa Spika,

33. Kufuatia ujio wa wimbi kubwa la wakimbizi toka Burundi kumejitokeza matukio ya uhalifu wa kutumia silaha za moto ndani na nje ya kambi ya wakimbizi ya Nyarugusu. Aidha, kutohana na upekuzi na ukaguzi kwa wakimbizi unaofanywa kwa pamoja na vyombo nya dola sanjari na taarifa za ki-intelijensia imebainika kuwepo kwa askari waasi walokimbia pamoja na raia wa kawaida ambao wanajaribu kuwashawishi vijana kujisajili ili kuijunga na vikundi nya waasi. Nitoe wito kwa wananchi na wakimbizi kushirikiana na vyombo vyetu nya usalama kwa kutoa taarifa za uhalifu, hususan umiliki haramu wa silaha za moto kwenye Makambi na katika maeneo mbalimbali.

VIII: MPANGO ENDELEVU WA USAFI WA MAZINGIRA NCHNI,

Mheshimiwa Spika,

34. Mtakumbuka kuwa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, aliamua maadhimisho ya miaka 54 ya Uhuru ya terehe 9 Desemba, 2015 yafanyike kwa kufanya usafi wa mazingira katika maeneo ya Umma na maeneo yanayowazunguka. Kwa ujumla Wananchi, Taasisi za Umma na Binafsi ziliitikia agizo hilo na kushiriki kikamilifu katika zoezi hilo. Nichukue fursa hii kuwapongeza

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa dhati Wananchi, Taasisi za Umma na Binafsi wote kwa kushiriki katika zoezi hilo kikamilifu. Mlionesha moyo wa uzalendo na ari kwa nchi yenu. **Nawapongeza sana!**

Mheshimiwa Spika,

35. Usafi ni dhana muhimu katika kulinda afya za binadamu na kudhibiti magonjwa mbalimbali ya mlipuko ikiwemo kipindupindu. Ili kufanikisha lengo hili, kunahitajika juhudzi za makusudi na za pamoja katika usimamizi wa Sheria, Kanuni na Taratibu tulizojiwekea. Hivyo, Serikali imeamua kulifanya zoezi la usafi wa mazingira kuwa endelevu. Kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Serikali imetoa Waraka unaoelekeza kuwa kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi iwe siku maalum ya kufanya Usafi wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika,

36. Napenda kuendelea kusisitiza katika kila ngazi yaani Viongozi na Wananchi kutimiza wajibu wako kwa kuhakikisha zoezi hili linakuwa endelevu. Aidha, napenda kuwahimiza Viongozi wa Mkoa, Wilaya na Halmashauri kusimamia usafi wa mazingira katika maeneo yao ya utawala zoezi ambalo litakuwa linafanyika kila Jumamosi ya mwisho wa Mwezi. Kila Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Nchini awe na mikakati ya kudumu ya usafi ikiwa ni pamoja kuhakikisha kuwa kuna Sheria Ndogo za usafi wa mazingira na zinatekelezwa ipasavyo. Aidha, Halmashauri zote Nchini zihakikishe kuwa uchafu uliokusanywa katika maeneo mbalimbali unazolewa na kupelekwa katika maeneo mahususi ya dampo. Simamieni kikamilifu Wakandarasi waliopewa zabuni hizo na kuona wanatimiza wajibu wao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika,

37. Kama tulivyoona Usafi wa mazingira ni jukumu la kila Mwananchi na linapaswa kuwa endelevu. Rai yangu kwa Watanzania wote ni kujenga tabia ya kuhakikisha kuwa mahali pa kazi na mazingira yanayowazunguka yanakuwa safi wakati wote. Kufanya hivyo, kutasaidia kuimarisha usafi wa mazingira na kuboresha afya. Hali kadhalika kupunguza mlipuko wa magonjwa yakiwemo Kipindupindu.

38. Wito wangu kwa Wananchi ni kuona kuwa zoezi la usafi ni la kila mmoja wetu na kuepuka kuchafua mazingira kwa makusudi ikiwemo kuepuka tabia za kutupa taka hovyo wanapokuwa katika vyombo vyaa usafiri na pia kutofanya biashara katika maeneo yasiyoruhusiwa ili kuzuia kutupwa taka hovyo. Watendaji wa Mitaa na Kata na Vijiji kutimiza wajibu wao wa kuhakikisha maeneo wanayoyasimamia yanakuwa katika hali ya usafi. Nitumie fursa hii kuwahimiza Wananchi, Taasisi na Jumuiya zote kuhakikisha wanaweka mazingira katika hali ya usafi na pia kushiriki katika siku ya usafi kama iliyopangwa na Serikali.

IX: UHUSIANO WA KIMATAIFA

Mheshimiwa Spika,

39. Nchi yetu imeendelea kuwa kivutio kikubwa katika mahusiano baina ya Nchi na Nchi, Jumuiya za Kikanda na Kimataifa. Hii inatokana na Viongozi wetu ambao wamekuwa katika mstari wa mbele kudumisha mahusiano yetu katika Medani za Kimataifa. Yapo mambo mengi yaliyofanyika na yanayo endelea kufanyika kama mwendelezo wa kudumisha ushirikiano katika Jumuia hizi za Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika,

40. Kutokana na juhudzi za Viongozi wetu kutangaza Nchi yetu Kimataifa, ni hivi karibuni tu Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliteuliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Bwana Ban Ki-moon kuwa mmoja wa Wenyeviti wa jopo la ushauri la ngazi ya juu kuhusu Afya ya Mama na Mtoto (Every Woman, Every Child) Duniani. Hii ni heshima kubwa kwa nchi yetu kwa kuwa itaiweka Tanzania kuwa mionganini mwa mataifa yenye kuheshimika duniani. Aidha, uteuzi huu ni chachu ambayo inaleta matumaini mapya katika kukabiliana na changamoto za afya ya mama na mtoto, hususan katika nchi zinazoendelea kama Tanzania. Nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa uteuzi huo. Tunamuombea heri na baraka tele katika kutekeleza jukumu hilo kubwa la Kimataifa kwa maendeleo ya watu wetu.

X: KUIMARISHA UTENDAJI SERIKALINI NA MAADILI

Mheshimiwa Spika,

41. Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi imedhamiria kurejesha nidhamu na maadili ya Watendaji wa Serikali na Watumishi wa Umma katika kutoa huduma mbalimbali kwa Wananchi. Katika kuhakikisha Watumishi wa Umma na Watanzania wote wanafanya kazi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuja na kauli mbiu ya "**Hapa Kazi Tu**". Tafsiri ya falsafa hii ni kuwataka Watanzania wote katika nafasi mbalimbali walizopo kufanya kazi kwa bidii na kujiepusha na vitendo vya uzembe, urasimu na kutenda kazi kwa mazoea.

42. Aidha, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 **chini ya Ibara ya 22** inaainisha kuwa, kila **Mtu anayo haki ya kufanya kazi**. Vilevile, **Ibara ya 25** inafafanua kuwa kufanya kazi ndiyo njia pekee ya kumwezesha Mtanzania kupata utajiri na ndilo chimbuko la ustawi wa wananchi na ni kipimo cha utu.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wakati akihutubia Mkutano wa kwanza wa Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa maneno yake alisema, napenda kunukuu:-

“Serikali nitakayounda, nataka iwe inawahudumia Wananchi kwa haraka na sio kuwasumbua sumbu na kuwazungusha. Natoa rai kwa Watumishi wa Serikali, hasa amba ni wazembe na wavivu, kujandaa. Wamevumiliwa kwa muda mrefu sasa basi. Kwa sababu Watumishi wa aina hiyo hawatavumiliwa katika Serikali nitakayoiongoza. Lughu za “**Hiyo ni changamoto tutaishughulikia**” au “**Mchakato unaendelea**” hazitavumiliwa katika Serikali ya Awamu ya Tano. Mimi nataka watu wa **Kazi tu**. Hatuwezi kulea watu amba wanalipwa mishahara lakini hawafanyi kazi wanazotakiwa kufanya, au wamegeuza Ofisi za Umma kuwa ni mahala pa kuchuma bila kufanya kazi.” mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika,

43. Ili kutekeleza maneno ya Mheshimiwa Rais na kuhimiza matakwa ya Kikatiba, kila Mtanzania anapaswa kushiriki na kujituma kwa uaminifu katika kazi halali za uzalishaji mali. Aidha, kila Mwananchi anapaswa kuwa na nidhamu ya kazi na kuhakikisha anafikia malengo yaliyowekwa. Nitumie fursa hii pia kuwakumbusha Watumishi wa Umma kuwa wamepewa dhamana ya kuwahudumia Wananchi kwa niaba ya Serikali. Hivyo wanawajibika kuhakikisha wanawahudumia Wananchi kwa haki, weledi, uadilifu na kwa taaluma zao. Ni lazima wahakikishe kuwa wanatatua kero za Wananchi. Sio sahihi wananchi kuwasilisha kero zao kwa viongozi wa ngazi za kitaifa hasa wakati wa ziara ilihali viongozi wa mikoa na wilaya wapo katika maeneo hayo kwa wakati wote.

44. Tunatambua kuwa wapo Watumishi wanaotekeleza vyema majukumu yao. Lakini pia wapo Watumishi amba hawazingatii maadili ya kazi zao na pia wanafanya kazi kwa uzembe. Serikali haitaacha kuchukua hatua za nidhamu kwa watumishi wote wasio zingatia kikamilifu sheria, kanuni na taratibu katika Utumishi wa Umma. Aidha, kwa kuzingatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Viongozi na Watumishi wote wa Umma lazima tufanye kazi kwa kuzingatia weledi na kujiamini. Kila Mtu anapaswa kujitathmini kama dhamana aliyopewa anaitendea haki.

Mheshimiwa Spika,

45. Huu sasa ni wakati wa kufanya mabadiliko ya dhati katika utendaji na uadilifu. Kwa maana hiyo napenda kusisitiza mambo yafuatayo kwamba:-

- (i) Kila Kiongozi na Mamlaka ya nidhamu ni lazima kuwajibika kusimamia Utendaji na Maadili ya Kazi. Hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa wakati na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi. TUSIONE HAYA HATA MARA MOJA, CHUKUENI HATUA.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- (ii) Wananchi wahudumiwe ipasavyo na kwa weledi, haki, uadilifu na heshima. Mambo haya yakizingatiwa hakuna mwananchi atakayesafiri kutoka kijijiini, Wilayani au Mkoani kutafuta huduma Makao Makuu ya Wizara, Ofisi ya Waziri Mkuu au IKULU.
- (iii) Madawati ya malalamiko yawepo katika Ofisi za Umma. Aidha, tayari maelekezo yametolewa ya Watumishi wa Umma wazingatia utaratibu wa kuva vitambulisho vyenye majina yao kwa urahisi wa Wananchi kuwatambua wanapowahudumia. AGIZO HILI LITEKELEZWE.

Mheshimiwa Spika,

46. Ni kweli kwamba, Mheshimiwa Rais ametumia dhana ya “**kutumbua jipu**” kama dawa ya kusimamia uwajibikaji hasa katika wale wenye dalili ya kukosa maadili ya Utumishi wa Umma. Tafsiri ya dhana hii ya “**Kutumbua jipu**” inalenga katika kuwarejesha Watumishi wa Umma na walioko Serikalini katika mstari mzuri wa utendaji. Nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote kama tulivyo na kwa umaja wetu tuumunge mkono Mheshimiwa Rais katika vita hii kubwa ya “**Kutumbua Majipu**”. Tukiwa pamoja na kwa kushirikiana tutaweza kuibadilisha Nchi yetu kuwa Nchi ya maadili na yenye sifa ya juu katika utendaji wa Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika,

47. Aidha, naomba nisisitize kuwa Serikali ya Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli inaongozwa na Katiba, Sheria, Kanuni na Taratibu za Nchi. Vilevile inaheshimu na kuthamini haki za Watumishi wa Umma wa ngazi zote na inatambua mchango mkubwa unaotolewa na Watumishi wa Umma katika kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa. Kamwe, Serikali haitamwonea Mtumishi yejote wala kumnyanyasa. Lakini pia haitamvumilia Mtumishi mzembe na asiye timiza wajibu wake. Serikali itaendelea kuchukua hatua za kurejesha nidhamu kwa Watumishi wa Umma ili kuwezesha Nchi yetu kuwa na Utumishi wenye kuzingatia uadilifu na uliotukuka.

XI: HITIMISHO.

Mheshimiwa Spika,

48. Uzoefu nilioupata katika muda mfupi tuliookaa pamoja hapa Bungeni, nimegundua kuwa tuna Waheshimiwa Wabunge mahiri waliobobea katika nyanja mbalimbali. Wapo wasomi wa ngazi zote, Wazee kwa Vijana amba wana uzoefu na Utaalam mkubwa. Ni imani yangu kuwa tutatumia utaalam na uwezo mkubwa tulionao katika kuijenga Nchi yetu na kuwasaidia Watanzania kutoka hapa tulipo hadi hatua ya mbele katika kuleta maendeleo. Wananchi walio tuchagua wanatutegemea. Nawaomba tutangulize uzalendo katika kila jambo tufanyalo kwa manufaa ya Taifa letu na watu wake. Tufike mahali

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambapo kwa elimu, busara na hekima tulizonazo kuacha kabisa ushabiki wa kisiasa badala yake tutizame mbele katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Spika,

49. Napenda kuhitimisha Hotuba yangu kwa kurejea tena nilivyosema hapo awali kwamba, baada ya kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu kwa mafanikio makubwa, kazi kubwa iliyo mbele yetu ni kuijenga Nchi yetu kwa umaja na mshikamano. Nawaomba tuweke maslahi ya Watanzania na Taifa letu mbele. Tudumishe amani na utulivu. Tupuuze sera zozote za kudhoofisha utaifa wetu kama Watanzania na kutugawa kwa misingi yoyote ile, iwe ya kikabila, imani za dini, rangi au kwa itikadi za kisiasa. Dhamira yetu sote iwe ni kukuza uchumi wa Nchi yetu na kuondoa umaskini ili kuwaletea Wananchi wetu maendeleo na maisha mazuri.

50. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuhakikisha kuwa Tanzania inapiga hatua mbele. Tufanye kazi kwa bidii kuunga mkono kaulimbiu yetu ya "**Hapa ni Kazi Tu**". Aidha tutumie juhudhi, maarifa na ubunifu zaidi katika kila jambo. Mimi naamini kuwa kwa ushirikiano katika Bunge hili na Wananchi kwa ujumla tutaweza kutimiza matarajio ya Wananchi waliotuchagua na matarajio ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika,

51. Naomba nitumie nafasi hii tena kuwashukuru wote waliosaidia kufanikisha mkutano huu. Nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kutuongoza vizuri na kwa weledi mkubwa. Kipekee niwashukuru Wenyeviti wa Bunge ambao wamekalia kiti kwa mara ya kwanza lakini kwa weledi mkubwa, **Hongereni sana!!**

Mheshimiwa Spika,

52. Nitumie nafasi hii kumshukuru Katibu wa Bunge na Wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri ya kuhakikisha mkutano huu unakamilisha shughuli zake kama ilivyopangwa. Niwashukuru Wataalam wote wakiwemo Waandishi wa Habari kwa kazi nzuri waliyofanya kufanikisha Mkutano huu.

Mheshimiwa Spika,

53. Nimalizie kwa kuwatachia wote safari njema mnaporejea kwenye maeneo yenu ya kazi na katika majimbo yenu. Ninaamini kwamba, Mwenyezi Mungu atatulinda na kutuweka salama sote kama tulivyo hadi kukutana tena katika Mkutano ujao.

Mheshimiwa Spika,

54. Baada ya kusema hayo, naomba sasa kutoa Hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe **19 Aprili, 2016** saa **3:00** asubuhi litakapokutana katika Mkutano wa **Tatu** kwenye Ukumbi huu hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika,

55. Naomba kutoa Hoja.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Ninayo matangazo machache...

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, hujatuhaji.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane. Nina matangazo machache, tangazo mojawapo ni la udhuru wa Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Spika alienda Dar es Salaam kwa ajili ya kufuatilia mambo muhimu, yale yanayolihusu Bunge hili, ilikuwa arudi leo na kuwepo wakati huu tukahirisha Bunge lakini hataweza kufika kwa sababu bado hajamaliza kufuatilia hayo mambo. Anawatakia kikao chema na pia ameniagiza niwashukuru sana kwa kushiriki kwenu, kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais lakini pia amesema niwashukuru sana kwa mapendekezo na changamoto mbalimbali mlizozitoa wakati wa mjadala wa hoja ya Mapendekezo ya Mpango. Kwa hiyo, ametoa shukrani zake nyingi sana kwa kuibua changamoto ambazo zitaifanya Serikali ifanye kazi yake kwa ufanisi. (Makofii)

Pia Mheshimiwa Spika ameniomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kipindi hiki tukahirisha Bunge mkumbuke kuzipitia Kanuni kwa sababu kila mtu alipewa nakala ili Bunge letu liweze kuendeshwa vizuri. Vile vile amenituma niwakumbushe kuvumiliana kwa sababu wakati mwingine maneno yanayotumika yanakuwa hayamfurahishi kila mtu lakini cha msingi ni kuvumiliana. Aidha, ametaka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja zote zilizotolewa Serikali itazifanya kazi na yeche atazifua tilia kwa karibu.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine ni kuhusu ratiba iliyopo mbele yetu, kwa sababu kama mlivyomsikia Mheshimiwa Waziri Mkuu ametutangazia kwamba Mkutano wa Tatu wa Bunge ambaao ni Mkutano wa Bajeti utaanza tarehe 19 Aprili, 2016. Nitawasomea ratiba ya mpaka hiyo tarehe 19 Aprili, 2016, naomba mzi-note hizi tarehe. Pamoja na vikao vitakavyofanyika kuanzia tarehe 8 Februari, 2016 hadi tarehe 14 Februari, 2016, hizi tarehe nadhani mlishaambiwa kwenye Kamati zenu kwamba mtakuwa mkikaa Dar es Salaam lakini zipo tarehe nyingine ambazo ni muhimu mziweke katika kumbukumbu zenu.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 14 - 27 Machi, 2016, ukihesabu hiki kipindi kitakuwa ni cha siku 14, kutakuwa na vikao vya Kamati za Bunge mahsus kwa ajili ya kazi za kawaida za Kamati. Vikao hivi vitafanyika Jijini Dar es Salaam.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 29 Machi, 2016 kwa mujibu wa Kanuni ya 96 ya Kanuni za Bunge, Serikali itawasilisha dondo na randama za vitabu vya bajeti kwa mwaka 2016/2017.

Tarehe 30 Machi, 2016, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(2) na (2) ya Kanuni za Bunge, kutakuwa na Mkutano wa Wabunge wote ambapo Serikali itawasilisha Mapendekezo ya Mpango na kiwango cha ukomo wa bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Mkutano huu utafanyika Dar es Salaam.

Tarehe 31 Machi, 2016 - 6 Aprili, 2016, kwa mujibu wa Kanuni ya 97(4), kwa kipindi cha siku saba, Kamati ya Bajeti itafanya uchambuzi wa mapendekezo ya mpango na kiwango cha ukomo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 baada ya kuwasilishwa kwa Wabunge wote.

Aidha katika kipindi hicho, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati za Kudumu za Kisekta zitatembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Tarehe hizo ni tarehe 31 Machi, 2016 - 6 Aprili, 2016. Wakati Kamati ya Bajeti inaangalia Mapendekezo ya Mpango, Kamati nyingine za Kisekta zitakuwa zikikagua miradi.

Tarehe 7 - 15 Aprili, 2016, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge kwa kipindi cha siku tisa, Kamati za Kudumu za Kisekta zitachambua taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hizo.

Tarehe 15 Aprili, 2016, kwa mujibu wa kanuni ya 98(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kutafanyika kikao cha pamoja kati ya Kamati ya Uongozi na Kamati ya Bajeti ili kujadili mambo muhimu yaliyojitezea kwenye Kamati za Kisekta wakati wa kujadili utekelezaji wa bajeti za Wizara mbalimbali. Kwa hivyo, Wajumbe wa Kamati ya Uongozi na Wajumbe wa Kamati ya Bajeti tarehe 15 Aprili, 2016 watakatana kwa ajili ya shughuli hiyo.

Mwisho, tarehe 16 na 17 Aprili, 2016, Wabunge wataelekea Dodoma tayari kwa shughuli za Mkutano wa Tatu wa Bunge ambao utaanza tarehe 19 Aprili, 2016.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa wengi wakitoka hapa wataelekea maeneo yao, tarehe 8 Februari, wote wanatakiwa kuwa Dar es Salaam kwa mujibu wa hii ratiba tuliyosoma. Kama umeifuatilia mapumziko kidogo yatakuwa kati ya tarehe 14 Februari, 2016 mpaka 14 Machi, 2016.

Tangazo lingine ni kuhusu uchaguzi wa uongozi wa Tawi la Commonwealth Parliamentary Association. Nimetaarifiwa kwamba walikutana

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

leo tarehe 5 Februari, 2016 katika ukumbi wa Spika, Ofisi ya Bunge Dodoma. Pamoja na mambo mengine, Kamati hiyo ilifanya uchaguzi wa viongozi wa tawi ikiwemo nafasi ya Mwenyekiti na Makamu wake.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa matokeo ya uchaguzi huu, naomba kuwataarifu kwamba waliochaguliwa ni wafuatao: Mwenyekiti wa Tawi atakuwa ni Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni na Makamu Mwenyekiti atakuwa Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu. Tangazo hili limetolewa na Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi, Mheshimiwa John John Mnyika aliomba Mwongozo kuhusu maelezo ambayo yalitolewa katika Bunge la Kumi kuhusu usambazaji na upatikanaji wa maji. Kwa maana ya kwamba Bunge la Kumi kulikuwa na makubaliano, kwa mujibu wa maelezo aliyotoa. Aliomba Mwongozo kwamba hoja ya kuahirisha Bunge ipo lakini hakuona taarifa kuhusu usambazaji wa maji na upatikanaji wake kama ambavyo ilikuwa ikifanyika katika Bunge la Kumi.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wangu kuhusu suala hili ni kama ifuatavyo. Ni kweli kwamba Bunge la Kumi lilitoliza uhai wake Julai, 2015 aliyekuwa Waziri wa Maji katika Serikali ya Awamu ya Nne, aliweka utaratibu wa kutoa maelezo kwa njia mbalimbali ikiwemo njia hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Mnyika. Hata hivyo, utaratibu huo haukuwa maamuzi ya Bunge bali ni ahadi ya Serikali kwa wakati huo. Bunge hili la Kumi na Moja litakuwa linaweka utaratibu wake wa namna bora ya kufikisha maelezo kwa Waheshimiwa Wabunge kwa nyakati tofauti. Hivyo, Serikali itakapokuwa tayari itawafahamisha Wabunge utaratibu wake wa kuafikishia taarifa kuhusu suala la maji.

Waheshimiwa Wabunge, tusimame tuimbe Wimbo wa Taifa.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Naibu Spika, hujatuhoji kuhusu hoja ya kuahirisha Bunge.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtahojiwa, naomba tusimame tuimbe Wimbo wa Taifa.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Sasa nawahoji kuhusu hoja ya Waziri Mkuu ya Kuahirisha Bunge mpaka tarehe aliyoitaja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nadhani waliosema ndiyo wameshinda. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Tuhesabu. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Bunge mpaka tarehe aliyoitaja Waziri Mkuu ambayo ni terehe 19 Aprili, 2016.

*(Saa 10.52 Jioni Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 19 Aprili, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*